JACKPOT BABA LAO!
TZS. 374,935,160
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

## RIPOTI MAALUM -2
Hivi ndivyo ilivyo hali ngumu ya wakazi Monduli





UKURASA 13

# Nipashe
Jumanne Novemba 1, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581116
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## WATU MIL. 61.7
# MZIGO MKUBWA

**SAMIA** ashtuka, wataalamu wachambua kwa kina, watoa angalizo... *Endelea Uk. 2 na 3*






MAJENGO: MILIONI 14.34



ZAHANATI: 7,889



VITUO VYA AFYA: 1,490



HOSPITALI: 688




S/MSINGI: 19,769



SEKONDARI: 5,857






**MICHEZO** YANGA YAAPA KUIMALIZA MECHI CAF KWA MKAPA UK. 32

**KATUNI** UK. 6

SENSA 2022

# Samia: Huu ni mzigo mkubwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA




Rais Samia Suluhu Hassan akionyesha kibao chenye idadi ya watu nchini baada ya kuzindua rasmi matokeo ya awali ya sensa ya watu na makazi 2022 katika hafla iliyofanyika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametangaza matokeo ya mwanzo ya Sensa ya Watu na Makazi kwa Mwaka 2022, akibainisha idadi ya Watanzania ni milioni 61.74, wanawake wakiwa milioni 31.6 sawa na asilimia 51.

Vilevile, Rais Samia amesema idadi hiyo ni mzigo mkubwa kwa taifa, hivyo lazima kuwapo mikakati madhubuti ya mipango ya maendeleo ya kuwahudumia kwa kuwa makadirio yanaonyesha ifikapo mwaka 2025, Tanzania itakuwa na watu milioni 67.96.

Akizindua matokeo hayo na mwongozo wa kitaifa wa matumizi ya matokeo hayo jijini hapo jana, Rais Samia alisema sensa hiyo imefuata vigezo vyote vya kimataifa na Tanzania ina watu milioni 61.74. Kati yao, milioni 59.85 wapo Tanzania Bara na milioni 1.88 wapo Tanzania Zanzibar.

"Kati yao, wanawake ni milioni 31.68 sawa na asilimia 51, tunaposema wanawake ni jeshi kubwa, wanaume wa Tanzania, simba wetu ni milioni 30.5 sawa na asilimia 49 ya watu wote," alitangaza matokeo ya sensa hiyo.

Rais Samia alisema kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita Tanzania ilikuwa na idadi ya watu milioni 44.92, hivyo kuna ongezeko la watu milioni 16.81 sawa na ongezeko la asilimia 3.2 kati ya mwaka 2012 na 2022.

"Kwa hiyo, bado tunaweza kwenda na kasi ile ile ya ukuaji wa watu ya milioni 3.2, kwa Tanzania Bara idadi ya watu imeongezeka kutoka milioni 43.62 mwaka 2012 hadi watu milioni 59.85 kwa mwaka 2022. Kwa Zanzibar idadi ya watu imeongezeka kutoka milioni 1.3 mwaka 2012 hadi milioni 1.8 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 3.7," alisema.

Aliongeza kuwa Zanzibar imetia fora kwa ongezeko la watu ingawa idadi yao ni ndogo.

Kuhusu takwimu za mikoa, Rais Samia alibainisha kuwa mikoa yenye idadi kubwa ya watu inaongozwa na Dar es Salaam yenye watu 5,383,728 sawa na asilimia 8.7 ya watu wote nchini, akitamka "ndio maana panapotokea upungufu wa chochote, malalamiko yanakuwa mengi huko kwa sababu ya wingi huo".

"Mkoa unaofuata ni Mwanza wenye watu 3,699,872 sawa na asilimia sita ya watu wote nchini. Kwa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi unaongoza kwa kuwa na watu 893,169 sawa na asilimia 47.3 ya wakazi wote wa Zanzibar ukifuatiwa na Mkoa wa Kaskazini Pemba ambao una watu 272,091 sawa na asilimia 14.4," alifafanua.

Akizungumzia kuhusu sensa ya majengo, Rais Samia alisema Tanzania ina jumla ya majengo milioni 14.34 ambapo kati yake, Tanzania Bara ni milioni 13.9 na Tanzania Zanzibar ni 440,421.

"Huduma za kijamii, vituo vya afya ni 10,067 ambapo zahanati 7,889, vituo vya afya 1,490, hospitali 688. Kwa upande wa elimu matokeo yanaonyesha Tanzania ina shule 25,626 ambapo za msingi ni 19,769 na sekondari ni 5,857," alisema.

"Inawezekana idadi hiyo ikawa si tatizo la kuumiza kichwa kwa nchi kubwa kama yetu, lakini ni mzigo mkubwa kwa taifa letu, jamii na uchumi kwa ajili ya kuwahudumia, kuanzia sasa lazima kuwapo mikakati madhubuti ya mipango ya maendeleo ya jinsi ya kuwahudumia watu hao," alihadharisha.

Rais Samia pia alitoa angalizo kuwa mwaka 2050 inakadiriwa Tanzania itakuwa na watu milioni 151.2.

Alitoa wito kwa viongozi na Watanzania kutumia taarifa hizo kwa madhumuni yaliyokusudiwa ya kuboresha maisha ya kila Mtanzania.

"Serikali imeandaa mwongozo wa kitaifa wa matumizi ya sensa ya watu na makazi kwa mwaka 2022 ili kutumika katika kutunga kutekeleza sera na mipango ya maendeleo ya kisekta katika ngazi zote za utawala, na ni wa kwanza kuandaliwa tangu tulipopata uhuru na ni wa kwanza katika Bara la Afrika," alisema.

Alisema lengo la mwongozo huo ni kuongeza uelewa na uwazi wa matumizi ya sensa ya mwaka huu kwa wadau wote hususan serikali kwenye kupanga mipango jumuishi ya kijamii, kiuchumi na kimazingira.

"Mwongozo utatekelezwa kwa miaka 10 kuanzia Novemba 2022 hadi Oktoba 2032, elimu ya matumizi ya matokeo ya sensa itatolewa kwa wananchi wote.

"Unaeleza kwamba kuna wajibu wa kila mdau kutumia matokeo ya sensa kwa wadau wote, utasaidia kufuatilia na kutathmini malengo yaliyowekwa katika mipango ya kitaifa ya maendeleo kwa pande zote za muungano tuliyopanga kutekeleza, tutafanyiwa tathmini kupitia mwongozo huu," alisema.

Rais aliagiza matokeo hayo yatumike katika kupanga miradi ya wananchi, bajeti, sekta binafsi na wawekezaji wote kwa mipango jumuishi na endelevu kwa taifa.

Alisema kuwa katika sensa hiyo zimepatikana takwimu za idadi ya majengo yote nchini na anuani za makazi.

"Taarifa hizi zina umuhimu mkubwa wa kufuatilia kuweka sera na mipango miji ya kuwezesha kufikia wananchi wanapoishi kwa urahisi zaidi ili kuwapatia huduma za kijamii," alisema.

Rais Samia alisema taarifa ya Umoja wa Mataifa ya mwaka huu kuhusu matokeo ya idadi ya watu duniani kulinganisha na mwaka 2012 ambao dunia ilikuwa na watu bilioni saba, inabainisha idadi inatarajiwa kuongezeka hadi kufikia watu bilioni nane mwaka huu.

"Hili ni ongezeko la watu bilioni moja katika kipindi cha miaka 10, taarifa hiyo inaonesha kuwa mwaka 2022 barani Afrika katika nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara, lina watu bilioni 1.2 na inakadiriwa kuongezeka hadi kufikia bilioni 2.1 ifikapo mwaka 2050," alisema.

Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema mwongozo huo utaongeza wigo wa matumizi ya takwimu katika upangaji wa maendeleo nchini.

Alisema dhamira ya dhati na serikali zote mbili ni kuhakikisha wanatumia vyema rasilimali zilizoko na kufanya uamuzi sahihi katika kupanga na kutekeleza mipango.

Waziri Mkuu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Sensa, Kassim Majaliwa, alisema sensa ya mwaka huu imekuwa na mafanikio kuliko sensa yoyote iliyowahi kufanyika kutokana na matumizi ya teknolojia na hamasa ya wananchi kuhesabiwa.

Awali, Kamisaa wa Sensa, Anne Makinda alisema ni wakati mwafaka kwa Watanzania kutumia takwimu za Ofisi ya Takwimu ya Takwimu na kuacha mambo mengine yasiyo muhimu wa kufanya kazi kwa weledi mkubwa.

Alisema matokeo yatakayotolewa yanatokana na uchambuzi wa maswali machache kati ya maswali 100 yaliyoulizwa na kujibiwa katika sensa hiyo.

Akitoa maelezo mafupi kuhusu sensa, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema sensa imefanyika kwa ufanisi mkubwa na imekwenda sambamba na miongozo ya Umoja wa Mataifa.

"Tunaomba Mheshimiwa Rais uendelee na utashi wa kisiasa wa mwongozo wa matumizi ya takwimu za sensa ili ulete majawabu kwa wananchi wetu.

"Nitoe mfano mdogo kwenye benki zetu, kinamama na vijana tunakwenda kwenye mikopo, hatutahitaji masharti magumu ya kutoa hati za viwanja, kupitia sensa ya anuani za makazi tumechukua takwimu zote za wafanyabiashara wadogo, biashara zao zipo sehemu gani.

"Kwa hiyo, ni rahisi sekta hii ya kibenki kutoa mikopo ya kutosha kwa kinamama ili kujikwamua kiuchumi na kuongeza vipato vyao," alisema.

Alisema kazi iliyobaki kwa sasa kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ni kufanya uchambuzi wa kina kwa masuala ya elimu, shughuli za kikazi, makazi ya watu wanayoishi, mazingira yao na itashirikisha watu wote ili matokeo hayo yafanyiwe uchambuzi wa kina na kuingia kwenye sera za nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alisema idadi hiyo itasaidia kujipanga zaidi na kufanya maandalizi kwenye madarasa na vituo vya kutolea huduma za afya ili wapate mahitaji muhimu.

## MATOKEO YA SENSA 2022



Rais Samia Suluhu Hassan akimkabidhi Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, vitabu vya matokeo ya mwanzo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 pamoja Kitabu cha Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Matokeo ya Sensa wakati wa uzinduzi jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Wataalamu watoa angalizo kasi ya ongezeko la watu

**Na Waandishi Wetu**

WATAALAMU wa sekta mbalimbali wametoa maoni yao kuhusu ongezeko la watu nchini, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza jana Tanzania ina watu milioni 61.74, wakitaja matokeo chanya na hasi ya ongezeko hilo.

Mchambuzi wa masuala mbalimbali, Dk. Nasibu Mramba alisema kwa sasa zimepatikana takwimu sahihi za idadi ya watu zitakazosaidia kwenye mipango ya maendeleo badala ya kuenenda kwa makisio.

"Katika kuangalia ukuaji wa nchi upo kwa kiasi gani au kipato cha mtu ni kiasi gani, tunapoangalia uchumi kwa ujumla tunagawanya na idadi ya watu. Kama unakosea idadi ya watu, unapata jibu ambalo sio sahihi. Kwa sasa ukisema kipato cha mtu ni kiasi gani kwa mwaka unakuwa upo sahihi.

"Idadi yetu inaongezeka kwa asilimia 3.2 kwa miaka 10, tunatakiwa kuhakikisha kwenye kila miaka 10 vitu vinaongezeka kwa asilimia hiyo. Kwa mfano, kama ni barabara ziongezeke kwa asilimia angalau tatu, shule, vituo vya afya, yaani kila kitu kiangalie watu watakavyokuwa wanaongezeka," alisema.

Mtaalamu huyo alisema kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoitoa kuwa kuna umuhimu wa kuzaa kwa mpango, ina tija kwa nchi.

"Sio Tanzania tu, ukilinganisha dunia na Afrika, idadi ya watu inaongezeka sana Afrika. Sasa ongezeko la watu lina faida na hasara. Kwa upande wa faida unapata nguvukazi na hasara ni kwamba inatakiwa ukuaji huo uende sambamba na ukuaji wa rasilimali, lakini kuna rasilimali huwa hazikui ikiwamo ardhi, hivyo tuzae kwa mpango.

Ofisa Mipango Miji wa Jiji la Dodoma, Azor William, alisema ongezeko la watu linatengeneza mahitaji, akifafanua: "Unatakiwa uwe na huduma za kijamii - shule, afya, miundombinu, makazi, huduma za maji, umeme na vitu vyote vinahusiana na ardhi. Kwa hiyo, wakiongezeka wanahitaji shule kadhaa ziongezeke, vituo vya afya viongezeke."

Alisema ardhi huwa haikui wala kuongezeka na madhara ya ongezeko hilo zipo kwenye mazingira, uchumi na jamii.

"Kwenye mazingira ongezeko la watu, kama mipango miji haijafanyika, inaweza kusababisha kuibuka kwa makazi holela, migogoro ya ardhi, watu kuvamia maeneo ya watu, watu kutokuwa na sehemu za kutupa taka," alisema.

Kuhusu faida, alisema ongezeko hilo linatengeneza fursa nyingi za uhitaji wa makazi yaliyopangwa vizuri, fursa za uwekezaji wa shule, masoko makubwa na biashara kukua.

**PROFESA UDSM**

Profesa aliyebobea katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Pius Yanda, alisema ongezeko hilo la watu litasababisha uhitaji mkubwa wa huduma za kijamii ikiwamo maji, ardhi na chakula ambazo nazo upatikanaji wake tayari umeshaanza kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

"Tunaona hizo rasilimali nazo zina changamoto. Kwa mfano, huwezi kuzalisha chakula kama mvua haitabiriki na hakuna ardhi ya kutosha. Kwa sasa tunapitia changamoto ya ukame na uharibifu wa mazingira ikiwamo mmomonyoko wa udongo," alifafanua.

Prof. Yanda alisema kutokana na ongezeko hilo la watu, ni wazo sehemu kubwa ya ardhi itatumika kwa ajili ya kilimo, ikizingatia kuwa asili ya kilimo nchini imejikita zaidi kwenye ardhi kwa kuwa jamii haina uwezo wa kulima kisasa.

Alisema ongezeko hilo pia litachangia uharibifu wa mazingira kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu ikiwamo kukata miti kwa ajili ya nishati kama kuni na mkaa pamoja na kujenga nyumba kwa ajili ya makazi.

Prof. Yanda alisema nchi itegemee idadi kubwa ya watu kuhama kutoka vijijini kwenda mijini, wakiamini watapata kazi na maisha yao kuwa mazuri, hali itakayoongeza ugumu wa upatikanaji wa huduma za kijamii.

"Mfano mzuri ni sasa ambapo upatikanaji wa maji umeshaanza kuwa wa shida, kwa sababu yaliyoko hayatoshelezi kukidhi mahitaji ya wakazi wote, hivyo kusababisha kuwapo na mgawo," alifafanua.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, Dk. Fabian Massaga, alisema mfumo wa huduma za afya ulivyo nchini kuanzia vituo vya kata, hospitali za wilaya hadi hospitali za rufani umetengenezwa kulingana na idadi ya watu inayohudumiwa na wataalamu wataokuwapo katika vituo husika.

Alisema kuongezeka kwa idadi ya watu nchini kuna maana kwamba hata utoaji huduma za afya unatakiwa kuongeza watoa huduma, vitendea kazi na miundombinu ili kutoa huduma iliyo bora kwa watu wote.

"Unajua kuna idadi ambayo inaelekeza kwa siku daktari aone wagonjwa wangapi, hivyo hapo lazima waongezeke nao, pia kwenye miundombinu. Tunashukuru tayari tulikuwa tumeshaanza kujiandaa, hivyo vyote vitaongezeka," alisema.

Daktari katika Kituo cha Afya, Daudi Zimulinda alisema ongezeko hilo la watu linachangia gharama za utoaji wa huduma za afya kuongezeka, hivyo bajeti ya serikali kwenye huduma za afya inabidi iongezeke ili kukidhi mahitaji ya wananchi.

Alisema elimu ya afya itolewe kwa wingi ili kupunguza magonjwa ya mlipuko na mengine ili kusaidia vituo visizidiwe na wagonjwa.

"Pia lishe bora izingatiwe, matumizi ya pombe na matendo hatarishi kwa afya yaepukwe, itasaidia kuepukana na magonjwa ya mara kwa mara kwa watoto na watu wazima," alisema huku akiitaka jamii kuzingatia uzazi wa mpango ili kupunguza idadi ya wanawake wanaohitaji kupata huduma za uzazi katika vituo vya afya.

Profesa wa Uchumi Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Razack Lokina, akichangia hoja hiyo baada ya kutafutwa na Nipashe jana, alisema: "Ongezeko hilo la watu litakuwa na faida inayoambatana na uzalishaji wa kijamii kuongezeka.

"Ongezeko la watu nchini lina maana ya kuwa na uhakika wa soko la ndani la bidhaa. Wakati imefika sasa kwa jamii kuongeza shughuli za uzalishaji ili watu wasomeshwe, wapate afya bora ili waweze kuchangia vyema Pato la Taifa".

***Imeandaliwa na Neema Emmanuel (MWANZA), Augusta Njoji (DODOMA), Jenifer Gilla (DAR) na Christina Haule (MOROGORO)**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA NISHATI**

**Telegramu "NISHATI".**
**Simu Namba: +255 26 2322018**
**Nukushi: +255 26 2320148**
**Barua pepe: ps@nishati.go.tz**

**Mji wa Serikali-Mtumba,**
**Mtaa wa Nishati,**
**S. L. P. 2494,**
**40474 DODOMA.**

**TAREHE: 27.10.2022**

**UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

Kwa mujibu wa kifungu cha 8(2) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, Waziri wa Nishati, Mhe. January Y. Makamba (Mb) amewateua wafuatao kuwa wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa **miaka minne** kuanzia tarehe **20 Oktoba 2022.** Hatua hii inakuja baada ya Rais kumteua Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, Profesa, Mark J. Mwandosya, tarehe **15 Agosti 2022.**

1. Bw. Fadhili J. Manongi – Mjumbe
2. Bi. Victoria M. Elangwa – Mjumbe
3. Bw. Haruna S. Masebu – Mjumbe
4. Dkt. James A. Mwainyekule – Mjumbe
5. Mha. Ngosi X. Mwihava – Mjumbe
6. Mha. Modestus M. Lumato – Mjumbe na Mkurugenzi Mkuu

**IMETOLEWA NA**
**MHA. FELCHESMI J. MRAMBA**
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA NISHATI**

MATOKEO YA SENSA YA SITA TANZANIA SENSA 2022

21717102

BAA LA UKAME

# Hivi ndivyo ilivyo hali wakazi Monduli

**Na Elizabeth Zaya** aliyekuwa MONDULI

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, iliangazia madhila yanayowapata wakazi wa kata za Lepurko na Sepeko wilayani Monduli mkoani Arusha ambao wanalazimika kuchuja maji yenye tope kwa kutumia majivu kutokana na ukame uliolikumba eneo hilo. Endelea kufuatilia kujua undani wa mustakabali wake.**

---

Mwenyekiti wa Kijiji cha Lepurko, Lendo Melambuki, anabainisha kijiji chake kina wakazi takriban 1,130 na walikuwa wanategemea maji kutoka Bwawa la Losikito ambalo nalo limekauka tangu Julai mwaka huu kutokana na ukame.

"Kwa sasa wakazi wa hapa Lepurko wanahangaika kutembea umbali mrefu kwenda Nanja kufuata maji. Haya tunayoletewa na serikali ya dharura ya ndoo moja kwa kila kaya, ni kidogo sana hayatoshelezi mahitaji. Tunahitaji maji ambayo yatakuwa ya kudumu kama ilivyo kwa maeneo mengine nchini," Melambuki anawasilisha kilio chao.

**HATUA SERIKALINI**

Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inaelekeza: "Lengo kuu la serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi". Katika hilo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nanja, Christopher Konyava, anasema wanaangalia kama maji hayo ya dharura yatasaidia, akisisitiza kila kitu huwa kina mwanzo mgumu.

Konyava anasema serikali imeonesha mikakati iliyonayo kwa ajili ya kumaliza tatizo la maji katika eneo hilo.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Monduli, Neville Msaki, anasema tathmini yao imebaini vijiji vinane vya kata mbili za wilaya hiyo (Lepurko na Sepeko) vimeathirika zaidi na ukosefu wa maji.

"Tulifanya tathmini na kugundua vijiji vinane vimeathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na vyanzo vyote vya karibu kukauka na tukaomba fedha serikali kuu, tukapewa Sh. milioni 100 kutekeleza mpango wa dharura kwa mwezi mmoja.

"Na kama hali hii ikiendelea itabidi tuombe tena na kwa sasa tunapeleka lita 60,000 kila siku katika vijiji vilivyoathirika na mpaka sasa tunasambaza maji kwa vijiji vinane vya kata mbili.

"Hali si shwari na vyanzo vyote vya maji vimekauka, hakuna kinachofanya kazi. Wilaya ya Monduli ina vyanzo vya maji 64 na kati yake, 61 vimekauka. Vitatu ambavyo ni mabwawa, navyo vinaelekea ukiongoni kukauka kutokana na kuzidiwa uwezo wa matumizi na udongo kujaa," Msaki anafafanua.



Utekelezaji wa mradi wa maji katika Jiji la Arusha ukiendelea. Mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 520 unatarajiwa kutatua tatizo la uhaba wa maji jijini humo na viunga vyake ikiwamo Wilaya ya Monduli.

Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Frank Mwaisumbe, anakiri athari za ukame katika wilaya hiyo ni kubwa na katika kuzikabili, wameanza kuchukua hatua za dharura, ikiwamo kugawa maji kwa kila kaya.

"Athari za ukame kwa Monduli ni kubwa ukizingatia kuwa eneo kubwa la wilaya hii ni miamba na karibu nusu yake haiwezi kutunza maji ingawa kwa upande mwingine eneo kama la Mto wa Mbu na Monduli Juu ni maeneo ambayo yana uwezo wa kuhifadhi maji, tofauti na sehemu nyingine zinazobaki ambazo ardhi yake ni kavu. Kwa hiyo, tuna ukame mkubwa.

"Vilevile, uharibifu wa mazingira katika wilaya hii ni mkubwa sana kutokana na wingi wa mifugo tuliyonayo na kutokuheshimu kutunza mazingira, kupeleka mifugo kwenye vyanzo vichache vya maji tulivyonavyo na hata kwenye maeneo ambayo yangesaidia kuleta mvua kama misitu ambayo mingi imeharibiwa sana na mifugo.

"Na kwa sababu hiyo, tumekumbwa na baa kubwa la ukame. Kwa miaka miwili mfululizo, vyanzo vingi vya maji na hata chemchemi zote zimekauka," anabainisha.

Mwaisumbe anasema serikali inatekeleza mpango wa muda mrefu, wa kati na wa dharura kutatua tatizo la maji katika wilaya hiyo.

"Mpango wa muda mrefu ni kumaliza kabisa tatizo la maji katika wilaya hii na tuna mradi mkubwa ambao utakamilika Desemba mwaka huu ambao unaanzia Ngaramtoni wa Sh. bilioni 520. Mradi huu utakuwa na tawi linalokuja Monduli ambalo gharama yake ni karibu Sh. bilioni 30 na huo ni mpango wa muda mrefu.

"Lakini mpango wa muda wa kati ni visima ambavyo tumepata fedha Sh. milioni 600 kwa ajili ya visima 12 ambavyo tutavichimba katika maeneo yenye ukame mkubwa zaidi na kazi hiyo imeanza. Mkandarasi yuko site

> "Mpango wa dharura wa kwanza ni huu ambao serikali imetoa Sh. milioni 100 kwa ajili ya kununua matangi ya kupeleka maji katika vijiji vinane vyenye hali mbaya ambavyo havina maji kabisa.

(eneo la mradi) na baadhi ya maeneo vimechimbwa, tunasubiri fedha za usambazaji wa maji kutoka katika hivyo visima.

"Lakini kwa sasa tuna dharura na mpango wa dharura wa kwanza ni huu ambao serikali imetoa Sh. milioni 100 kwa ajili ya kununua matangi ya kupeleka maji katika vijiji vinane vyenye hali mbaya ambavyo havina maji kabisa, hivi ndivyo vyenye hali mbaya sana.

"Tunafanya hivyo kwa sababu tunaogopa kunaweza kutokea magonjwa ya mlipuko na ndiyo maana tukachukua tahadhari hizo za haraka na serikali kupitia Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, imeidhinisha fedha hizo ili kuwapatia maji wananchi," anafafanua.

Mkuu wa Wilaya huyo anabainisha hili ni juma la tatu tangu waanze kupeleka maji hayo ya dharura kwenye vijiji hivyo vinane na wameomba fedha zaidi serikalini kutekeleza mpango huo wa dharura.

"Na kwa sababu hatujui dharura hii itaisha lini, tumeomba fedha nyingine Sh. bilioni nne kwa Wizara ya Maji watusaidie ili tusambaze maji yanayotoka katika visima tulivyovichimba lakini kuna vyanzo vingine ambavyo vina maji ya mtiririko ambavyo havihitaji gharama kubwa, vitatusaidia sana katika kusambaza maji na kuleta ahueni kwa wananchi wa Monduli," Mwaisumbe anabainisha mikakati yao.

**KAULI YA WAZIRI**

Akiwa jijini Arusha jana kukagua maendeleo ya mradi mkubwa wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 520, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliyefuatana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, alisema mradi huo ukikamilika, utatatua tatizo la uhaba wa maji katika jiji hilo na viunga vyake, ikiwamo Wilaya ya Monduli.

Mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2017, ukitarajiwa kukamilika Juni mwakani ukihusisha uchimbaji wa visima virefu 56.

Aweso alibainisha kuwa kwa sasa Jiji la Arusha linazalisha lita milioni 35 za maji huku mahitaji ya maji yakiwa lita milioni 109 kwa siku na baada ya kukamilika kwa mradi huo, shida ya maji katika jiji hilo na viunga vyake itakwisha kwa kuwa mradi huo una uwezo wa kuzalisha lita milioni 200 kwa siku.

Katika kukabiliana na hali mbaya iliyoripotiwa Monduli, Waziri Aweso alisema wako katika hatua za kutafuta mkandarasi atakayesambaza maji kwenye wilaya hiyo na maeneo ya jirani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christine Ishengoma, alisema maeneo mengi nchini kwa sasa yanakabiliwa na shida ya uhaba wa maji, akitaka serikali kuchukua hatua, ikiwamo kushughulikia mgawo wa umeme ambalo alisisitiza umeathiri kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wakiwamo wa Mkoa wa Arusha.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), katika utabiri wake wa Septemba mwaka jana, pia wa Aprili mwaka huu, ilibainisha kuwapo kwa ukame na joto kali na hivyo kuathiri baadhi ya shughuli za kiuchumi zikiwamo za kilimo na ufugaji.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso

## TANGAZO


A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO
DRINKING WATER
FURAHIA MAISHA
NA MAJI ASILIA
500ml
1000ml
1500ml
6L
12L
18.9L
+255 659 536 937, +255 758 979 641, +255 659 785 276
kdw@bbl.co.tz
kilimanjarodrinkingwater
kilimanjaro_drinking_water
617072202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ratiba mgawo maji isipendelee maeneo, wananchi wanaumia

**WIKI** iliyopita Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alitangaza rasmi kuwapo kwa mgawo wa maji katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

Sababu ya kuwapo kwa mgawo huo ni vyanzo vya maji vinavyozalishwa na mtambo wa Ruvu Juu na Ruvu Chini kuwa na upungufu mkubwa wa maji kutokana na ukosefu wa mvua za kutosha.

Wakati akitangaza hatua hiyo, Makalla alionya kusiwe na upendeleo wowote wakati mgawo huo utakapokuwa ukiendeshwa.

Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo wananchi wana masikitiko makubwa kwa kuwa tangu mgawo huo ulipoanza wana wiki moja sasa hawajapata maji.

Pamoja na ratiba kutolewa na kuonesha maeneo na mgawo utakavyoendeshwa, lakini haifuatwi na wananchi kuendelea kuteseka.

Kwa mfano wananchi wanaoishi maeneo ya Bungu, Boko na Tegeta, hawajapata maji kwa wiki moja sasa na matokeo yake wanahangaika kutafuta hata yasiyo salama ili yaweze kuwasaidia shughuli za nyumbani kama kufulia, kusafisha vyoo na nyingine ambazo hazitaathiri afya zao.

Maji ya kunywa wanalazimika kununua yanayotengenezwa na kampuni zinazozalisha maji hayo ili kunusuru afya zao na magonjwa ya milipuko.

Kila mmoja anaelewa mabadiliko ya tabianchi yamesababisha madhara yote hayo kutokea kutokana na kuathiri mvua kunyesha na kusababisha vyanzo vya maji kupungua kwa kiasi kikubwa.

Lakini, ombi la wananchi ni mgawo huo usiumize watu au kuwakomoa kwa kuwafungia maji kwa wiki nzima bila kutoka.

Kama kuna sababu nyingine inayofanya mgawo huo kutozingatia ratiba, ni bora wananchi wakaambiwa ukweli kuliko kuwaacha wakilalamika na kuilaumu serikali yao.

Baadhi ya wananchi wanachojua kila kitu kipo ndani ya uwezo wa serikali, hawaelewi kuwa vitu vingine vinasababishwa na mabadiliko ya tabianchi ambayo hiyo serikali yao haiwezi kuzuia.

Kutopata huduma ya maji kwa muda mrefu kunaweza kusababisha majanga mengine ya magonjwa kwa sababu ya kukosekana usafi.

Magonjwa kama corona yanakingwa kwa kuwa kwenye mazingira safi yakiwamo ya kunawa mikono kila wakati.

Tusije kushangaa mlipuko wa magonjwa ya kipindupindu nayo yakalipuka kwa kukosekana kwa huduma ya majisafi na salama.

Chonde chonde, mamlaka zinazohusika na huduma ya maji mgawo usisahau maeneo mengine kwa kuteseka wiki nzima bila kupata huduma hiyo.

Ukosefu wa maji huzua migogoro, kwa mfano mtu ana tangi lake amehifadhi maji yake na jirani yake hana hata ndoo ya kunywa, anapokwenda kumuomba na akinyimwa, lazima atamchukia kwa kutomsaidia.

Aliyehifadhi maji yake anaogopa kuyagawa kwasababu hajui lini atapata maji mengine kutokana na ratiba kutoeleweka.

Kukosekana kwa ratiba ya mgawo usioeleweka husababisha pia watu kushindwa kulala vizuri kwa kuvizia labda yatatoka usiku mwingi.

Wengine wanategesha mabomba kwa kuyafungua ili yakitoka wasikose hata hiyo ndoo moja. Lakini kwa hali ilivyo sasa, ukifungua mabomba hata ule mlio unaotoa matumaini kuwa maji yapo njiani yanakuja haupo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




### Muungwana Lazima Nilonge

## Fursa Kiswahili tunakula kwa kuona

Na Miki Taseni

**NCHI** za Afrika Mashariki zinaingia katika hatua nyingine za kujipambanua zinavyoendana na lugha ya Kiswahili, na mielekeo ya kisera au kiitikadi kuhusu matumizi ya lugha hii. Kimsingi unaweza kusema ipo mielekeo ya aina mbili, mwelekeo hasi wa kujifungia ndani ya Kiswahili unaofuatwa na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Asasi rafiki kwa mwelekeo huo, kama Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hawa ndiyo wadau wakuu wa lugha hii Bara.

Mwelekeo nwingine ni chanya, unaofuatwa na taasisi ya ufundishaji lugha kadhaa za kimataifa yenye maskani yake eneo la uwanja wa mpira wa Amaan jijini Zanzibar hiyo ni ZOI, ilijipambanua kwa wasikilizaji wa redio mojawapo jijini Dar es Salaam kuelezea mantiki ya kile inachokifanya, hasa kulenga kuinua fursa kwa kutumia lugha. Pia ilitoa vielelezo mahiri vya ufundishaji wake na msikilizaji anapata picha haraka ni wapi utaalamu huo unahitajiwa au unaweza kutumika. Kiswahili ni sehemu ya nyenzo zao; lengo lao siyo ukuzaji wa Kiswahili, ni kuzielewa lugha tofauti.

Washiriki mjadala huo redioni walikiri kuwa Kenya ina mikakati makini ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi, na hata wanapotakiwa waalimu wa lugha hiyo kwa mfano katika mkakati mpya nchini Uganda, na hata DRC, Kenya ndiyo inatazamiwa kutoa waalimu wengi. Sababu ni kuwa itakuwa rahisi kwa mwalimu kutoka Kenya kuongea Kiingereza kwa ufasaha ili afundishe Kiswahili au ajifunze Kifaransa kwa haraka akafundishe Kiswahili DRC. Huku Bara hakuna mwamko wa kuendana na lugha nyingine.

Mada yenyewe ya redioni kwa upande wa wataalamu wa BAKITA ilikuwa kielelezo tosha cha mwelekeo wake, wakijadili kuandikwa mabango ya biashara kwa lugha ya Kiingereza jijini au nchini kwa jumla. Hapakuwa na tofauti zozote miongoni mwao kuhusu uchanya wa matumizi hayo, ila masikitiko kuwa tunakuza lugha ya wenzetu na kuacha lugha yetu. Cha kushangaza ni kuwa mwelekeo wa kutaka kusiwe na matumizi mapana ya Kiingereza hapa nchini unataka wengine duniani wajifunze Kiswahili, wakati watajifunza kama lugha ya nyongeza, iwe ni kwa ajili ya ufanisi kibiashara au ni mwamko tu wa kitamaduni au fasihi, fasheni.

Hoja hii inaonyesha aina fulani ya uchoyo wa kiitikadi ambao si jambo geni hapa Dar es Salaam, ndiyo maana nyimbo za muziki wa dansi kuwasifu viongozi wa nje (hasa barani Afrika) zimeimbwa hasa na wageni, kwa mfano wanamuziki kutoka Zaire, baadaye DRC. Ni nadra kuona jina mataa hapa jijini la mtu ambaye hakuwa kiongozi wa juu kitaifa (rais, waziri mkuu) na hata hapo yapo yanayokosekana, na kwa mawaziri ndiyo kabisa hakuna. Wazee wa mitaa na manispaa kwa mfano Sinza wamejaza mitaa majina ya wanyama, badala ya viongozi kuanzia uhuru, hivyo kuna mitaa ya swala, punda, ng'ombe, si Salim Ahmed Salum wala John Malecela, au Cleopa Msuya na Mosses Nnawie.

Suala hapa ni kuwa utamaduni wa aina hii ni sehemu ya kile kinachozuia ari ya kwenda mbele kitaifa, tunaona tukishiriki kutumia Kiingereza itakuwa taabu kuwa tunawaenzi, au kununua bidhaa yao ya lugha. Kuwa nchi hii imepata faida ngapi za kuwapo lugha hiyo?

Wataalamu wa BAKITA wanalilia matumizi ya Kiswahili na kinachofanyika nchini, wahitajike kunyoosha lugha, kutafsiri na mahitaji kama hayo, hivyo hawataki ushindani wa Kiingereza ndani ya nchi yao ya Kiswahili. Tatizo ni kuwa Kiswahili kilitumika kama nyenzo ya utawala wakati Wajerumani walipounda 'Deutsch Ostafrika,' na ikawa endelevu hata leo.

Ndiyo hapo unapata picha kuwa wale wenye furaha tele na mwingiliano wa lugha uliopo sasa watachangamkia fursa na kustawi, tena kama taasisi binafsi za kibiashara na siyo wanaotegemea bajeti ya serikali kuwakoromea Watanzania kuwa Kiswahili kiwe ndiyo kila kitu. Wakati wanangoja 'mkono uanguke' wapate mlo, wenzao wanaojua soko na mahitaji ya lugha sokoni, ndani na nje ya nchi, watakuwa wanachanja mbuga. Wakiamka kumekucha, tunajua lugha nyingi na utalii unakuzwa na wanaojua lugha za wageni kutoka nchi hizo, wawatembeze na kuwapa maelezo ya kina. Siyo apatikane mkalimani anayejua Kiswahili awaelezee, katu.

# Shaka: Watanzania wote tumuunge mkono Samia

Na Mwandishi Wetu

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, amesema ni muhimu Watanzania wote wakamuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na kazi kubwa anayoifanya kuleta maendeleo nchini.

Shaka aliyasema hayo juzi Msalato mkoani Dodoma alipokuwa akijibu maswali ya waandishi wa habari waliotaka kujua ni kwa kiasi gani CCM inaridhishwa na utekelezaji wa Ilani yake ya Uchaguzi (2020-2025).

Aliulizwa maswali hayo baada ya Rais Samia kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato mkoani humo.

"Wote tuna jukumu la kujenga nchi bila kuangalia itikadi zetu za kisiasa. Haya yanayofanyika ni kwa maslahi mapana ya Watanzania. Ni imani yetu kwamba wenzetu wa vyama vingine wataunga mkono jitihada hizi.

"Ni kweli Ilani inayotekelezwa ni ya Chama Cha Mapinduzi lakini maendeleo yanayoletwa ni ya Watanzania wote kwa ujumla. Kwa hiyo nitoe wito tumeanza vizuri, Mheshimiwa Rais tangu ameingia madarakani ametuunganisha pamoja. Tunakwenda vizuri kikubwa ni kuendelea kusisitiza kuwa umoja wetu ndio ushindi wetu," alisema.

Aidha, Shaka alisema kuimarika kwa ujenzi wa miradi ya kimkakati ni kufungua fursa za kiuchumi kwa Watanzania hivyo ana imani kwamba wananchi watatumia vyema fursa ambazo zinatolewa na serikali ya CCM.




Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, akionesha ufunguo kama ishara ya uzinduzi wa jengo la Maalim Seif Makao Makuu ya chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ukarabati MV. Kazi wafikia 80%

Na Mwandishi Wetu

UKARABATI wa kivuko cha MV. Kazi kinachofanya safari kati ya Magogoni na Kigamboni jijini Dar es Salaam, umekamilika kwa asilimia 80 na mwezi ujao kinatarajia kurejea kuanza kutoa huduma mwezi ujao.

Kivuko hicho kiliondolewa rasmi kwenye maji mwishoni mwa Februari, mwaka huu, baada ya kufikia muda wake wa ukarabati na ni miaka mitatu hadi mitano tangu kianze kutoa huduma.

Hayo yalibainishwa na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), Lazaro Kilahala, mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika yadi ya Songoro, Kigamboni, Dar es Salaam ambako kivuko hicho kinaendelea kufanyiwa ukarabati.

"Tumefanya ukaguzi wa mwisho takribani mwezi mmoja uliopita. Kikubwa kilichokuwa kinasubiriwa ni vifaa kwa sababu ile kazi sehemu kubwa ilikuwa kufunga vifaa vipya vya injini, gia boksi na mifumo mipya ya injini.

"Kwa hiyo zile kazi ambazo zilikuwa zinaweza kufanyika kabla ya vifaa hivyo ilikuwa zaidi ya asilimia 80 na zote zilifanyika ikiwamo kuondoa vipande vya bati ambavyo vimeharibika na kupiga rangi upya," alisema.

Awali, Mwakilishi wa Songoro Marine, Hamad Aweso, alisema ukarabati wa kivuko hicho umefikia hatua nzuri na kwamba kuna vifaa ambavyo vilichelewa kufika kwa wakati zikiwamo injini za kivuko hicho. Alisema kwa sasa vifaa hivyo vimeshafika, hivyo kazi iliyobaki ni kuvifunga ili kivuko kirejee kutoa huduma.

"Kwa sasa hivi zoezi linaloendelea ni la kufunga hizi injini na kwa hali inavyoendelea, tunategemea mwisho wa Novemba zoezi zima litakuwa limekamilika na chombo kitakuwa kimekwishaingizwa majini," alisema.

Kivuko cha MV. Kazi kina uwezo wa kubeba abiria 800 na magari 22 sawa na tani 170 na tangu kuondolewa kwake, eneo la Magogoni Kigamboni limebakia na vivuko viwili vinavyotoa huduma ambavyo ni MV. Magogoni na MV. Kigamboni. Vivuko hivyo vinasaidiana na vivuko viwili kutoka kampuni ya Azam Marine kutoa huduma eneo hilo.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **STICK UP AUCTION MART, BROVITAS COMPANY LIMITED, MANGWEMBE 2011.CO LTD na INDEPENDENT AGENCIES & COURT BROKERS LTD** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD**. Ikiwa wahusika watashindwa kufanya malipo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| | NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|---|
| | BROVITAS COMPANY LIMITED | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | FLORA B KOMBA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | NAMTUMBO - RUVUMA |
| 2 | STEVEN JOVINUS NGONYANI | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI, KIWANJA NA 1044, KITALU DD | BOMBAMBALI - SONGEA |
| | | NYUMBA YENYE HATI MILIKI KIWANJA NA.393, KITALU SS- MALI YA JOSEPH MENDRAD NSWILA | MKUZO-MSAMALA - SONGEA |
| | INDEPENDENT AGENCIES & COURT BROKERS LTD | | |
| 4 | SAMAMBA J BWIRE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI KIWANJA NO.1346, KITALU J | HIMO-MOSHI |
| 5 | RABIEL R MDIMU | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAZUZIANO | MABOGONI-MOSHI |
| 6 | KOLMAN J MASSAWE | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MOITA KPOK-ARUSHA |
| 7 | ALIMINI KIDESI MSAHANI | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | ILAITAYOK-ARUSHA |
| 8 | SALUM J NEHEMIA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO NA KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | ENGOSENGEU NA MURIET-MOROMBO-ARUSHA |
| 9 | MZEJU PETER URIO | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAZUZIANO | MAJANI YA CHAI-ARUSHA |
| 10 | MARY B SHAYO | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | ERANAGAU-ARUSHA |
| 11 | LUCAS MEDA FRANSIS | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KANGE-TANGA |
| | STICK UP AUCTION MART | | |
| 12 | HAWA HASSAN MSANGI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | BARABARA YA AFRIKA MASHARIKI - ARUSHA |
| 13 | EDGAR PETER SILAYO | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MASHARIKI-MURIETI-ENGARAU-ARUSHA |
| | MANGWEMBE 2011 CO LTD | | |
| 14 | MOHAMED MICHAEL KITUNGULU | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI KIWANJA NO.94, KITALU M | KIBAONI - IFAKARA |
| 15 | HASSAN NASSORO AMIR | GHALA LENYE HATI MILIKI KIWANJA NO.184, KITALU E | UPOGORO - IFAKARA |
| 16 | ABUGA MORIS MPUNDUGA | NYUMBA AMBAYO HAIJAKAMILIKA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBASA, MJIMWEMA - IFAKARA |
| 17 | JOYCE WINIFRIDA MANYUKA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MANGWALE - IFAKARA |
| 18 | TWAHA S TEMA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBASA - IFAKARA |
| 19 | BAHATI MASALA LUBAZU | NYUMBA YA WAGENI YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBASA - IFAKARA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipwa kulingana na makubaliano ya benki na mnunuzi.Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Stick up Auction Mart**
**S.L.P Arusha**
**Namba za simu: 0786559593**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji.**
**Mangwembe 2011.CO.LTD**
**S.L.P**
**Namba za simu; 0752632033**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Independent agencies & court broker's ltd**
**S.L.P Moshi**
**Namba za simu: 0716264733**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Brovitas Company Limited**
**S.LP Songea**
**Namba za simu; 0763801591**

**NA**

**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**Namba za simu: 0768790399, 0754774949**

217126202



Baadhi ya wajasiriamali wa Kata ya Majohe wakiwa katika shamba darasa la mboga linalomilikiwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wakijifunza jinsi ya kulima kilimo bora cha bustani za mboga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# LHRC yachambua miswada itakayojadiliwa bungeni

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimekuja na mapendekezo kadhaa kwa ajili ya kusaidia kuboresha miswada minne inayotarajiwa kupitishwa kuwa sheria katika Mkutano wa Nne wa Bunge la 12.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, aliitaja miswada hiyo kuwa ni wa Bima ya Afya kwa Wote 2022, Ulinzi wa Taarifa Binafsi 2022, Marekebisho ya Sheria Mbalimbali No.3 2022 na Sheria ya Uwekezaji 2022.

Kuhusu Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote 2022, alisema kituo hicho kinapongeza serikali kuleta mswada huo, kwa kuwa imekuwa kilio cha wadau cha siku nyingi na kwamba utasaidia wananchi katika kuwapunguzia mzigo wa gharama za matibabu.

"Hata hivyo, muswada huu una vifungu tata na vinavyoweza kusababisha uvunjifu wa haki za binadamu au kusababisha changamoto katika utekelezaji wake, kwa mfano kifungu cha 3 kinatoa tafsiri ya neno mtu asiye na uwezo lakini kwa bahati mbaya hakijadadavua vigezo vya mtu asiye na uwezo ni vipi na mtu asiye na uwezo ni nani," alisema.

Henga alisema kutokana na utata huo, LHRC inatoa wito kwa serikali kabla Bunge halijaahirishwa, kanuni hizo ziwasilishwe mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, zipitiwe ili kuona kama hazikinzani na sheria mama, kwa kuwa uzoefu unaonyesha kwamba kanuni nyingi zinazotungwa na mamlaka mbalimbali wakiwamo mawaziri hukinzana na sheria mama.

Aliongeza kuwa hata taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ya mwaka 2020 ilionyesha hivyo na kituo kinampongeza Waziri wa Afya kwa kukubali kufanya hivyo.

"Kifungu cha 20(1), kifungu hiki kinaweka takwa la lazima kwa mwajiri kuwasilisha jina la mwajiriwa wake kwa skimu ya bima ya afya ndani ya siku 30 tangu aliposaini nae mkataba wa ajira," alisema.

Alifafanua kuwa LHRC inaona muda huo ni mdogo, ambapo inapendekeza ziwe siku 60, ili kumpa mwajiri muda wa kukamilisha taratibu zake za ndani, na kwamba kifungu cha 21(2) kinapendekeza kumpa mamlaka ya kutunga kanuni waziri mwenye dhamana ya afya zitakazoweka takwa la lazima kwa kila Mtanzania kuwa na Bima ya Afya.

"Tunapendekeza kiongezwe kifungu kidogo cha (3) kitakachoeleza ni namna gani na mikakati gani itachukuliwa na serikali, ili kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa na bima ya afya bila kuhusisha matumizi ya nguvu," alisema.

Aidha alisema; "badala ya kujificha kwenye kichaka cha kanuni, tunapendekeza pia kanuni hizo zifanyiwe mapitio na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, ili kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara pindi Bunge linapopitisha sheria fulani ambapo sheria mama huonekana kuwa na ahueni kuliko kanuni."

Alisema kifungu cha 22(2), kinapendekeza watu wote wasio na uwezo watakuwa na haki za kuwa na bima ya afya, ambapo utaratibu wake utaainishwa kwenye kanuni na mwenye dhamana ya afya.

"LHRC tunapendekeza kiongezwe kifungu kidogo cha (4) ambacho kitaeleza watu wasio na uwezo ni kina nani na vigezo vya kuwapata watu hao badala ya kujificha kwenye kichaka cha kanuni," alisema.

Alizidi kusema kifungu cha 22(3), kinapendekeza vyanzo vya mapato vya kuhakikisha wanaoitwa watu wasio na uwezo vinaainishwa baada ya waziri mwenye dhamana ya afya kushauriana na waziri mwenye dhamana ya fedha.

Mkurugenzi Mtendaji huyo aliongeza kuwa kifungu cha 32, kinapendekeza kufungamanishwa kwa mifumo mingine ya kiserikali kama takwa la lazima kwa kila Mtanzania kuwa na bima ya afya, na kwamba kama kifungu hicho kitapita kama kilivyo, Mtanzania hatoweza kupata huduma mbalimbali hadi anamiliki kadi ya Bima ya Afya.

Henga alisema LHRC inapendekeza kifungu hicho kifutwe, kwa madai kwamba kitasababisha lekea uvunjifu wa haki nyinginezo za msingi ikiwamo elimu, kufanya kazi, kupata habari, kuishi, uhuru wa mtu kwenda atakako, kutambuliwa kama raia na haki nyingine zinazofanana na hizo.

Kuhusu Muswada wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi 2022, alisema kifungu cha 14, cha Muswada kinapendekeza takwa la lazima kwa taasisi zote zinazojishughulisha na ukusanyaji, uchakataji na udhibiti wa taarifa binafsi kusajiliwa na tume ya ulinzi wa taarifa binafsi ambapo kifungu cha 16 cha muswada kinaweka bayana kuwa kipindi cha usajili kitakuwa cha miaka mitano, huku kukiwa na nafasi ya kusajili tena, na kwamba katika kifungu hicho, taasisi zote za serikali zinazojishughulisha na ukusanyaji, uchakataji na udhibiti wa taarifa zitatafasiriwa kama zimesajiliwa baada ya sheria hiyo kuanza kutumika.

# Bunge labaini kikwazo kipya upatikanaji maji

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christine Ishengoma, amesema mgawo wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini, umeathiri kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi likiwamo Jiji la Arusha.

Kutokana na hali hiyo, kiongozi huyo amesema kamati yake itawasiliana na Waziri wa Nishati, January Makamba ili kutafuta suluhu dhidi ya mgawo wa umeme ambao umeshika kasi katika maeneo mengi nchini na kuathiri upatikanaji wa huduma muhimu kwa jamii. Dk. Ishengoma alibainisha hayo jana jijini hapa wakati wa ziara ya siku moja ya kamati hiyo kukagua miradi inayotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Arusha (AUWASA).

Alisema maji ni moja ya huduma muhimu katika jamii, akisisitiza haiwezekani serikali ilete mradi mkubwa wa zaidi ya Sh. bilioni 520 katika Jiji la Arusha halafu wananchi waendelee kukosa maji kutokana na umeme unaokatwa mara kwa mara.

"Sisi kama kamati tunataka kuona miradi ya maji nchini, kama huu wa AUWSA, ikiwa na matokeo chanya kwa wananchi kwa sababu maji ni hitaji muhimu katika jamii.

"Lakini kikwazo hapa ni umeme unakatika mara kwa mara na tumeliona hili na tutawasiliana na TANESCO (Shirika la Umeme) kupitia waziri mwenye dhamana ili kuona ni namna bora ya kutatua changamoto hii," alisema.

Dk. Ishengoma pia alisema kamati hiyo imeridhishwa na maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 520 unaohusisha uchimbaji wa visima virefu pamoja na ujenzi ofisi za kanda za AUWSA ambazo zimejengwa Moshono, Lemara na Murieti jijini hapo.

Alisema lengo ni kusogeza huduma kwa wananchi, ukiambatana na ujenzi wa mabwawa 18 ya kutibu majitaka yaliyoko Kata ya Terati, kituo cha kusukuma maji Na. 5 eneo la Chekereni pamoja na tangi la kupokea maji lita milioni 10 lililojengwa eneo na Ngaramtoni. Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliyefuatana na kamati hiyo, alisema kwa sasa Jiji la Arusha linazalisha lita milioni 35 huku mahitaji ya maji yakiwa lita milioni 109 kwa siku na baada ya kukamilika kwa mradi huo, shida ya uhaba wa maji katika Jiji la Arusha na viunga vyake itakwisha kwa kuwa mradi huo una uwezo wa kuzalisha lita milioni 200 kwa siku.

Kuhusu kuchelewa kwa mradi huo, Aweso alisema ni kutokana na mlipuko wa homa ya mapafu (COVID-19) uliosababisha vifaa vilivyoagizwa kutoka nje ya nchi kutokufika kwa wakati kwa sababu viwanda vilifungwa.

"Kikwazo kingine ni msamaha wa kodi kwa makandarasi na ugumu wa kuomba kuongezwa muda pamoja na ugumu wa miamba nyakati za uchimbaji wa visima," alifafanua.

Waziri Aweso alitaja kikwazo kikubwa kinachoukabili mradi huo kwa sasa ni mgawo wa umeme, unaosababisha baadhi ya maeneo kukosa maji katika Jiji la Arusha kwa kuwa mitambo ya AUWSA ya kusukuma maji ni mikubwa na si rahisi kuendeshwa kwa jenereta.

Awali mradi huo ulioanza mwaka 2017, ulipangwa kukamilika Desemba 31, mwaka huu, lakini sasa unatarajiwa kukamilika Juni mwakani.

## Operesheni kusaidia w'biashara kupatiwa leseni

Na Julieth Mkireri, KIBAHA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kibaha inatarajia kuanza operesheni sehemu za biashara kubaini kama kuna wafanyabiashara wasio na leseni ili wapatiwe.

Hayo yameelezwa wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo kuwa kwa kufanya hivyo itasaidia kuongeza mapato.

Akizungumza katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kibaha, Erasto Makala, alisema oparesheni hiyo itakuwa ni endelevu na kwamba timu ya mapato itashiriki moja kwa moja.

Makala alisema, lengo la operesheni hiyo ni kuhakikisha wanaongeza makusanyo ya mapato kupitia leseni za biashara.

"Katika operesheni hii wale wafanyabiashara ambao hawana leseni watapatiwa fedha zitakazopatikana hapa zitasaidia kuondoa vikwazo," alisema.

Aidha, alisema kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2023 hakutakuwa na chaguo la pili kwa kuwa kwasasa wameanza kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa kulingana na fedha waliyopata.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kibaha alisema wamepokea Sh. milioni 340 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 17 ili kuwezesha wanafunzi watakaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 2023 wote kupata nafasi.

Katika maeneo ambayo yanadaiwa kuwa na vikwazo vya upungufu wa vyumba vya madarasa aliwashauri madiwani kuwahamasisha wananchi kushirikishwa kuchangia kuanza ujenzi na serikali itatenga fedha kukamilisha.

**"Katika operesheni hii wale wafanyabiashara ambao hawana leseni watapatiwa fedha zitakazopatikana hapa zitasaidia kuondoa vikwazo," alisema.**

# Utetezi kesi ya Zumaridi wakwama kusikilizwa

Na Pelucy Yohana, SAUT

MSHTAKIWA namba sita, Suzana Simon katika kesi inayomkabili, Dian Bundala maarufu mfalme Zumaridi, amekwama kufikishwa mahakamani na kusababisha utetezi kukwama kusikilizwa.

Mshtakiwa huyo katika kesi namba 10, anadaiwa kubaki mahabusu huku kukiwa hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na Magereza kuhusu sababu ya kutofikishwa mahakamani.

Wakili wa upande wa utetezi, Amri Linus, alidai mahakamani kuwa mshtakiwa huyo hakufikishwa mahakamani na hawajapewa sababu ya kutofikishwa kwake.

Alidai kuwa mahakama haiwezi kuendelea kusikiliza shauri hilo na kuomba kuahirishwa kesi hiyo mpaka siku itakapopangwa ili kuendelea na utetezi wao.

Katika hatua nyingine mahakama hiyo ilisikiliza kesi namba 11 inayomkabili Zumaridi, shauri la kutumikisha watoto kinyume na sheria.

Akisoma shauri hilo wakili wa upande wa Jamhuri, Martha Mwadenya, aliiomba mahakama kuahirisha shauri hilo na kupangiwa tarehe nyingine kwa kuwa upelelezi haujakamilika.

Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, Boneventure Lema, aliahirisha shauri hilo mpaka litakaposomwa tena Novemba 14, mwaka huu, huku shauri namba 10 likipangiwa kuendelea kusikilizwa leo.




Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara, (CBE), Prof. Emmanuel Mjema, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), kuhusu kongamano la kitaaluma litakalofanyika Dodoma hivi karibuni. Kushoto ni Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Prof. Tandi Lwoga na Naibu Mkuu wa Chuo Mipango na Fedha, Dk. Emmanuel Munishi. **PICHA: JOSEPH MWEDAPOLE**

# Madiwani waombwa kushughulikia mawakala wauza mbolea ya ruzuku

Na Elizabeth John, NJOMBE

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sunday Deogratias, ameliomba Baraza la Madiwani kuwabaini mawakala wanaouza mbolea za ruzuku na madiwani kuwashughulikia mawakala wanaouza mbole ya ruzuku ili kuwaumiza wakulima. Alisema hayo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23, kuwa kumekuwa na udanganyifu kwa baadhi ya mawakala kutoa nembo za ruzuku na kuuza kwa utaratibu usio rasmi.

"Waheshimiwa madiwani kuna baadhi ya mawakala ambao tumewabaini wanauza mbolea kwa utaratibu usio rasmi na tayari wameshaanza kuchukuliwa hatua za kisheria, kwa sababu haiwezekani serikali yetu inajitahidi kuwakomboa wananchi gharama za mbolea halafu wengine wanauza kwa manufaa yao binafsi," alisema Deogratias.

Ofisa Kilimo Wilaya ya Ludewa, Clementina Kabaka, alisema kwa kuwa wakulima hawajazoea mfumo kwa sasa wanaendelea kuwaelimisha na kuwasajili.

"Mpaka sasa kuna mfumo wa ufuatiliaji ambao unasaidia kuwakamata wahalifu wanaojaribu kudanganya takwimu, kila siku hufuatilia kijiji kwa kijiji kujiridhisha na zoezi la ugawaji wa mbolea za ruzuku niwaombe wakulima kuandaa fedha za kununulia mbolea," alisema Kabaka. Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Wise Mgina, alisema hakuna sababu ya kuwafumbia macho mawakala wa aina hiyo wanaorudisha nyuma juhudi za serikali na kuwaumiza wananchi.

"Mkurugenzi niwapongeze kwa juhudi mnazozifanya kwa lengo la kuleta maendeleo katika wilaya yetu, hivyo niwasihi mwendeleze juhudi hizo nasi madiwani tutawaunga mkono," alisema Mgina.

# Lindi yazalisha wanasayansi chipukizi 12 shule sekondari

**Na Mwandishi wetu**

Taasisi ya Wanasayansi Chipukizi Tanzania Young Scientists Tanzania (YST), imechagua wanafunzi 12 kutoka shule za sekondari sita za Mkoa wa Lindi ambao watawakilisha katika maonesho ya kitaifa ya kazi za sayansi na teknolojia yatakayofanyika jijini Dar es Salaam.

Wanafunzi hao walichaguliwa katika maonesho ya kimkoa yaliyofanyika wilaya ya Lindi na shule 25 za mkoa huo zikiwa na wanafunzi 50 zilishiriki kuonesha kazi za sayansi na teknolojia walizozifanyia kwa muda wa miezi mitano.

Akizungumzia hatua hiyo, Mwanzilishi Mwenza wa YST, Dk. Gozibert Kamugisha, alisema maonesho ya kitaifa yatafanyika Desemba 8, mwaka huu na yatashindanisha kazi bora za wanasayansi chipukizi kutoka shule za sekondari mikoa yote ya Tanzania.

Alisema, wanafunzi waliochaguliwa Mkoa wa Lindi wamejaribu kugundua njia mbalimbali za kutatua matatizo yanayoikabili jamii kwenye masuala ya kilimo, afya, mazingira na kupata utatuzi wa masuala hayo.

"Vijana wetu wamejaribu kugundua njia mbalimbali za kutatua matatizo yanayoikabili jamii hususani kwenye masuala ya kilimo, afya na mazingira na kupata utatuzi wa masuala hayo," alisema.

Dk. Kamugisha alisema wanafunzi hao wametumia Sayansi wanayofundishwa darasani katika masomo ya Kemia, Baiolojia na Fizikia kuweka katika vitendo zaidi na kutatua matatizo wanayokabiliana na kuboresha maisha yao.

Alisema maonesho ya kimkoa yaliyoanza katika Mkoa wa Lindi yatafanyika mikoa yote nchini kwa lengo la kuchagua wanasayansi bora watakaoshiriki kwenye maonesho ya kitaifa Desemba, mwaka huu.

Maonesho ya mwaka huu ya kimkoa yaliyofanyika mkoani Lindi chini ya udhamini wa Taasisi ya Shell Tanzania.

Jumla ya tafiti bora sita za kisayansi zilichaguliwa kutoka kwenye maonesho hayo ambazo zitashiriki kwenye maonesho ya kitaifa.

Taasisi ya YST imekua ikiongoza juhudi za kutoa maarifa na ujuzi wa kisayansi na teknolojia kwa wanafunzi wa sekondari na walimu wa sayansi. Kwa miaka 10 sasa programu hii imekuwa na mafanikio na kuamsha ari na mwamko wa wanafunzi kujihusisha na utafiti wa kisayansi imeongezeka.


Mwalimu Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Lindi, Dk. Bora Haule, alilipongeza shirika hilo kwa kuwa mstari wa mbele kuwawezesha wanafunzi na walimu kuwa wabunifu na wanasayansi wa siku zijazo.

Pia, aliwataka wanafunzi walioshiriki kwenye maonesho hayo kuongeza bidii kwenye utafiti wao kwa kuwa njia waliochagua ni sahihi na yenye manufaa kwao.

"Niwatie moyo sana vijana kwa hatua mliyoifikia ya kubuni miradi hii ambayo inasaidia kuleta suluhu kwenye jamii yenu, endelezeni tafiti hizi kwa manufaa ya baadaye," alisema.

Mratibu wa YST Mkoa wa Lindi, Ashura Lema, aliwapongeza wanafunzi kwa kuonesha ubunifu wa hali ya juu ambao unatoa majibu dhidi ya changamoto zilizopo.

Aliwataka wanafunzi hao kuendeleza vipaji na ubunifu waliouanza ili kuiwezesha jamii kunufaika na ubunifu wao.



Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uchambuzi wa kituo hicho wa miswada minne itakayojadiliwa na kupitishwa kuwa sheria. Kulia ni Mkurugenzi wa Uchechemuzi, Fulgence Massawe. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Waombwa kulinusuru bwawa la maji kutoweka

**Na Thobias Mwanakatwe,**
ALIYEKUWA IGUNGA

BODI ya Maji Bonde la Kati imeunda Jumuiya za Watumiaji Maji kwa lengo la kulinusuru bwawa la maji Mwamapuli Kijiji cha Mwanzugi, wilayani Igunga, mkoani Tabora ambalo kasi ya uharibifu ilianza kuongezeka na kuhatarisha kutoweka.

Uzinduzi wa jumuiya hizo ulifanyika juzi na Ofisa Maendeleo ya Jamii Mwandamizi kutoka Bodi ya Maji Bonde la Kati, Neleya Bundala, alisema kuundwa kwa jumuiya hizo ni utekelezaji wa pamoja wa agizo lililotolewa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ili wanajumuiya wenyewe waweze kusimamia vyanzo vyao vya maji. Bundala ambaye ni Mratibu wa Jumuiya za Maji, alisema wanajumuiya na wananchi kwa ujumla wanawajibika kutunza vyanzo vya maji visiharibike kwa kuwa wao ndio watumiaji wa kwanza wa maji kwa mujibu wa sheria.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Igunga, Sauda Mtondoo, alisema bwawa la Mwampuli ni muhimu kwa uzalishaji wa mpunga, matumizi ya maji na viumbe kama samaki.

Mtondoo alisema kutokana na umuhimu wa bwawa hilo suala la usimamizi na uhifadhi wa maji ni jukumu la kila mtu na sio serikali pekee na kuwataka wananchi waungane kupiga vita uharibifu unaofanywa na baadhi ya watu.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Kati, Danford Samson, alisema kuundwa kwa Jumuiya za Watumiaji Maji kumekuwa kukisaidia kupunguza migogoro ya maji kwa kuwa ulinzi unakuwa unafanywa na wanajumuiya wenyewe.

Samson alisema ukataji miti ovyo, kulima karibu na vyanzo vya maji na unyweshaji mifugo ndani ya maeneo ya vyanzo vya maji ni sababu kuu za uharibifu wa vyanzo vya maji vinavyotegemewa na wananchi na kusababisha upungufu wa maji.

Diwani wa Kata ya Nguvumoja wilayani Igunga, Alfred Mguba, alisema juhudi zinazofanywa na Bodi ya Maji Bonde la Kati kuhakikisha bwawa la Mwampuli halifanyiwi uharibifu kuinusuru skimu ya umwagiliaji ya Mwampuli ambayo inategemewa na wananchi kwa shughuli za kilimo cha mpunga.

Wananchi kwa upande wao walishauri bwawa hilo liwekewe mpaka kutokana na mwingiliano wa watu wanaolima kandokando na taka zote zinapoingia ndani ya bwawa kina cha maji kinapungua na kuathiri skimu ya umwagili.

Mwezi Agosti, mwaka jana, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani, aliagiza uongozi wa Wilaya ya Igunga kuwaondoa wavamizi wa chanzo cha maji katika bwawa hilo.

Alisema wavamizi hao wanaendesha shughuli za kilimo ambacho kinasababisha mchanga kuelekea katika bwawa hilo.

Mradi wa umwagilaji wa Mwamapuli una ukubwa wa hekta 630 zinazomilikiwa na wakulima 970 na hekta hizo zina uwezo wa kuzalisha tani 5,000 kwa mwaka za mpunga.

## Mikenge waiomba serikali kumaliza mgogoro wa barabara

**Na Faustine Feliciane**

WANANCHI wa Kijiji cha Mikenge, Kata ya Kimbiji, Wilaya ya Kigamboni jijini Dar es Salaam, wameiomba serikali kumaliza mgogoro wa barabara kati yao na mwekezaji Kampuni ya ASM (T) LTD.

Mgogoro huo umewazuia wananchi na wawekezaji katika eneo la pwani ya bahari kushindwa kuitumia kufika kwenye shughuli zao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa kijiji hicho, Lameck Mayala, alisema suala hilo limefikia hatua ya ASM kutakiwa kulipwa fidia ili kufungua barabara iliyofungwa kwa kujenga ukuta.

"Walikuja hapa watu wa kufanya tathmini, waliuangalia huu ukuta na kusema wanaenda kuandaa ripoti kuifikisha kwa waziri tayari kwa maamuzi, lakini mpaka sasa kumekuwa kimya wananchi na wafanyabiashara wengine wanaendelea kuteseka kwa kukosa barabara ya kuwafikisha kwenye maeneo yao kazi," alisema Mayala.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Mwinyipingu Mbwana, alisema mgogoro huo umekuwa wa muda mrefu licha ya viongozi wa Wilaya ya Kigamboni kuufahamu bado suluhisho lake limekuwa kitendawili.

"Kwa sasa sisi tunaiomba serikali itusaidie, vijana wengi wamepoteza kazi baada ya wawekezaji wengine kufunga hoteli zao kutokana na kufungwa kwa barabara hii," alisema Mwinyipingu.

Mmoja wa wawekezaji waliokuwa wakiitumia barabara hiyo kufika katika maeneo yao, Arif Sheikh, alisema waliwekeza maeneo hayo kwa kujenga hoteli kubwa kwa kuchukua mikopo benki, lakini kwa sasa wamelazimika kufunga kutokana na kukosekana kwa barabara ya kuwafikisha kwenye maeneo yao.

Kama mwekezaji niliifuatilia kwa kina na kufika kwa Waziri wa Ardhi, Anjela Mabula, ambaye alikiri kuwa suala hilo lipo mikononi mwake.

"Mheshimiwa waziri alinihakikishia kuja kulitolea ufumbuzi suala hili na aliniambia suala hilo lipo mikononi mwake, lakini mpaka sasa kimya kimetawala na huyu mwenzetu ASM ameamua kuifunga kabisa kwa kujenga ukuta huu mnaouona, tunaomba serikali itusaidie kulimaliza suala hili ili na sisi tuendelee na biashara zetu, tulilazimika kuwaondoa kazini vijana wengi kwa sababu ya biashara kukwama," alisema Sheikh.

Kwa upande wake, Waziri wa ardhi, Anjelina Mabula, alisema hana jibu la moja kwa moja kuhusu mgogoro huo na atakuwa kwenye nafasi nzuri ya kuliongelea akipata maoni ya Kamishna wa Ardhi na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kigamboni.

Aidha, alikiri kulifahamu jambo hilo lakini majibu yake ni mpaka anatakapoiona ramani ya mipango miji kujua kama kweli eneo hilo lilikuwa na barabara.

"Suala la watathmini kwenda walienda kuangalia namna ya kukidhi haja ya wananchi ya kuwapo barabara, baada ya tathmini yao waone namna gani barabara inapatikana, kwa sasa sina jibu la moja kwa moja mpaka nitakapojiridhisha, bado sijaenda kuliona eneo husika," alisema Waziri Mabula.



## Serikali yataka utafiti kisayansi wa mifugo, uvuvi

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

SERIKALI imeagiza watafiti kuendelea kufanya utafiti wa kisayansi kwenye sekta za mifugo na uvuvi ili kuleta mabadiliko katika sekta hizo kwa kuwa bado inahitaji watafiti wa kutosha.

Pia watafiti wa masuala ya kisayansi ambao wameshafanya utafiti wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanawasilisha utafiti wao kwa mamlaka husika ikiwamo kwa halmashauri.

Aliyasema hayo jana Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Charles Muhina, wakati akifunga mkutano wa 45 wa Chama cha Wanataaluma wa Sayansi ya Mifugo na Uvuvi (TP).

Dk. Muhina alisema ili sekta hizo zisonge mbele ni lazima kuwapo na watafiti watakaofanya kazi zao kwa uzalendo kwa kuwa itasaidia kutoa majawabu ya matatizo yanayowakabili wadau.

Pia alisema, kupitia utafiti watafanikiwa kutatua matatizo mbalimbali katika jamii ikiwamo majanga ya mabadiliko ya tabianchi na ugonjwa UVIKO-19 kwa kiwango kikubwa imeangusha na kuharibu malengo ya katika sekta hiyo

"Tukijifunza kwa nchi ambazo zimeendelea hata kama majanga yatatokea wafugaji na wadau katika sekta ya nyama hawayumbi wanabaki vile vile tujiulize wale wanatumia mbinu gani ambayo ni mbadala na sisi tutumie kwa kuwa tutakuwa tumeweza kupiga hatua kubwa sana," aliongeza.

Mwenyekiti wa Chama hicho, Dk. Jonas Kizima, alisema katika mkutano huo mkuu na watajadiliana mada 27 ambazo zote zinalenga kuimarisha maslahi ya taifa.

"Tuko Arusha tumelenga kuhakikisha tunajadili na kuja na majibu ya mambo mbalimbali hasa ya kwenye sekta yetu kwa kuwa tunaamini kuwa sisi tuna mchango mkubwa," alisema.

Joseph Joackim kutoka katika Kampuni ya Trouw Nutrition, alisema mkutano huo, utaweza kuboresha mambo mbalimbali yanayoikabili sekta ya mifugo.

Alisema, akiwa ni mdau wa mifugo wanaungana na watafiti wote,kwa kuwa utafiti utafanyika ni vizuri ili ziweze ziweze kuzaa matunda.

Hata hivyo, alisema kampuni hiyo,imeweka mikakati wa kuboresha sekta ya ikiwa ni pamoja na kutoa elimu na mbinu mbadala kwa wafugaji kuvuna mazao yenye faida kubwa .

# Bunge lataja chanzo mgawo wa umeme

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christine Ishengoma, amesema mgawo wa umeme kwa baadhi ya mikoa nchini, unachangiwa kwa kiasi kikubwa kwa kukosekana kwa maji maeneo mengi ya Jiji la Arusha licha ya kwamba kuna vyanzo vya maji vinavyotosheleza mahitaji ya wananchi.

Dk. Ishengoma aliyasema hayo jana wakati wa ziara ya siku moja ya kamati hiyo alipotembelea na kukagua mradi wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 520 unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (AUWSA).

Alisema, kuna umuhimu kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO mkoani Arusha kuimarisha miundombinu ya mgawanyo wa nishati hiyo maeneo ya vyanzo vya maji ili kuruhusu mamlaka kuzalisha na kusambaza huduma kwa wananchi.

"Tunawaomba TANESCO kwenye vyanzo vinavyotegemewa wasikate umeme kwa kuwa maji ni uhai. Binadamu akikosa maji hawezi kuishi, hivyo wakazi wa Arusha tembeeni kifua mbele mambo yatakuwa sawa. Tutazungumza na wenzetu magumu haya yatapita," alisema.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema mahitaji ya maji kwa jiji hilo ni lita za ujazo milioni 109 na mradi una uwezo wa kuzalisha lita milioni 200.

Licha ya kuzungumza hayo, aliuagiza uongozi wa AUWSA kuhakikisha mradi huo unawanufaisha wananchi wa sehemu ulikopita wakati ukitekelezwa.

Mwenyekiti wa Bodi ya ya AUWSA, Dk. Richard Masika, alitoa rai kwa wananchi kushirikiana na mamlaka hiyo kutunza miundombinu ya vyanzo vya maji kwa maslahi yao na kizazi kijacho.

Mkurugenzi Mtendaji wa AUWSA, Justine Lujomba, aliwatoa hofu wananchi kuwa mradi utapunguza adha ya upatikanaji wa maji ndani ya jiji na maeneo jirani.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Arusha, Herini Mhina, alisema shirika hilo,linajitahidi kutokukata umeme kwenye sehemu za vyanzo nyeti na vikubwa vinavyopeleka maji kwenye mfumo wa ugavi wa AUWSA.

"Sehemu kama Mbuguni kwenye visima vikubwa hatukati umeme. Pia visima vya Seed Farm eneo la Ngaramtoni kwa kuwa inaleta maji jijini hapa na Monduli kwa kuwa hatugawi umeme tunahakikisha muda wote uko ili wananchi wapate huduma ya maji," alisema.




Baadhi ya wananchi wa Jiji la Arusha wakipata maelezo kwa wataalamu wa afya kutoka Hospitali ya Tengeru kuhusu uzazi wa mpango na kipimo cha kupima Virusi vya UKIMWI kwa njia ya mate katika ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa AICC jana. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

## Wakulima 38,000 wasajiliwa mfumo ruzuku ya mbolea

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAKULIMA 38,173 mkoani Manyara wamesajiliwa kwenye mfumo wa mpango wa ruzuku ya mbolea kwa msimu wa mwaka 2022/23 inayotolewa na serikali.Idadi hiyo ilitolewa jana na Kaimu Mkuu wa Idara ya Uchumi na Uzalishaji wa mkoani Manyara, Samweli Dahaye, wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kwa msimu huu wa kilimo.

Dahaye alisema wakulima 38,173 waliosajiliwa ni sawa na asilimia 5.7 na lengo lilikuwa kusajili wakulima 666,601.

Alisema wakulima waliosajiliwa kwenye mfumo wa Halmashauri za Wilaya ya Mbulu na Mji wa Mbulu ni 10,616, Babati 8,267, Kiteto 7,289, Babati Mjini 4,456, Hanan'g 4,147 na Simanjiro 3,398.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, alisema ni vizuri wakulima wakajisajili ili wapate kadi zao na kupatiwa mbolea na kwamba kama mtu hataki mbolea hiyo, atabaki na kadi yake siku akihitaji ataitumia kuchukua mbolea.

Katibu Tawala wa Mkoa wa manyara, Karolina Mthapula, alisema maelekezo ya awali yalikuwa yanaelekeza wasajiliwe watu ambao wanaotaka mbolea tu lakini baadaye serikali ilielekeza wakulima wote wapate.

Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janeth Mayanja, alisema wako wakulima ambao hawatumii mbolea kulingana na ardhi yao, hivyo kuwaambia watumie mbolea wanahisi wanakwenda kuwapoteza na kusababisha ardhi kuharibika.


"Wakulima wasiposajiliwa hatutajua mahitaji yao,tuweke nguvu kwenye umuhimu wa kujisajili kwa faida ya baadaye hata kwenye mahitaji mengine," alisema Mayanja.

Mayanja alisema ni vizuri kuwekeza nguvu kwenye utoaji wa elimu ili wakulima waridhie.

Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Mbaraka Batenga, alisema wanaposisitiza suala la mbolea bado watu hawana elimu ya afya ya udongo hivyo ni vizuri ukapimwa kwanza.

"Kiteto kuna wakulima ambao hawaamini katika mbolea na shida watu wengine wanakodi mashamba na mtu anawezaje kuweka mbolea hana uhakika mwakani atakodishiwa tena," alisema Batenga

Naye Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera, alisema wenye mashamba mapya hawataki kutumia mbolea.





## Wadaiwa kukimbia na mikopo ya halmashauri

**Na Oscar Asseng,** TANGA

VIJANA 70 waliokopeshwa pikipiki katika Jiji la Tanga kupitia vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, wameshindwa kurejesha mikopo na hawajulikani waliko.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Dk. Sipora Liana, wakati wa hafla ya kukabidhi mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 377 kwa vikundi 43 vya uzalishaji mali kwa kipindi cha mwaka 2022/23.

Alisema vijana hao, maarufu bodaboda, wameshindwa kurejesha mikopo hiyo na wamejiondoa stahiki ya awamu hii ya kukopesheka.

Mkurugenzi huyo alitoa angalizo kwa wanaochukua mikopo hiyo kurudisha kwa wakati ili vikundi vingine vipate fursa ya kukopeshwa.

Mstahiki Meya wa Jiji la Tanga, Abdrahaman Shiloo, aliagiza vikundi vipya vilivyopata mikopo hiyo awamu hii kuitumia kwa malengo yaliyoandika kwenye mikataba yao.

"Natoa wito kwenu kutumia fedha kwa uangalifu na uaminifu ziweze kuleta tija kwa wanavikundi wote na hatimaye mfanikiwe kuirejesha kwa wakati," alisema Shiloo.

Pia aliwakumbusha vikindu hivyo, kuwa fedha hizo ni mtihani kwao kwa kuwa ni kipimo kuangalia uwezo wao wa kuongezwa au kupunguziwa mkopo huo.

Alisema katika kipindi kilichopita cha mwaka wa fedha wa 2021/22, halmashauri hiyo, ilitoa mikopo wa zaidi ya Sh. milioni 980 milioni kwa vikundi visivyopungua 20.

Wanufaika wa mikopo hiyo waliipongeza serikali kwa kuwajali wananchi kwa kuwa imelenga kuwakwamua kiuchumi na kupambana na umaskini.

Rashidi Hussein, kutoka Kindi Farmers Youth Group, alisema wamepewa mkopo wa Sh. milioni 40 ukilinganisha na kipindi kilichopita walipewa mkopo wa Sh. milioni 20 na walifanikiwa kurejesha kwa kipindi cha miezi mitatu.

Walisema kikundi hicho, kinajishughulisha na biashara ya kuuza mchele katika eneo maarufu lililoko barabara 16 jijini humo.

Naye Seif Ally kutoka kikundi cha wenye ulemavu, alisema mkopo huo wameutumia kununua bajaji watakazotumia kujiingizia kipato na baadaye watarejesha.

# Makongoro awapa kibarua ma-DC lishe

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, amewaagiza wakuu wa wilaya za mkoa huo kwenda kutia saini mkataba wa lishe kwenye wilaya zao ili kudhibiti udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Makongoro alitoa agizo hilo jana wakati akitia saini mkataba wa lishe, unaolenga kuboresha lishe za watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Alisema mkoa huo uko nafasi ya 23 kitaifa kwa lishe, hivyo watu wa huko huzaa watoto ambao hawafundishiki darasani, hivyo ni vizuri kuanzia ngazi ya kijiji hadi mkoa, wahakikishe wanatoa elimu ili kuepuka kuwa na watoto wenye udumavu na hawafundishiki.

"Tujitahidi sisi ni mkoa kiongozi hapa Tanzania kwenye mambo mengi hata hili la lishe tusibaki nyuma,"alisema.

Naye Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Laurencia Peter, akizungumza na Nipashe, baada ya kutia saini mkataba huo, alisema mkataba kuhusu lishe utatiwa saini mpaka ngazi ya kijiji.

Peter alisema ni vizuri wazazi wakawa tayari kuchangia chakula shuleni kwa kuwa utoaji wa chakula shuleni ni eneo ambalo hawafanyi vizuri.

"Kuna uhusiano mkubwa sana kati ya chakula na kufanya vizuri darasani ndio maana tunawaambia wazazi kuridhia kuchangia chakula," alisema.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) ya mwaka 2019, zaidi ya watoto milioni 200 duniani hawapati lishe toshelezi.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa watoto wawili kati ya watatu wenye umri kati ya miezi sita hadi miaka miwili hawapati chakula kinachosaidia makuzi ya haraka ya miili yao na ubongo.

Hivyo hali hiyo inahatarisha makuzi duni ya ubongo, kushindwa kujifunza, kinga ya chini na ongezeko la maambukizi na mara nyingine vifo.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Regina Ndege (kulia) na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Wilaya ya Simanjiro, Anna Shinini, wakiwashukuru wanawake waliojitokeza kwenye kikao cha Baraza la UWT la wilaya walipojadili maendeleo yao juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wapongezwa kwa ujenzi bweni la wasichana

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WAJUMBE wa Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango katika Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru, wameridhishwa na kitendo cha wananchi wa Kata ya Kimnyaki kujitolea kuanza ujenzi wa bweni la wasichana kwenye Shule ya Sekondari Kimnyaki ambalo litakuwa na uwezo wa kulaza wanafunzi 80.

Walielezea kuridhishwa na hatua hiyo wakati kamati hiyo ilipofanya ziara ya kukagua shughuli za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa robo ya kwanza mwaka wa fedha 2022/23.

Akiwasilisha taarifa ya mradi huo, Mkuu wa Shule ya Sekondari Kimnyaki, Maria Chami, alisema mradi huo ulianzishwa kwa nguvu za wananchi kwa kufanya harambee na kupata fedha Sh. milioni 19 ambazo zilianzisha ujenzi wa msingi.

Mkuu huyo wa shule alisema mradi huo uko katika hatua za awali na hadi kukamilika kwake utagharimu Sh. milioni 150.8 huku halmashauri ikitoa Sh. milioni 10 kupitia mapato ya ndani.

Diwani wa Kimnyaki, Elikimu Marivei, alisema wananchi wa eneo hilo wameamua kuunganisha nguvu kujenga bweni la wasichana kwa lengo la kuimarisha ulinzi wa mtoto wa kike kwa kuwa wanakabiliwa na vishawishi vinavyosababisha mimba na ndoa za utotoni.

"Tumeamua kujenga bweni kumwezesha mtoto wa kike kusoma na kutimiza ndoto zao bila vikwazo ikiwa ni utekelezaji wa malengo ya serikali ya kuboresha miundombinu ya elimu nchini," alisema.

Pia wajumbe hao waliwapongeza wananchi hao pia kuridhishwa na maendeleo ya ujenzi na walimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kuendelea kutoa fedha kwa mujibu wa bajeti ili kuunga mkono juhudi za wananchi hao.

Makamu Mwenyekiti Halmashauri ya Arusha, Selina Mollel, aliwapongeza wananchi wa kata hiyo kupitia diwani wao na aliwataka wananchi wengine kuiga mfano huo kwa kuwa juhudi hizo ni kwa manufaa ya wasichana na wakazi eneo hilo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 1, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 16

**Maadili na taaluma ni chanda na pete, wizara yatoa waraka wa elimu**



Ukurasa 17

Si watu, simba na mifugo kukaa pamoja hata kreta ilivyotokea



Ukurasa 19

**Yaibuliwa programu kuziibua shule mikoa tisa kitaifa zilizoko mkiani**

TEKNOLOJIA

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

# Ukame unapotishia uhai, maji ya bahari ni jibu, mtaalamu ashauri kuwekeza

• Kilometa 1,424 za ukanda bahari ni utajiri mkubwa



Miundombinu ya kusafisha maji ya bahari kuondoa chumvi. **PICHA: MTANDAO**

WAKATI ukame na ukosefu wa maji ukielekea kuwa tatizo la dunia nzima linakoelezwa ni mabadiliko ya tabianchi, nchi zenye bahari kama Tanzania zinaweza kuwa na unafuu kukabiliana na uhaba huo? Inawezekana kuanza kusafisha maji hayo yanayotajwa kuwa bahari haina mwisho na kuondoa chumvi ili yatumike kwenye kilimo, viwandani, ujenzi na nyumbani? Vipi gharama na wataalamu uwapo au inabidi kuanza mafunzo.

Swali hilo linajibiwa na Dk.Kamugisha Byabato, mhadhiri wa uhandisi katika vyuo vikuu mbalimbali mstaafu, anayeeleza kuwa kusafisha maji bahari kunawezekana akieleza kuwa kuna njia mbili ya kuvukisha au 'distillation' na kutumia mitambo yenye kemikali za kuchukua chumvi kwenye maji.

Anaeleza kuwa njia kuvukisha au kutengeneza mvuke ndiyo bora kwa Tanzania kwa sababu inatumika sehemu nyingi kwenye viwanda vya kutengeneza chumvi ya mezani, hivyo si jambo geni nchini.

Wazalishaji wa chumvi wanavukisha maji bahari, mvuke ukiondoka wanabakiwa na mabonge ya mchuvi, hivyo inawezekana kutumia utaalamu huo na kupata faida mbili akitaja kuvuna chumvi na maji baridi kwa pamoja.

Tanzania ina ukanda wa Bahari ya Hindi wenye urefu wa takribani kilometa 1,424 au maili 800 kuanzia Mtwara hadi Tanga, eneo ambalo maji hayo yanaweza kuvunwa kwa ajili ya kilimo, ufugaji, matumizi nyumbani na viwandani na sekta zote za huduma na uzalishaji.

Anakumbusha kuwa katika mchakato huo wanaozalisha chumvi wanavukisha maji ya bahari na kuondoka na chumvi lakini hawajishughulishi na maji ambao ni mvuke na huo hasa ndiyo maji salama yasiyo na taka.

Akizungumzia jinsi ya kupata maji hayo anasema njia rahisi ni kwa kutumia mwanga wa jua kuyapata, mfano maji yakishakusanywa kwenye eneo au 'karai' kubwa au bwawa linalotengenezwa yanafunikwa na kioo juu, na ndani inawekwa miundombinu hasa kama mpira au bomba ili kuukusanya mvuke unaozalishwa baada ya maji kupigwa na jua.

"Tunachohitaji ni jua ndiyo nishati ya kuvukisha majibahari. Tunatengeneza miundombinu lakini jua lipo hatuna haja ya kutumia mafuta, kuni au umeme kuchemsha majibahari ili kupata mvuke unaotupa maji. Hapo kwetu kuna urahisi mkubwa."

"Cha muhimu kwenye mchakato huu ni jua ili kupata mvuke kutoka kwenye maji ya bahari. Nitoe mfano wa kuchota maji na kuyaweka kwenye kitu kama karai lenye kina kiasi na kulifunika na kioo juu kinaweza kuwa cha glasi au plastiki. Kingine ni mabomba au kuweka vifaa kama mrija unaochukua mvuke unaokusanyika na kwa kutumia maji hayo ya bahari unapozwa baada ya kuukusanya ndiyo majisafi salama yanayotokana na mvuke," anaeleza.

INAENDELEA UK.18

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Elimu, huduma msaada kisheria kuwa tumaini jipya kwa wanawake

KUWAPO kwa elimu ya huduma ya msaada wa kisheria inayotolewa na wasaidizi wa kisheria katika kata 14 za Wilaya ya Kilwa mkoa wa Lindi, kumefungua ukurasa mpya kwa kufanikisha mabadiliko yanayowawezesha wananchi kuripoti mikasa ya ukatili wa kijinsi, kufuatilia na kupata haki zao.

Kufikisha elimu ya msaada wa kisheria katika wilaya hiyo ikilenga wakazi wa kata 14 ni jukumu lililofanywa na jukwaa la wanawake la Tumaini Jipya kwa Wanawake Kilwa (TUJIWAKI) kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la ActionAid.

Wananchi walifundishwa sheria mbalimbali zikiwamo sheria ya ndoa, mirathi, ya mtoto, makosa ya jinai na ya ardhi waliopata mafunzo walikwenda kwa wananchi wa kata 14 za wilaya hiyo na kuwaelimisha, anasema Pili Athumani Katibu wa TUJIWAKI.

Anaongeza kuwa lengo kuu ni kusaidia wananchi kufahamu sheria hizo, kujua wapi wanaweza kupata msaada wa kisheria, kuripoti masuala ya ukatili wa kijinsia, kuongeza upatikanaji na kulinda haki za binadamu na kutatua changamoto za ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mnufaika, Pili Omari (51) mkazi wa Kijiji cha Singano, Kata ya Kivinje, ni miongoni mwa wananchi 22 wanaozungumzia jinsi huduma ya msaada wa kisheria ilivyowabadilisha maisha baada ya kuachwa na mume kwenye mahojiano na Nipashe yaliyofanyika Kilwa Kisiwani hivi karibuni.

Pili anasema aliolewa mwaka 2018 lakini ilipofika Agosti 2022 mumewe alimwacha wakati huo walikuwa wamevuna ufuta na kupata Shilingi 300,000, kikawa chanzo cha kukatazwa kukanyaga shambani kwake.

"Baada ya kupata fedha nyingi kwa mara ya kwanza, kwa mkupuo, mume wangu alibadilika na kunifukuza akinipa kitanda pekee na kubakia na shamba la ekari 20 tulilokuwa tunalima ufuta. Nilikwenda TUJIWAKI kuomba msaada wa kisheria nikapata haki yangu, tukigawana nusu ya shamba."

Anaeleza kuwa anapokea eneo lake na ametenga ekari nne za kilimo cha ufuta, mahindi na mpunga na uwanja ili fedha atakazopata ajenge nyumba kwani baada ya kuachana na mumewe anaishi nyumba ya kupanga.

Akizungumza na Nipashe, Mratibu wa ActionAid Kilwa, Steven Benard, anayeelezea miradi hiyo, anasema wanafurahishwa na mafanikio wanayoyapata Wanakilwa kupitia shughuli



Pili Omari, (kulia) akivuna ufuta shambani kwake pamoja naye ni Theodora Mkundi, Mwenyekiti wa TUJIWAKI. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

> Baada ya kupata fedha nyingi kwa mara ya kwanza, kwa mkupuo, mume wangu alibadilika na kunifukuza akinipa kitanda pekee na kubakia na shamba la ekari 20 tulilokuwa tunalima ufuta.



Pili Athumani

zao zinazoanza kuzaa matunda kwa kuibua kesi mbalimbali za ukatili wa kijinsia na watuhumiwa kushtakiwa.

"Haikuwa kazi rahisi kufika hapa tulipo leo, ilichukua miaka kadhaa kuelimisha watu kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia (GVB) unaoathiri wanawake na watoto hasa wa kike," anasema.

Tunaona kinamama wengi wanajua kutafuta msaada wa kisheria na wanaripoti GBV katika kituo cha msaada wa kisheria, TUJIWAKI, dawati la jinsi na watoto polisi na ofisi za ustawi wa jamii.

"Kesi zilizoripotiwa hadi sasa baada ya jamii kupata elimu ya GBV na huduma ya msaada wa kisheria kuanzia mwaka 2021 ni 128. Zikifikishwa dawati la jinsia la polisi, TUJIWAKI na ofisi za ustawi wa jamii, kati ya hizo kesi 56 zilipelekwa mahakamani."

Bernad anasema katika kesi zilizofikishwa mahakamani 56 za GBV ni 14 zilihukumiwa wakati nyingine 13 ziliondolewa na kwamba mbali na hilo, mwaka 2022 kesi nyingine 136 za ukatili wa ziliripotiwa katika maeneo hayo na kati ya hizo 22 zilikwenda mahakamani, nyingine ziliondolewa na 15 zinaendelea.

Anasema kabla ya Actionaid Kilwa kutoa mafunzo kwa wananchi na wasaidizi wa kisheria, jamii ilikuwa hairipoti matukio ya ukatili wa kijinsia wala haikujua wapi wanaweza kupata msaada wa kisheria na haki zao.

"Hivi sasa tumetoa mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria 14 ambao wanatoa huduma ya msaada wa kisheria, ushauri na huduma nyingine katika kata 14 za wilaya ya Kilwa kupitia TUJIWAKI, kati ya hao nane na wanawake sita.

Kupitia jukwaa la wanawake, ActionAid Kilwa na wadau wengine wamefunza watu takriban 4,700 wakiwamo watoto 4,110 kuwafundisha wapi pa kupata msaada wa kisheria, anasema Mratibu wa ActionAid Kilwa, Bernard.

"Kati ya waliofunzwa wanawake ni 2,200, wanaume 191, watu wazima ni 590 na kati ya hao wanaume ni 360 na wanawake 230 na kwamba hadi sasa wilaya ya Kilwa ina wasaidizi wa kisheria 31, kati yao 17 wanatoka Kilwa Women Paralegal Unit (KIWOPAU) na 14 ni kutoka TUJIWAKI.

Anaeleza kuwa wameamua kutoa mafunzo haya baada ya kugundua kuwa asilimia kubwa ya wananchi hawana uelewa wa masuala haya ambayo yanachangia kwa kiasi kikubwa watu kuvunja sheria na kusababisha madhara ndani ya jamii ikiwa wanawake wengi kutelekezwa na wenza na kuacha watoto wakihangaika bila matunzo.

Katibu wa Tumaini Jipya kwa Wanawake Kilwa (TUJIWAKI), Pili Athumani, anasema elimu iliyotolewa kupitia radio, matamasha na majukwaa ya wanawake wilayani Kilwa imeleta matokeo mazuri, masuala ya kuripoti matukio ya ukatili yamekuwa ya juu kuliko miaka ya nyuma baada ya wanawake kupata elimu ya ukatili wa kijinsia na kutambua wapi wanaweza kupata haki zao.

ELIMU

NA PANKRAS LUOGA

# Eti utaoa lini au khee hujaolewa? Yanawakoroga wasio na ndoa

• Wazazi, jamii acheni kuyauliza haya



Jamii na wazazi wanapotamani ndoa, wengine hufikia hatua ya kulazimisha watoto wao kuoa au kuolewa wakiamini ni jambo la lazima. **PICHA: MTANDAO**

NI kawaida kusikia mzazi au mlezi wa kijana wa kiume akiuliza 'kwani utaoa lini?' Na mtaani au kwa jamaa au ndugu wengine swali linaendelea safari hii likielekezwa kwa msichana naye akihojiwa na wanaomzunguka. 'Ehe kwani bado hujaolewa tu? Unangoja nini?' Wazazi, walezi na jamii wamekuwa wakiuliza maswali haya kwa nia njema huku wakiamini kuwa ni muhimu kila binadamu kupata mume au mke, kuingia kwenye ndoa na kuanzisha familia.

Lakini maswali haya yamekuwa mengi na muda mwingine kuulizwa sehemu ambayo si sahihi na hivyo kuwa kero kubwa kwa vijana katika jamii hasa wale ambao bado hawajabahatika kupata watu wanaowapenda na kuwatamkia uwezekano wa kuvalishana pete na kuingia kwenye ndoa.

Tukumbuke ndoa ni taasisi inayoundwa na watu wawili wanaopendana, wanaoendana na hivyo kukubaliana kwa hiari yao wenyewe kuishi kwa pamoja kama mume na mke wakipanga kufanya hivyo mbele ya jamii zao na madhehebu wanayoyaamini au hata kwa viongozi wa serikali.

### KUHOJIHOJI KUNA ATHARI?

Wakati mwingine ni vyema kujiuliza ni nini madhara ya maswali haya? Jibu, yamekuwa mengi mno mpaka kuwa kero kwa walengwa na kuwafanya baadhi ya vijana hasa wale wa kike wenye umri wa zaidi ya miaka 30 ambao bado hawajapata wachumba kuamua kuwakwepa wazazi, walezi au wanajamii na wengi wakikimbia kwa kuhamia mbali ili kuondokana na kero hiyo.

Mbaya zaidi maswali haya yamekuwa yakiulizwa bila kujali muda, sehemu wala utu wa kijana anayehojiwa. Baadhi yao huamua kuolewa na kuingia kwenye ndoa na mtu yoyote atayekuja mbele yao ili tu kuondokana na maswali hayo. Wakidai kuwa ni kuondoa gundu au mkosi.

Wahenga walisema ndoa ndoano, kwani wengi huangukia kwenye vipigo na manyanyaso ya kila aina wengine hadi kuuawa na waume au wake zao. Hii inaweza kuwa sababu mojawapo ya kuwapo kwa migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi kwa sasa katika jamii.

Wengine huwapelekea kuwa na msongo wa mawazo hivyo kupata matatizo ya afya ya akili pia huondoa uwezo wa kujiamini na kuthubutu pamoja na ubunifu miongoni mwa vijana. Mbaya zaidi wengine kufikia hatua ya kujidhuru wenyewe kwa kunywa sumu au kujinyonga ili kukwepa maswali hayo na kujisikia vibaya na kujiuliza, jamii itamwonaje kama bado hajaweza kuingia kwenye ndoa?

> Yote hayo yanaweza kusababisha vijana wa kike na kiume kukosa kujiamini, misimamo na ubunifu katika kile wanachokitaka katika maisha yao ya sasa na ya baadae.

### NINI KIFANYIKE?

Wazazi na walezi na jamii nzima lazima waanze kujitathmini hasa kuhusu umuhimu wa maswali haya katika maendeleo ya kijana ambaye anahojiwa na jamii kwa ujumla. Na kuachana na tabia ya kuuliza maswali hayo na kuwaachia vijana waamue wenyewe kuendana na uhalisia wa maisha na malengo yao na kile wanachokutana nacho.

Zaidi wazazi na jamii wajiulize maswali haya yana msingi, je, ni muhimu sana kuuliza maswali haya katika karne hii ya 21? Yanapoulizwa kwa vijana yana faida gani hasa na pia yana madhara kwa wanaohojiwa na jamii ya Mtanzania wa sasa?

Hali ya wazazi, walezi na walimu kujitafakari na kuacha kuwauliza vijana wao maswali hayo kutafanya waishi kuendana na uhalisia wa maisha ya sasa na kuongeza umakini katika kutimiza na kufikia malengo yao.

Zaidi kutaongeza hali ya kujiamini kwa vijana hasa wale wa kike ambao bado hawajaolewa na hivyo kutokuwa katika ndoa. Mwisho, itaondoa dhana mbaya miongoni mwa jamii kuwa kutoolewa ni mikosi na kulazimisha kuingia kwenye ndoa hata na watu wasiopendana nao na kusababisha kuwapo kwa migogoro na kuvunjika kwa ndoa katika jamii.

Matokeo mengine ni kupunguza idadi ya matukio ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia, shinikizo la damu kwa wanandoa, matatizo ya afya ya akili, lakini kutelekeza familia kunakosababishwa na wenza kuchukiana na hata kususiana watoto.

### WITO KWA JAMII

Wazazi na jamii waache tabia ya kuwauliza vijana maswali hayo ambayo zama hizo ni kama yasiyo ya maana kwenye maendeleo na mipango yao ya kimaisha hasa wale ambao bado hawajabahatika au hawajapenda kupata watu wanaowapenda ili kuingia nao kwenye ndoa.

Hii itasaidia vijana hawa kutumia juhudi na muda wao katika kufikia malengo yao kuliko kufikiria kuhusu lini nitaolewa au kuolewa hata kama sio malengo yake.

Tusipofanya hivyo basi vijana wanaanza kuwa na msongo wa mawazo na kukata tamaa na hadi kuamua kuingia kwenye ndoa na watu wasiowapenda, wasioendana nao wala kuwa na upendo nao ili tu kuondokana na kero ya kuulizwa maswali hayo na wazazi na jamii. Au wakati mwingine kuwaridhisha wazazi au walezi bila kujua pengine changamoto alizonazo mhusika.

Yote hayo yanaweza kusababisha vijana wa kike na kiume kukosa kujiamini, misimamo na ubunifu katika kile wanachokitaka katika maisha yao ya sasa na ya baadae. Wazazi na jamii waache kuwa chanzo cha kuwa na kizazi chenye matatizo ya afya ya akili, kisichokuwa na ubunifu, kisichojiamini na kusimamia malengo yake na chenye kugubikwa na ndoa zenye migogoro na kuvunjika baada ya muda mfupi.

Pamoja na hayo wakumbuke swali kubwa na la msingi kwao linafaa kuwa ninini jukumu, mchango na nafasi yao kama wazazi, walezi na jamii katika kutengeneza maisha bora na kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya vijana wao wasichana kwa wavulana si kuwauliza lini wataoa au mbona hadi leo hawajaolewa.

***Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi katika Fani ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Afya - MUHAS***

***Maoni: 0757-645746.***

ELIMU

NA BEATRICE MOSES

# Maadili na taaluma ni chanda na pete, wizara yatoa waraka wa elimu



Watoto wanapokosa uangalizi, maadili nyumbani na shuleni huishia kushiriki uhalifu. **PICHA: MTANDAO**

SHULE za binafsi na za serikali kuanzia za awali, msingi na sekondari zinachuana kitaaluma, licha ya kuwa mashindano haya si rasmi, vinara wa matokeo bora kwenye mitihani ya kitaifa hutangazwa, hata hivyo imebainika kuwa pamoja na ushindani wa kitaaluma kuna eneo ambalo halijapewa msukumu. Ni suala la upungufu wa kimaadili.

Upungufu huo wa maadili unachochea mambo mengi ikiwamo ukatili miongoni mwa wanafunzi wenyewe, walimu, ndugu hata wazazi na walezi wanatajwa kuhusika kwa namna tofauti.

Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa kulitambua hilo imetoa Waraka wa Elimu namba 6 wa mwaka 2022 kuhusu usimamizi wa maadili kwa wanafunzi wa shule zote za umma na binafsi.

Waraka huo ambao pamoja na mambo mengine kadhaa unataka jitihada za makusudi za kuhakikisha upatikanaji wa matokeo bora kitaaluma unakwenda sanjari na utunzaji wa maadili shuleni, tayari umeanza kutekelezwa tangu Oktoba mwaka huu.

Akizungumzia na Nipashe jijini Dar es Salaam kuhusu waraka huo Mtendaji Mkuu wa Chama cha Wawekezaji Binafsi katika sekta ya elimu (TAPIE) Dk. Albert Katagira, anayemiliki shule za Tusiime, anasema bila kuwekeza kwenye maadili hakuna mafanikio na kwamba mahali popote ambapo hamna nidhamu hakuna tija.

Anasema waraka umekuja wakati muafaka na kimekuwa ni kilio chao cha muda mrefu na kila shule kwa sasa ina kamati za ushauri nasaha ambazo zimeweka msukumo kwa serikali kuja na waraka huo unaotoa mwongozo katika kuhamasisha maadili na nidhamu kwenye shule zao.

> “Tumewekeza sana kwenye miundombinu lakini bila kukaa chini na kuweka nguvu kwenye nidhamu hayo yote hayatakuwa na maana kwa vile watoto wengi kwa sasa wamekengeuka kwenye maadili.

Dk. Katagira anasema: “Hata matokeo kutokuwa mazuri kwa viwango vilivyotarajiwa ni kutokana na kukosekana kwa nidhamu na kukengeukwa kwa maadili miongoni mwa watoto, hivyo ni wazi kuwa juhudi za pamoja zinahitajika ili kuhakikisha nidhamu inasisitizwa ili kuwa na maendeleo kitaaluma.”

“Tumewekeza sana kwenye miundombinu lakini bila kukaa chini na kuweka nguvu kwenye nidhamu hayo yote hayatakuwa na maana kwa vile watoto wengi kwa sasa wamekengeuka kwenye maadili,” anasema.

Anaeleza kuwa TAPIE imekubaliana kuwa katika kuhakikisha waraka huo unatekelezwa inatakiwa kwenye kila mkutano mkuu wa mwaka ambao unahusisha wazazi na walezi wasomewe waraka huo na kukumbushwa majukumu yao. Kwa upande wa wanafunzi katika baadhi ya shule tayari wamesomewa.

Anafafanua kuwa hata kwenye vikao vya kamati za shule waraka huo unapaswa kusomwa ili kuweka msisitizo wa utekelezaji wake ikiwa ni hatua ya kupata matokeo mazuri kwenye maadili kwa ujumla wake.

Kwa upande wake mmiliki wa Shule ya Fortune binafsi iliyoko Dar es Salaam, Hope Kaiza, anasema waraka ni muhimu kwa malezi ya sasa ambayo yana changamoto nyingi kwa kiasi kikubwa.

“Unakuta wazazi wanapambana kwenye shughuli za kujitafutia kipato watoto nyumbani wanakuwa mikononi mwa ndugu wengine, au wasaidizi wa kazi ambao baadhi yao hawapo makini hasa kwenye maadili,” anakumbusha Hope.

Kaiza ambaye ni Makamu Mwenyekiti TAPIE anasema kutokana na kukosekana kwa umakini kwenye malezi baadhi ya watoto wanajifunza mambo ambayo ni kinyume na maadili na yasiyoendana na umri wala mazingira yao.

“Hivyo wizara kutoa waraka huo ni jambo jema linalopaswa kuungwa mkono na kuwa muda mwingi mtoto anakuwa shuleni, hivyo shule ina nafasi kubwa ya kusaidia kumpa malezi bora,” anakumbusha.

Katika waraka huo ambao umesainiwa na Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, uliotolewa Oktoba 10, inaelekezwa kuwa unapaswa kuanza kutekelezwa kwenye shule zote za serikali na binafsi.

Wizara hiyo imetuma waraka huo kwa taasisi kadhaa zikiwamo za dini zote na elimu pia nakala zake zimepelekwa kwa wakuu wa ubora wa shule wa kanda na wilaya ili kusimamia na kuhamasisha utekelezaji wake.

“Imebainika kuwa kumekuwa na jitihada kubwa kutoka kwa wadau wa elimu nchini kusisitiza matokeo bora kitaaluma na kuacha au kuweka au kuwa na jitihada ndogo katika ujenzi wa maadili na tabia njema za wanafunzi,” inaelezwa katika waraka huo.

Halikadhalika unabainisha kuwa hali hiyo kwa kiasi kikubwa, inaweza kutoa mwanya kwa watoto kujenga tabia zisizokubalika na kusababisha mmomonyoko wa tamaduni na maadili ya Kitanzania.

Katika waraka huo imeelezwa kuwa kuna vyanzo vya taarifa vinavyofanya kazi ya kufundisha na kutoa malezi katika mfumo rasmi au usio rasmi na umevitaja kuwa ni pamoja na video nyumbani, vibanda-umiza kunakoonyesha picha za ngono, kompyuta michezo ya kompyuta na mitandao kama facebook na twitter.

Aidha, matumizi ya simu, redio, katuni, vinyago na vikaragosi, mabango mbalimbali, vitabu, magazeti, majarida na vipeperushi, mavazi, tabia na mitindo ya maisha ya watu kutoka ndani na nje ya nchi vimegusiwa, pia ‘mastaa’ au walio maarufu, wasanii na wana michezo, makundi rika na kumbi za starehe vinatajwa pia na kutakiwa kufuatilia na kuchukua hatua.

Waraka huo unatoa maagizo 11 yanapaswa kutekelezwa ili kulinda maadili shuleni ambayo ni pamoja kuanzisha au kuimarisha kamati za maadili au nidhamu shuleni kwa usimamizi wa karibu wa walimu wakuu na wakuu wa shule ili zifanye kazi za ujenzi wa tabia na maadili mema kwa wanafunzi kwa ufanisi.

Halikadhalika, umetaka kuimarishwa kwa mabaraza na madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto ili kuhakikisha kwamba maadili yanajadiliwa katika vikao vyote kama ajenda ya kudumu na shule zote za awali, msingi na sekondari ziweke msisitizo katika kufundisha somo la dini ili kuweka msingi imara wa maadili kwa wanafunzi.

Maofisa Elimu Kata wanatakiwa washirikiane na viongozi wa vijiji, mitaa na vitongoji kukabiliana na tatizo la watoto kukulia kwenye vyanzo vya taarifa vinavyoharibu maadili ya wanafunzi, mfano vibanda-umiza vyenye sinema za ngono.

Pia kila shule inaagizwa kuwa na sanduku la maoni ili wanafunzi watoe taarifa zitakazowezesha kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya ujenzi wa tabia njema na maadili miongoni mwao.

Aidha, shule zinaagizwa kuanzisha au kuboresha utendaji wa vyama vya wanafunzi kama skauti kama chombo muhimu katika ujenzi wa maadili miongoni mwa wanafunzi, pia vikao vyote vya walimu, wazazi, walezi na kamati na bodi za shule zinajadili changamoto mbalimbali kuhusu nidhamu au maadili ya wanafunzi.

SAYANSI

NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA

HIFADHI NGORONGORO NI ZAIDI

# Si watu, simba na mifugo kukaa pamoja hata kreta ilivyotokea

NIANZE na kumshukuru Mungu, kwa kuturehemu na kutujalia wasomaji wa Nipashe amani mioyoni mwetu, kutukirimia zawadi ya uhai, aidha ni vyema pia kumshukuru kwa kujalia Tanzania kuwa na rasilimali nyingi ikiwamo ardhi ya kutosha, ardhioevu yenye maji mengi pamoja na samaki aina mbalimbali kwenye mito, mabwawa, maziwa.

Upo pia ukanda wa Bahari ya Hindi takribani kilometa 1,424 au maili 800 kuanzisha Mtwara (mpakani na Msumbiji) hadi Tanga (mpakani na Kenya). Kadhalika, taifa limesheheni maliasili za kutosha wakiwamo wanyamapori, misitu na malikale na nguvu kazi ya kutosha inayojihusisha na uzalishaji kwenye sekta mbalimbali.

Moja ya hifadhi muhimu na ya aina yake ni Ngorongoro inafahamika kama 'Eneo la Hifadhi la Ngorongoro' lenye ukubwa wa kilometa za mraba 8,292 sawa na hekta 829,200. Hii ni sehemu ya Wilaya ya Ngorongoro yenye makao makuu Loliondo, mkoani Arusha.

Wilaya hiyo ina kilometa za mraba 14,036 sawa na hekta 1,403,600, hivyo, eneo la uhifadhi la Ngorongoro ni takribani asilimia 59 ya eneo lote la wilaya na kivutio kikubwa katika hifadhi ni 'kreta' ya Ngorongoro hivyo na jina la wilaya lilitokana na uwepo wa 'Ngorongoro Kreta'.



Mwonekano wa Bonde la Ngorongoro ambalo ni maajabu ya dunia, likisheheni rasilimali nyingi za kiuchumi, kihistoria na malikale. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

### UPEKEE WA NGORONGORO

Hili ni bonde la aina yake. Kulingana na uzoefu na mapokeo pamoja na tafiti mbalimbali zilizofanyika miaka mingi iliyopita, inaaminika kwamba 'Ngorongoro Kreta' ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa Watanzania iliyopatikana zaidi ya miaka milioni 2.5 iliyopita.

Hali hiyo ilisababishwa na volkano kama ilivyotokea Kilimanjaro, mlima ambao pia chanzo chake ni volkano. Kwa Ngorongoro mambo yalikwenda tofauti maana badala ya ule ujiuji kutoka chini ya ardhi kuruka na kupandishwa juu ya ardhi na kutengeneza mlima lakini haikuwa hivyo, badala yake kulitokea mtarafuku chini ya ardhi na kusababisha uwepo wa shimo kubwa ambalo lilisababisha uji uji laini kuporomoka na kurejea chini zaidi hivyo kutengeneza kreta au shimo kubwa kwenye eneo la Ngorongoro.

Leo ni kivutio cha aina yake kama ilivyo Kilimanjaro, mlima ambao ni mrefu zaidi barani Afrika na kilele chake kufunikwa na barafu kama yalivyo baadhi ya maeneo barani Ulaya na Amerika ya Kaskazini na kusini mwa dunia yaliyofunikwa na barafu wakati wote hata mwaka mzima.

> Katika kukubali udhamini wa wanyamapori wetu tunatamka kwa dhati kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba wajukuu wa watoto wetu wataweza kuufurahia urithii huu wa ajabu na wa thamani...



Dhamira ya kusema Ngorongoro ni zaidi ya wanyama , mifugo na watu kuishi pamoja inatokana na ukweli kwamba kwanza, ni urithi wa Tanzania lakini ni urithi kwa dunia nzima. Pili ni sehemu pekee yenye kuhudumia watu na wanyama kwa pamoja tofauti na hifadhi za taifa nyingine.

Ikumbukwe, mwaka 1948 wakoloni Waingereza, waliokuwa wakiitawala Tanganyika walipitisha sheria ya kuanzisha Hifadhi za Taifa, lakini ikaaanza kutumika mwaka 1951, mwaka mmoja kabla Malkia Elizabeth kuanza utawala 1952 hadi 2022 alipofariki dunia.

Baada ya sheria kutumika ikaanzishwa hifadhi ya kwanza ya taifa ambayo ni Serengeti, wakati huo eneo la Hifadhi ya Ngorongoro likiwa ni sehemu ya Serengeti. Kutokana na kuwapo Wamasai wakiishi ndani ya eneo la hifadhi ya taifa, changamoto nyingi zilijitokeza kutokana na hali hiyo ya uwepo wa wanyama na binadamu wanaoishi ndani ya eneo moja.

Mwaka 1959 ikaonekana ni vyema kutenganisha mbuga ya Serengeti na Eneo la Hifadhi-Ngorongoro, kuanzia hapo Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro likaanzishwa chini ya Sheria ya 'Eneo la Hifadhi Ngorongoro. Kuanzia hapo Serengeti ikabaki sehemu yenye wanyama bila makazi ya binadamu ndani yake na Ngorongoro ikawa ya mchanganyiko watu, wanyama pori na mifugo. Kuwapo na kreta au shimo la volkano lenye kina kati ya mita 400 hadi 600 kutoka juu na upana (diameter) wa kati ya kilometa 16 hadi 19 (Caldera) kukaongeza thamani ya sehemu hiyo iliyohifadhiwa.

Kidunia hii siyo kreta au shimo dogo lakini pia imesheheni wanyamapori wengi wakiwamo watano wakubwa ndiyo maana mwaka 2015 ilitangazwa kuwa moja ya maajabu saba asilia duniani.

Kutokana na mabadiliko hayo ya kijiografia na kusababisha kuwapo kreta au shimo hilo pamoja na hali ya hewa kuendelea kuwa nzuri kama kupata mvua za kutosha, uoto wa asili ikiwamo misitu, mimea mingine na nyasi aina mbalimbali vikistawi, iliwavutia wanyama mbalimbali kuishi na kuwa na wanyama wengi kama faru weusi ambao ni nadra sana kuwapata mahali pengine.

Kadhalika, Hifadhi ya Ngorongoro inafahamika kama makazi ya binadamu wa mwanzo mathalani, kutokana na utafiti uliufanyika maeneo ya Olduvai Goji na Laetoli mkoani Arusha lilivumbuliwa fuvu la binadamu. Ndiyo maana kreta ya Ngorongoro wakati mwingine, hujulikana kama 'Edeni ya Afrika' na Wamasai wakiyaona na kuyaita 'tundu jeusi'.

Kusema kweli, Kreta ya Ngorongoro ni eneo lenye manufaa mengi kwa Tanzania na nje ya mipaka. Ukiacha wanyama na watu bado kuna vitu lukuki vya kuona na vyenye manufaa mengi kihistoria, kiuchumi, kiutalii, kijamii, kiutamaduni na kimazingira. Hatua zinazochukuliwa na serikali ili kulihifadhi eneo la Hifadhi ya Ngorongoro linalindwa na kutunzwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kama alivyowahi kusema Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, katika Azimio la Arusha, kuashiria uhifadhi nchini akasisitiza:

"Katika kukubali udhamini wa wanyamapori wetu tunatamka kwa dhati kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba wajukuu wa watoto wetu wataweza kuufurahia urithii huu wa ajabu na wa thamani..."

Sehemu hii ya Tamko la Arusha la mwaka 1961, inaashiria uhifadhi endelevu ikionyesha dhamira ya dhati ya Hayati Nyerere siyo tu kuangalia manufaa kwa kizazi kilichoko bali pia aliweka mkazo kwa vizazi vijavyo ili vinufaike na rasilimali asilia kama hiyo.

Wiki ijayo tutaangazia nini watalii wa nje na ndani wangependa kujifunza au kuburudika na hifadhi zenye mvuto wa aina yake, aidha, kujionea uhalisia wa Wamasai wanaoishi eneo moja na wanyamapori, kwa kuchambua wanaishi vipi na mifugo yao na kumudu maisha ya kila siku. Nini kinafanyika ili waendelee kuishi bila kuathiri ekolojia.

ITAENDELEA

# Ukame unapotishia uhai, maji ya bahari ni jibu, mtaalamu ashauri kuwekeza



Ukame unavyosababisha watu kusotea maji. **PICHA:MTANDAO**

**INATOKA UK.13**

Dk. Byabato, mbobezi kwenye masuala ya uhandisi na teknolojia, anapoulizwa iwapo kuna uwezekano wa kupata maji ya kutosha kwa mahitaji mengine mengi zaidi ya kunywa na kupika, anasema inawezekana kwa wataalamu kufanya ukokotoaji na kuangalia kwanza yanahitajika maji kiasi gani, na kwa ajili ya shughuli zipi? Aidha kuangalia uwepo wa jua ni la kutosha pwani? Upepo ni wa kasi gani, miundombinu au vifaa vinavyohitajika vitanunuliwa wapi, ili kazi ianze.

Anafafanua kuwa uzalishaji maji bahari unategemea nishati jua ya kutosha na masuala mengine ya kiuchumi yanapaswa pia kuangaliwa kuwa pamoja na maji na chumvi kuna bidhaa nyingine zinazoweza kupatikana.

> Ukianza usiache yakauke ukiyatumia uendelee siku zote maana kama yanakatika, hewa inaingia kwenye bomba hizo ni lazima zitapata...

**KUSAFISHA KIKEMIA**

Njia ya pili ni ya kikemia ya kupitisha maji ya bahari kwenye mitambo itakayokuwa na kemikali za kuikamata chumvi yote na kuacha maji baridi yasiyo na taka za chumvichumvi.

Ni ipi njia rahisi kwa Tanzania ni kuvukisha au kutumia mitambo ya kukamata chumvi, akijibu swali hilo, Dk. Byabato anasema kila jambo lazima kuwe na nia ya dhati ya kulifanikisha na kitu cha awali ni kuujua ukweli kwa kufanya utafiti kuhusu vifaa mfano kioo kitatumika cha glasi au plastiki, mabomba yatakuwa ya chuma au plastiki, maji yatakusanywa karibu na pwani au ni kilometa kadhaa ndani ya bahari.

"Kisayansi ni mpaka tufanye majaribio wenyewe, tuanze kufanya utafiti wenyewe kwanza. Ni kama upo usemi kuwa hatugundui tena gurudumu leo lipo, lakini katika kulitengeneza tairi kuna mbinu mpya zinazotumika kila uchao, tukiamua kufanya hilo jukumu, tufanye mbinu zetu kwanza halafu tukalinganishe kazi zetu na wengine".

Anasema duniani hakuna jambo jipya lakini ni lazima pia kutumia wataalamu walioko hata na yeye Dk. Byabato kuonyesha mwanga wa jinsi gani ya kufanya jukumu hilo na mbinu za kutumia, kuanzia kwa wahandisi wa hapa nchini.

Unapoamua kufanya jambo unaanza na swali je, ninachotaka kukifanya kinawezekana? Waliokwenda mwezini walianza kwa kujiuliza iwapo inawezekana kwenda mwezini na kurudi wakiwa salama? Basi hawakuwaza gharama la muhimu ni uwezekano.

Unapooanza suala la kisayansi unaangalia kama upo uwezekano wa kiufundi wa kutekeleza jambo unalokusudia. Baada ya kujiridhisha unanza kuangalia gharama ."Hilo ndilo la msingi kusafisha maji bahari inawezekana tuangalie kawanza uwezekano wa kiufundi wa kutekeleza jambo hilo ili tuwe na maji ya kutosha, nyumbani, viwandani, hospitalini kwenye kilimo na ujenzi, baada ya hapo tunaangalia gharama. Tusianze na hofu hasa eti ni mchakato wa gharama kubwa."

Mhandisi Byabato anaamini kuwa Tanzania ina wataalamu wa kutosha wa kufanyakazi hiyo naye ni mmojawapo na kwamba inawezekana kusafisha maji hayo na kupata huduma hiyo kwa matumizi mbalimbali na kutoa angalizo.

"Maji ya bahari yaliyovukishwa ni ya mvuke hayana madini wala chumvichuvi, kwa ajili ya matumizi ya kunywa tutalazimika kuyaongezea madini na virutubisho vingine muhimu vinavyokosekana," anasema na kwamba kwa upande wa hospitalini ni maji bora ndiyo yanayofaa kutumiwa.

Lakini si kila mahali pana ulazima wa kuyachuja, akisema maji ya bahari yanaweza kutumiwa vile vile yalivyo wala hayahitaji kufanya badiliko. Mfano kwenye mifumo ya kupoza vitu mbalimbali viwandani au kulainisha yanaweza kutumiwa bila kusafishwa mbali na kuondoa taka zinazoweza kuambatana nayo kutoka baharini.

Mtaalamu huyu wa teknolojia anakumbusha kuwa maji ya bahari yanahitaji vifaa vinavyokabiliana na kutu mfano mabomba ya chuma mara nyingi hayafai, lakini kama yataanza kutumiwa ni lazima muda wote bomba lipitishe maji, lisiache hata wakati mmoja."Ukianza usiache yakauke ukiyatumie uendelee siku zote maana kama yanakatika, hewa inaingia kwenye bomba hizo ni lazima zitapata..."

**MATAIFA YANAYOYATUMIA**

Kuwait inakuwa nchi ya kwanza duniani kusafisha maji bahari na kuyasambaza kwa matumizi makubwa ya nyumbani, kazi iliyoanza mwaka 1951 wakati kiwanda cha kwanza cha kuondoa chumvi kilipopewa jukumu hilo.

## WANENAVYO MALENGA

### MEZA KITI VIWE BORA

Mwili wako binadamu, usikae palepale,
Lazima tujifahamu, twende hapa pia pale,
Vinginevyo twala sumu, magonjwa haya na yale,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kazi zako wafahamu, za kukaa palepale,
Na wewe wajifahamu, maumivu hapa pale,
Ili uweze jikimu, usikae palepale,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Ufanye kazi kwa zamu, pale kwenye meza pale,
Kisha jipatie hamu, uinuke toka pale,
Hebu zunguka kwa zamu, uende hapa na pale,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kiti chako wafahamu, unachokalia pale,
Ili afyayo idumu, kiwe bora kiti kile,
Kipande shuka kwa zamu, na mgongo uwe vile,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kompyuta kwako muhimu, mejaa mezani pale,
Usawa wake muhimu, shingo ibakie dole,
Kuwa juu sana sumu, afya itakuwa lele,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Egonomia elimu, ndiyo wapatiwa tele,
Afya zetu ni muhimu, tusifikishane kule,
Miili iwe migumu, tuwe na nyingi kelele,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kiti kukaa muhimu, kiwe kimeenda shule,
Miguu tunafahamu, kaa iwe chini pale,
Kuning'inia ni sumu, wala usibaki vile,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Vya kukanyagia muhimu, hasa kwa wafupi wale,
Kufika chini vigumu, kikalia viti vile,
Hicho ni kitu muhimu, tusipate shida zile,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kuzingatia muhimu, egonomia ni shule,
Kudharau kwako sumu, hutakuwa vilevile,
Mwili takuwa mgumu, maumivu yaleyale,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

Kulinda afya muhimu, maarifa haya tele,
Sote tuingie zamu, tuzipunguze kelele,
Migongo kuwa migumu, kunywa kunywa dawa zile,
Inuka kaa inuka, meza kiti viwe bora.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**Simu: +255 767 22360**
**na barua pepe: lwagha@gmail.com**

ELIMU

NA DEVOTA MWACHANG'A

# Yaibuliwa programu kuziibua shule mikoa tisa kitaifa zilizoko mkiani



Wanufaika, wanafunzi wa Shule ya Msingi Mkoani Kibaha, wakiwa na wataalamu wa mradi unaowaboreshea elimu. **PICHA: DEVOTA MEACHANG'A**

KWA mtazamo wa watu wengi neno 'shule bora' huleta taswira ya zile zenye elimu bora, mazingira mazuri ya kujifunzia, walimu wa kutosha, vifaa vya kujifunza na wanafunzi wenye uwezo wa juu kitaaluma.

Kwa mradi wa elimu uitwao "Shule Bora Program" mtazamo wake unalenga mabadiliko ya kielimu na kuzikomboa shule za serikali kwenye mikoa iliyotajwa kuwa chini kitaaluma, hususani kwa watoto wa kike na wenye ulemavu.

Serikali nchini iko katika jitihada kuhakikisha inaleta maendeleo katika sekta elimu, ikiwamo kuhakikisha watoto wote nchini wenye umri wa kwenda shule wanapata elimu bora.

Takwimu zinaonyesha, watoto wengi wanapojiunga na kuendelea na masomo, matokeo ya elimu yamekuwa na changamoto nyingi, kukitajwa asilimia nane ya wanafunzi katika elimu ya msingi wanafikia kiwango cha taifa kujua kusoma kwa ufasaha, huku wastani kuna wanafunzi 62 kwa kila mwalimu mmoja katika shule za msingi za serikali.

Serikali sasa imeungana na Shirika la Maendeleo la Uingereza (UKaid) na katika kitwacho 'Shule Bora Programu' inayolenga kufanikisha kuwapo elimu sawa kwa watoto wote, kupitia maboresho ya kila mtoto kupata msingi mzuri wa elimu ya awali.

### PROGRAMU ILIVYO

Mradi wa "Shule Bora" uliopo kiufundi chini ya 'Cambridge Education Tanzania (UKAID) unaotarajiwa kuwakomboa watoto takriban milioni nne wanaosoma katika shule za umma kwenye mikoa tisa, ambayo ni; Dodoma, Katavi, Kigoma, Mara, Pwani, Rukwa, Simiyu, Singida na Tanga, ikishirikiana na mashirika ya ADD International, International Rescue Committee na Plan International.

Raymond Kanyambo, ni Meneja Mawasiliano wa Mpango huo kutoka UKAID, anasema gharama za mradi wa Shule Bora ni bajeti ya Paundi za Kiingereza milioni 89 sawa na shilingi bilioni 271, ukitekelezwa kuelelekea mwaka 2027.

Matarajio ni mradi kutengenezwa mfumo wa elimu utakaoziba pengo kati ya wasichana na wavulana, pia kuinua viwango vya kusoma na kuandika.

Programu ya Shule Bora inajipanga kutoa msaada wa kiufundi kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia), Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na wakala zinazohusika katika mageuzi ya kielimu.

### WANUFAIKA?

Shule ya Msingi Mkoani iliyoko katika Halmashauri ya Mji Kibaha, iko katika zitakazonufaika kwenye mkakati wa kuwakwamua wanafunzi wa kike, wenye ulemavu na wenye mazingira magumu kupata elimu bora.

Mwalimu Mkuu, Ester Richard anaeleza jumla ya wanafunzi 885 (wavulana 51% na wasichana 49%), akifafanua: "Shule yetu ni miongoni mwa shule za msingi 72 zilizoko Halmashauri ya Mji Kibaha mkoani Pwani."

"Shule inakabiliwa na uhaba wa walimu, ukosefu wa vyoo, uhaba wa walimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na changamoto nyingine," anaeleza.

Anafafanua kwamba Shule ya Msingi Mkoani, ina jumla ya watoto 35 wenye mahitaji maalumu, wakiwamo wenye ulemavu wa viungo, ulemavu wa akili, wasiosikia, wasioona na wenye ulemavu wa ngozi.

"Miongoni mwao wapo wenye ulemavu zaidi wanaohitaji kuhudumiwa na kufundisha kwa ukaribu; pamoja na changamoto hiyo, kuna walimu wanne tu wenye sifa za kufundisha watoto wenye mahitaji maalumu."

Mwalimu Mkuu anaendelea: "Ukiacha ukosefu wa walimu, tunakabiliwa na changamoto nyingine mbalimbali kama vile kukosa vifaa saidizi vya kufundishia na vya utambuzi wa watoto wenye changamoto ya ujifunzaji mfano uoni hafifu na usikivu mdogo."

Richard anaishukuru serikali kupeleka vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa elimu ya mahitaji maalumu vikiwamo vihesabio na vitabu vyenye maandishi makubwa.

Anataja kasoro iliyopo, ni hitaji la chumba cha darasa kwa watoto wenye mahitaji maalumu, viti mwendo (wheelchair), vifaa vya kusaidia usikivu na chati za kubandika ukutani.

### MAFUNZO YANAVYOWAFIKIA

Mshauri wa Mawasiliano wa Programu kutoka Asasi ya Cambridge Education Tanzania, Daniel Harris, mafunzo maalumu yaliandaliwa kwa maofisa habari na mawasiliano wa serikali kwenye halmashauri hiyo.

Harris anaelezea kwamba, ni hali inayowajengea uwezo kuutambua mradi wa 'Shule Bora' kuimarisha upatikanaji sawa na mafunzo bora kwa mwanafunzi, kuanzia ngazi elimu ya awali, msingi na kumwandaa kwenda sekondari.

Kwa mujibu wa mafunzo hayo yalitolewa kwa awamu tatu kati ya mwezi Agosti na Septemba katika Kanda ya Ziwa (Mwanza), Morogoro na Kigoma.

Mshauri Harris, anasema maofisa habari na mawasiliano, ni wadau wakubwa wakiwa na jukumu la kutumia mawasiliano katika kuongeza uelewa wa umma kuhusu mpango huo wa elimu.

### WADAU SERIKALINI

Revocatus Kassimba, ni Ofisa Habari Mkuu Mkoa akiwa na maoni: "Mkoa wa Rukwa utanufaika sana na programu hii, kumekuwapo na hitaji kubwa la watoto kuandikishwa shule hasa wilaya za Kalambo, Nkasi na Sumbawanga ambako mwitikio wa elimu kwa wote hasa wasichana na walemavu ni mdogo."

Ofisa Habari Mkoa wa Tanga, Jamal Zuberi, anasema: "Nimefurahi sana serikali kuja na mpango wa elimu bunifu, mafunzo tuliyoyapata kuhusu mradi yametufungua, hatukuwa na uelewa kuhusu mradi huuo huu.

"Naamini nitakuwa mjumbe wa kuutangaza mradi katika mkoa wangu. Tukishirikiana kwa karibu viongozi wa mkoa na maofisa habari tutautambulisha vema mradi huu kwa umma."

> Naamini nitakuwa mjumbe wa kuutangaza mradi katika mkoa wangu. Tukishirikiana kwa karibu viongozi wa mkoa na maofisa habari tutautambulisha vema mradi huu kwa umma.

Ofisa habari kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Suzan Adamson, ana rai inayohusu wenye nafasi kama yake, kwamba washirikishwe katika miradi ya namna hiyo, ili wapate taarifa sahihi wazitoe kwa wananchi, ikizingatiwa wana mengi kuhusu miradi wana nafasi ya kuizungumzia.

Pia Ofisa Elimu ya Watu Wazima Wilaya ya Rufiji, mkoani Pwani, Hamisi Chikaula, anataja utayari wao kutekeleza mradi wa Shule Bora kwa kuhamasisha jamii kuwapeleka watoto shule, na wataalamu wa elimu wana jukumu la kupunguza changamoto zinazoikabili jamii katika sekta hiyo, kwa kuboresha mazingira ya elimu, ikiwamo ya awali.

Ofisa Habari wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Richard Marwa, anasema sasa wamefikishwa katika hatua ya kuweza kuwashawishi viongozi wao kuwashirikisha katika uandaaji taarifa za miradi ya maendeleo, yakiwamo ya masuala ya elimu, kuanzia ngazi ya awali.

# HABARI PICHANI



Mratibu mstaafu wa Elimu, Kata ya Mtindiro wilayani Muheza, mkoani Tanga, Elias Mbia Kanali, ambaye ni mkulima na mfugaji katika kijiji cha Kibaoni mkoani humo akuhudumia kuku wake. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Halima Bulembo (kulia), akizungumza na madiwani katika kikao cha Baraza la Madiwani juzi kwenye ukumbi wa Tate Plus wakati akiwahamasisha madiwani na watendaji kwenda kusimamia ujenzi wa madarasa ya sekondari mpaka Desemba 30, mwaka huu yawe yamekamilika. **PICHA: STEVEN WILLIAM**




Mwezeshaji wa Shirika lisilo la kiserikali la C-SEMA, Dominic Vitus, akitoa elimu ya jinsi ya kupambana na rushwa ya ngono katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike yaliyoandaliwa na Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), ambayo yalifanyika kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari Makumbusho Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CHEMSHABONGO NA -00 18 00-


Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia

1. ustawi
6. ng'ata
8. hirizi
9. mnyama wa kusafiria
10.keti
12.maisha ya starehe nyingi
13.chombo cha mti cha kutwangia
14.mafuta 16.toa msaada
17.jiji la kitalii Tanzania
20.fanya kama wengine 21.maoni
24.Siha 25.Furkani
26.alikuwa mwanasoka mashuhuri Ivory Coast 27.kinyume cha ufu

Chini:


1. jina la mtawala wa Misri
2. sadiki
3. kopi
4. laasiri
5. mwanamuziki toka Kigoma
7. mtoto 10.mtoto wa ndege
11.kagua 15.mtu aliye katika safari
18.Kampala ni mji wake mkuu
19.majimbo 22.malizika kwa kitu
23.Lugha ya Pakistani




## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

MAJOSHO
MTIHANI
MABUBU
UMATI
KARABATIA
ULAFI
AMALI
UTAFITI
UMIMI
ANUA
MLAJI
MUKU
BARA

AWA
TAI
AKA
IGA
AKA
AHA
AGA
ASI
TOA
ILA
BIBI
MKAA





## Viongozi dini waombwa kushirikiana na polisi kukemea migogoro

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

VIONGOZI wa dini na mila wilayani Rungwe, wameombwa kushirikiana na Jeshi la Polisi pamoja na wadau wengine kukemea uhalifu kwenye jamii ili kupunguza migogoro na kuchochea maendeleo.

Mkuu wa Jeshi la Polisi wa Wilaya ya Rungwe, Mrakibu wa Polisi, Philip Mhako, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha kujadili namna ya kukabiliana na matukio ya uhalifu kwenye jamii ikiwamo mauaji.

Alisema, katika wilaya hiyo kumekuwa na matukio mbalimbali ya ajabu yanayotokea na baadhi yake yakihusishwa na imani za kishirikina.

Alisema katika wilaya hiyo kuna migogoro mingi ya ardhi inayohatarisha amani na kuwataka viongozi hao kushiriki kusuluhisha kabla haijaleta madhara kwenye jamii.

"Juzi juzi kulikuwa na tukio kule Busokelo, mtu mmoja alifariki dunia, sasa wengine wakawa wanataka kuzika na wengine wakawa hawataki wakidai kuwa alikuwa amerogwa, imani za hivi ninyi mnatakiwa kutusaidia kukemea," alisema Kamanda Mhako.

Alisema viongozi nwa mila na wa dini ndio wanaoishi na wananchi na kwamba ni watu wanaoaminika na hivyo wakikemea jambo lolote ni rahisi kueleweka kuliko mtu mwingine yeyote.

Aliwataka wananchi wilayani humo pia kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo inapotokea jambo lolote ambalo watahitajika kufanya hivyo huku akiwataka kuacha kujichukulia sheria mkononi inapotokea kutoelewana.

# Wanaoharibu vyanzo vya maji, misitu kushughulikiwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa mila wilayani Mbeya, wametangaza kuanza kuwashughulikia watu wote wanaofanya shughuli za kibinadamu kwenye misitu iliyohifadhiwa pamoja na kwenye vyanzo vya maji ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Walitoa tangazo hilo mwishoni mwa wiki kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Idugumbi, Kata ya Utengule-Usongwe, uliokuwa umeitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua.

Mkutano huo ulikuwa na lengo la kuhamasisha utunzaji wa mazingira hasa kuzuia ukataji miti ovyo kwenye misitu iliyohifadhiwa pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kuzuia kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo hayo.

Mwenyekiti wa Machifu wa Mkoa wa Mbeya, Rocket Mwashinga, alisema kwa sasa wameamua kushirikiana na serikali kutunza maeneo hayo kutokana na serikali ya wilaya hiyo kuanza kuwatambua na kuwashirikisha.

Alisema, mtu yeyote atakayekutwa anafanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo hayo na ikaonekana kwamba kwenye taratibu za kiserikali ameshindikana, watamchukulia hatua za kimila.

Aliwataka machifu wote katika wilaya hiyo kuhakikisha wanashirikiana na viongozi wa serikali za mitaa kutunza maeneo hayo kwa maelezo kuwa kwa sasa maeneo mengi yameharibiwa na madhara wameanza kuyaona.

"Tangu zamani wazee wetu walikuwa wanawatoza faini ya ng'ombe watu wanaofanya makosa, sasa kwa kuwa serikali imeanza kututambua nawahakikishia kwamba tutatumia mbinu mbalimbali kushughulika na wanaoharibu mazingira," alisema Chifu Mwashinga.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Chuachua alisema Kijiji cha Idugumbi ni miongoni mwa maeneo katika wilaya hiyo ambayo wananchi wameharibu mazingira kwa kiasi kikubwa.

Alisema, wananchi wa maeneo hayo wanakata miti mpaka kwenye maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya kuni na kuchoma hali ambayo alisema serikali haiwezi kuvumilia.

Alisema serikali inakusudia kuanzisha operesheni maalumu ya kuwasaka na kuwachukulia hatua kali wote wanaofanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo hayo ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayoikabili dunia kwa sasa.

Dk. Chuachua alisema, kwa sasa kumekuwa na upungufu mkubwa wa maji kwenye vyanzo kutokana na wananchi kufanya shughuli zinazosababisha maji kukauka.

"Kuna watu wanalima kwenye msitu wetu uliohifadhiwa, sasa nawaambieni kwamba mwenye nia ya kulima asiende kulima, aliyelima asipande na aliyepanda asipalilie, kwahiyo muondoke kwenye maeneo hayo kabla hatujaanza kuchukua hatua," alisema Dk. Chuachua.

Aliwataka wananchi hao kuondoka kwenye maeneo hayo kabla ya Novemba 5, mwaka huu na kwamba operesheni maalumu ya kuwaondoa kwa nguvu itaanza kufanyika kwenye maeneo yote yaliyovamiwa.

Alisema, kutokana na uharibifu wa mazingira unaoendelea, kumekuwa na upungufu wa mvua hali inayohatarisha maisha ya viumbe hai wakiwamo binadamu.

Alisema, katika kijiji hicho upo mradi wa maji ambao serikali imewekeza zaidi ya Shilingi bilioni nne, lakini kwa sasa ufanisi umeshuka kutokana na uharibifu wa mazingira na awali ulikuwa unazalisha lita milioni tisa kwa sasa lita milioni tatu.

Aliwataka viongozi wa serikali za mitaa katika maeneo yote kushirikiana na wananchi pamoja na maofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), kutunza misitu kwa kutoa elimu kwa wananchi.

Kijiji cha Idugumbi ni miongoni mwa vijiji vinavyozunguka hifadhi ya misitu asilia ya Mlima Mbeya na eneo ambalo mara nyingi wananchi wanaanzisha moto unaoteketeza misitu.



Baadhi ya wachuuzi wa eneo la Kawetere jijini Mbeya wakiwauzia karoti na vitunguu abiria kwenye mabasi jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Makandarasi miradi umwagiliaji kutoongezewa muda

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI mkoani Mbeya imesema haitawaongeza muda makandarasi wanaojenga skimu za umwagiliaji wa mpunga wilayani Mbarali watakaochelewa kuanza utekelezaji wa miradi hiyo kwa makusudi.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Juma Maditto, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa makabidhiano ya mikataba ya ujenzi wa skimu nne za umwagiliaji kati ya serikali na makandarasi.

Aliwataka makandarasi hao kuanza mapema ujenzi wa miradi hiyo ili kuendana na msimu wa kilimo kwa wananchi wa maeneo hayo na kwamba serikali itachukua hatua kwa watakaozembea.

Aliwataka kuanza kupeleka vifaa muhimu vya ujenzi kwenye maeneo ya kazi ili kuepuka kushindwa kufikisha vifaa hivyo mvua ikianza kunyesha na kuchelewesha kazi.

"Hatutaki kusikia baadaye mtu anasingizia kwamba ameshindwa kufikisha mawe ama kokoto kwenye eneo la kazi kwa sababu mvua inanyesha, pelekeni vifaa hivyo mapema sasa hivi ili kuepuka visingizio hivyo," alisema Maditto.

Baadhi ya wakulima walisema wana hofu ya kutoanza kwa wakati msimu ujao wa kilimo kutokana na kuchelewa kwa ujenzi wa skimu hizo za umwagiliaji ambazo wanazitegemea.

Mmoja wa wakulima hao, Jafary Mwinjuma, alisema wakati wa ujenzi wa miundombinu hiyo ni lazima ya zamani itavunjwa na kusababisha maji kutofika mashambani.

Alisema kilimo cha mpunga katika maeneo mengi ya wilaya hiyo kinategemea umwagiliaji na endapo miundombinu hiyo itachelewa lazima madhara yatatokea.

"Sisi wakulima wa skimu ya Uturo miundombinu yetu itafumuliwa umbali wa mita 60, sasa hatujui kama wataikamilisha kujenga ndani ya mwezi mmoja maana mpaka sasa bado hawajaanza hali ambayo pia inatupa wasiwasi kama tutalima mwaka huu ama la," alisema Mwinjuma.

Naye Emmanuel Kidolelo, aliwaomba makandarasi waliopata zabuni ya kujenga miundombinu hiyo kuwashirikisha wakulima ili kuikamilisha kwa wakati na kilimo kiendelee kama kawaida.

Alisema wakulima hawana utaalamu wa kujenga miundombinu hiyo, lakini kwa kuwa wana uzoefu wa kulima wanayajua maeneo korofi na hivyo wakishirikishwa itakuwa rahisi kwa wakandarasi hao kuijenga kwa wakati na kwa ubora.

Alisema endapo wakandarasi hao watategemea utaalamu wao pekee kuna hatari wakakwama kukamilisha miundombinu hiyo na mwisho wakawachelewesha wakulima kuendelea na shughuli zao.

Mwakilishi wa Tume ya Umwagiliaji Mkoa wa Mbeya, John Chacha, alisema kazi ambazo makandarasi hao watafanya ni kujenga mabanio, mifereji ya kupeleka maji mashambani na ya upili kwenye mashamba.

Alisema, mikataba hiyo minne ina thamani ya Sh. milioni 52 na makandarasi wote waliopewa kazi hizo ni wazawa.

Alisema watahakikisha wanasimamia ujenzi wa miradi hiyo kwa ukaribu ili ikamilike kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa huku akiwataka makandarasi kuepuka kufanya uhuni wa aina yoyote.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema katika wilaya hiyo kuna skimu za umwagiliaji 85 ambazo wakulima wanazitumia, lakini zenye miundombinu mizuri zipo 34 pekee na baadhi ya skimu wakulima wamekuwa wakitumia miundombinu ya kienyeji.

Alisema kwa sasa serikali imepanga kuboresha skimu zote lakini kwa kuzijenga kwa awamu tofauti na kuwataka wakulima kuendelea kujiandaa kuongeza uzalishaji.





# Tanroads yaanika mpango kabambe ujenzi barabara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila, amesema katika mwaka huu wa fedha wataendelea kuratibu na kusimamia, ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa kilometa 36,362.

Mativila, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wakala huo.

Alisema hadi kufikia Juni mwaka huu, mtandao wa barabara za lami ulikuwa umefikia kilometa 11,513.

"TANROADS inaendelea kudhibiti uzito wa magari barabarani na kulinda maeneo ya hifadhi ya barabara ambapo hadi sasa zina mizani 70 ya kudumu 22, ya kuhamishika mizani 15," alisema

Kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, alisema miradi 14 yenye urefu wa kilometa 883 imekamilika kati ya Aprili 2021 hadi sasa ambayo imegharimu Sh. trilioni 1.37.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni barabara ya Kidahwe hadi Kasulu yenye urefu wa kilometa 63, Nyakanazi hadi Kibondo kilometa 50, Mbinga hadi Mbamba Bay kilometa 66, Njombe hadi Moronga kilometa 53.9 na Moronga hadi Makete kilometa 53.30.

Barabara zingine zilizokamilika ni Makutano hadi Natta kilometa 50 Mkoa, Kikusya Ipinda hadi Matema kilometa 39.10 na Chunya hadi Makongolosi Kilometa 39.

"Miradi ya madaraja makubwa manne iliyokamilika ni pamoja na daraja la Tanzanite, Ruhuhu, Magara, Mara, Msingi,Singida, ,Sibiti na daraja la Wami.

"Miradi mitatu ya madaraja makubwa ipo katika hatua mbalimbali ya utekelezaji kwa gharama ya Sh. bilioni 701 miradi hiyo ni daraja la JPM, Magufuli Kigongo Busisi Km 3.2 (Mwanza), Pangani (M 520) na Kitengule (M 140).

Kadhalika, alisema serikali imekamilisha usanifu wa kina wa madaraja makubwa sita ambayo yanasubiri kuanza utekelezaji wake.

Madaraja hayo ni pamoja na daraja la Simiyu katika barabara ya Mwanza - Musoma, Bwawa la Mtera katika barabara ya Iringa - Dodoma, daraja la Mzinga katika barabara ya Dar es Salaam -Kibiti, Mitomoni (Ruvuma0 Mkenda (Ruvuma) na daraja la Jangwani.

Mativila alisema, pia serikali inaendelea na ujenzi wa barabara ambapo miradi 44 ya barabara yenye urefu wa kilometa 1,523 na gharama ya Sh. trilioni 3.8 ipo katika hatua mbalimbali ya ujenzi nchi nzima.

Alisema, kwa mwaka wa fedha ulioisha kati ya Julai 2021 hadi Mei, mwaka huu, mikataba 20 inayohusisha miradi ya ujenzi wa barabara na viwanja vya ndege inayogharimiwa moja kwa moja na fedha za ndani na mingine kugharimiwa kwa fedha za washirika wa maendeleo ilisainiwa.

Alisema, mikataba ya ujenzi wa barabara zenye jumla ya kilomita 582.455 imesainiwa na mikataba ya ujenzi wa kiwanja cha ndege msalato na kumalizia jengo la kiwanja cha ndege Songwe pamoja na mizani ya Rubana ilisainiwa.

"Gharama ya miradi yote 20 ni Sh. bilioni 1,460.84 ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji," alifafanua.



Wakazi wa Jiji la Dodoma wakipita bila msongamano kwenye Mtaa wa One Way baada ya Halmashauri ya Jiji kuwaondoa wafanyabiashara wadogo (machinga) jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Meya awataka madiwani kutafuta majibu ya kero

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MSTAHIKI Meya wa Jiji la Dodoma Prof. Davis Mwamfupe, amewataka madiwani wa Halmashauri ya Jiji hilo kujikita katika kutafuta majawabu ya kero zinazowakabili wananchi ili kuwaletea maendeleo.

Prof. Mwamfupe alitoa rai mwishoni mwa wiki alipokuwa akifunga kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo jijini hapa.

Alisema wananchi wanaowaongoza wanahitaji kutatuliwa kero zao, hivyo madiwani hawana budi kutumia nafasi walizonazo kujikita katika kutatua shida mbalimbali ili wapate maendeleo na kujikwamua kiuchumi.

Pia alisema, kero za wananchi bado ziko nyingi nchini hivyo kama wawakilishi wa wananchi wakishirikiana kwa pamoja na serikali wataziondoa na kuleta maendeleo kwa wananchi wao.

"Ninawaomba madiwani wezangu tusibadili mwelekeo wa kufanya kazi kwa pamoja bali lengo letu liwe moja la kutatua kero kwa faida ya kuwaletea maendeleo kupitia miradi iliyopo kwenye kata zetu," alisema

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, aliwataka watendaji wa idara kusimamia maagizo yanayotolewa na serikali kwa ajili ya wananchi kwa kushirikiana na madiwani hao.

Mafuru alisema, shughuli zote wanazosimamia kwa upande wao watambue kuwa ni kwa ajili ya faida ya mandeleo ya wananchi kwa maana hiyo wafanye kwa uaminifu na weledi mkubwa.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo aliwataka madiwani hao kusimamia miradi ambayo ipo kwenye kata zao ili iweze kukamilika kwa wakati na wananchi wanufaike nayo.

# TADB yawapiga jeki wakulima wa zabibu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imetoa mafunzo ya siku tatu ya namna ya utunzaji fedha na uzalishaji ili kukuza kilimo cha zabibu kwa wakulima wa mkoa wa Dodoma.

Ofisa Maendeleo ya Mikopo Midogo wa TADB, Angelina Nyaisambo, alibainisha hayo wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wakulima kutoka maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Nyaisambo alisema lengo la mafunzo hayo ni pamoja na kuwaelekeza wakulima namna ya utumiaji mikopo wanayokopa kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha zabibu ambalo ni zao la biashara.

"Tumeanza kutoa mafunzo kwa wakulima ili kuhakikisha wanakuwa imara na mikopo wanayokopeshwa," alisema.

Nyaisambo alifafanua kuwa wakulima wengi hawajui namna ya utunzaji fedha hivyo elimu hiyo ni muhimu ili wajue kujiwekezea kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

Pia alisema, benki hiyo inafanya hivyo ili kutoa fursa za wakulima kujitokeza kupata mikopo ambayo wataitumia katika msimu wa kilimo cha zabibu ambacho ni zao la biashara na linastawi kwa wingi mkoani Dodoma.

Naye mkulima Zabron Maunga, alisema benki hiyo imefanya jambo jema kuwapa mafunzo hayo kwa sababu walikuwa wengi hawajui namna bora ya utunzaji fedha.

Alisema hivi sasa watajitokeza kuchukua mikopo ili kuinua kilimo cha zabibu ili kujikwamua kiuchumi wao na familia zao kwa ujumla.

Kadhalika, alisema Dodoma zabibu inastawi sana hivyo wakipewa mikopo na benki hiyo wataongeza upanuzi wa mashamba ikiwamo kupanua kiasi cha mavuno kila msimu.

Aliishukuru TADB kutokana na kutoa mikopo hiyo pamoja na kuwataka waendelee kuwasaidia wakulima wa zao la zabibu mkoani hapa ili kulima kwa tija.

Hivi karibuni, Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, alitembelea baadhi ya viwanda vya kuzalisha mvinyo ambavyo vinazalisha mchuzi na kuwataka waweke bidii katika kilimo hicho.

Mavunde alisema, zao hilo lina soko duniani kote hivyo wasibweteke badala yake walime kilimo hicho.

Alisema serikali ipo pamoja nao kuhakikisha zao hilo la kimkakati linazidi kuimarika hapa nchini na wakulima wanasonga mbele.

# Surua yazidi kuwa tishio Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WILAYA ya Magharibi A Unguja, imetajwa kuwa na wagonjwa wengi wa surua wapatao 364 ikilinganishwa na wilaya zingine za Zanzibar.

Akitoa mada ya ugonjwa wa surua katika mafunzo ya waandishi wa habari kuhusu maradhi ya kuambukiza, Ofisa Tawala Kitengo cha Elimu ya Afya kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Khadija Ali Khamis, alisema idadi ya watu 1,313 waliripotiwa kuwa na ugonjwa huo.

Khadija alisema, kwa Unguja waliripotiwa wagonjwa 997 sawa na asilimia 76 na Pemba 318 sawa na asilimia 24, huku vifo vilivyotokana na ugonjwa huo vikiwa vinane.

Alisema, Wilaya ya Magharibi A Unguja ndiyo inayoongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi, ikifuatiwa na Wilaya ya Magharibi B Unguja yenye wagonjwa 338 sawa na asilimia 26, Mjini 191 (asilimia 15) na Chakechake 142 ambao ni asilimia 11.

"Kati ya wagonjwa wote 1,315 waliolazwa hospitalini ni 81 ambapo Hospitali ya Kidongo Chekundu ina wagonjwa 15, Global Hospital sita, Al-rahma mmoja, Mnazi Mmoja 30, Vitongoji 12, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Bububu wagonjwa wanne, Wete watatu na Abdalla Mzee 10,"alisema ofisa huyo.

Pia alisema kati ya wagonjwa hao, wengi wao ni watoto walio chini ya umri wa miaka mitano wakiwamo watoto wa kiume 693 sawa na asilimia 53 na watoto wa kike 622 (asilimia 47).

Alisema, surua ni moja ya magonjwa ya kuambukiza yanayotisha kwa binadamu. Alisema licha ya kuwapo kwa chanjo, imekuwa ikisababisha vifo vingi vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Alisema, surua huenezwa na virusi jamii ya paramyxovirus, ambavyo hupatikana katika mfumo wa njia ya hewa na hukaa katika kamasi na majimaji yaliyoko katika mfumo wa hewa.

Hata hivyo, alisema watu ambao hawajapata chanjo ya ugonjwa huo wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa na miongoni mwa athari za ugonjwa huo inahusishwa na aina mbalimbali ya mashambulizi kwenye ubongo na kupoteza maisha.

Naye Meneja wa Elimu ya Afya, Hamad Magarawa, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo na hauwashambulii watoto pekee bali hata rika zote, wakiwamo watu wazima kuna uwezekano wa kupata ugonjwa huo.

Alisema Wizara ya Afya inaendelea na kampeni ya kutoa chanjo ya ugonjwa huo kwa watoto wote ambao hawajapatiwa chanjo hiyo.

Akifungua mafunzo hayo Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, aliwataka waandishi wa habari kuwa mabalozi wazuri wa kutoa elimu kwa umma kuhusu ugonjwa huo wa surua kupitia taaluma yao.

"Waandishi wa habari mnanguvu kubwa ya kuielimisha jamii kupitia vyombo vyenu vya habari dhidi ya ugonjwa huu na ndio maana tumewakusanya hapa kuwapatia elimu hii ili kuisaidia nchi" alisema, Naibu Waziri huyo wakati akifungua mafunzo hayo yaliyofanyika ukumbi wa sanaa Raha Leo Zanzibar.

## Bandari Malindi kuongezwa kina

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Bandari Zanzibar limesema linaendelea na uchimbaji wa mchanga katika gati namba tatu la bandari ili kuongeza kina kikubwa cha maji bandarini hapo.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari mjini Zanzibar, Kaimu Ofisa Uhusiano wa Shirika hilo, Hassan Juma Amour, alisema mpango huo ni utekelezaji wa serikali wa muda mfupi wa kuboresha miundombinu ya Bandari ya Malindi.

Hassan alisema, hali hiyo itarahisisha uingiaji wa meli kubwa za mizigo zinazofika katika bandari hiyo ya Malindi Zanzibar.

Alisema, shirika hilo limeona upo umuhimu wa kuboresha na kuzidisha kina kwa kuwa kunasababisha msongamano na ucheleweshaji wa kupokea mizigo ya wananchi na maji kwenye gati namba tatu ili kusaidia gati namba moja inayotumika hivi sasa.

"Shughuli hii itakapokamilika bandari inakuwa na uwezo wa kupokea meli za mizigo zenye ukubwa hadi mita 100 na kuondoa usumbufu uliopo hivi sasa," alisema.

Pia alisema itawasaidia wananchi na wafanyabiashara kupunguziwa muda wa kupokea makontena yao pamoja na kupunguziwa gharama za kusafirisha kontena kutokana na kutokuwapo kwa msongamano katika bandari hiyo.



Ofisa Utawala Kitengo cha Elimu ya Afya wa Wizara ya Afya, Khadija Ali Khamis, akizungumza na waandishi wa habari ambao hawapo pichani kuhusu ugonjwa wa surua. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Shehena ya tani 30 tende yateketezwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKALA wa Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA) umeteketeza tani 30 za tende ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu kutokana na kuharibika.

Tani hizo za tende zimeteketezwa katika ghala kuu lililoko Kibele Wilaya ya Kati Unguja ambazo zimeshaharibika vibaya na kutoa wadudu.


Akizungumza jana na waandishi wa habari baada ya uangamizaji wa tende hiyo, Mkaguzi wa Chakula kutoka ZFDA, Muhammed Shazil Shauri, alisema tende hiyo haijamaliza muda wake wa matumizi bali imeharibika kutokana na uhifadhi mbaya katika ghala.

Alisema mmiliki wa tende hiyo ni kampuni ya biashara ya Majani iliyoko Shakani Wilaya ya Magharibi Unguja. Alisema baada ya kufanya ukaguzi katika ghala hilo, walikuta tende inatoa wadudu na haifai kwa matumizi ya binadamu.

Muhammed, aliwataka wafanyabiashara kujitahidi kuboresha maghala ya kuhifadhia bidhaa kuwa na hewa ya kutosha na mpangilio bora ili kuepuka bidhaa kuharibika kabla ya muda wa matumizi kumaliza.

Naye mmiliki wa kampuni hiyo Ravia Jihadi, alisema watafuata maelekezo ya uhifadhi wa bidhaa ili kuepukana na hasara ambayo ameipata baada ya tende hizo kuteketezwa.

"Gharama kamili bado hatujafanya tathmini lakini tumeingia hasara kubwa kwa sababu mzigo ni zaidi ya tani 30," alisema.





# Raia wa Kenya akutwa amejinyonga Serengeti

**Na Mathias Marwa,** SERENGETI

MTU mmoja aliyedaiwa kuwa raia wa Kenya amejinyonga kwa kutumia mkanda wa suruali yake katika Kijiji cha Merenga, Wilaya ya Serengeti na kugundulika mtoto akiwa amening'inia ndani ya choo.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa serikali ya kijiji hicho, Moses Ryoba, alimtaja marehemu kuwa ni Didas Kegunya (28), mkazi wa Masaba nchini Kenya ambaye alifika nyumbani kwa binamu yake, Mwita Mwikwabe Oktoba 23, mwaka huu na kujinyonga siku iliyofuata.

Mwikambe akielezea tukio hilo, alisema binamu yake alikuwa haeleweki mwenendo wake tangu alipofika nyumbani kwake kutokana na kuwa na maongezi yasiyoeleweka ikiwa ni pamoja na kudai kutafutwa kwa madai ya kumuua mama yake.

"Tukio hili linatushangaza sana maana toka jana alipofika hakuwa katika hali ya kawaida, alikuwa anaongea kuwa alimuua mama yake na watu wanamfuatilia, ilhali mama yake yuko hai," alieleza Mwikambe.

Alisema kuwa alipowasiliana na ndugu wa marehemu kutaka kujua kama amemuua mama yake, walishangaa kusikia yuko Serengeti kwa kuwa siku nyingi hawakujua alipo.

Hata hivyo, haikufahamika kama mtu huyo alikuwa na tatizo la afya ya akili.



Ujenzi wa soko la biashara katika Mji wa Manispaa ya Shinyanga ukiendelea ambao utagharimu Sh. milioni 120 kupitia fedha za mapato ya ndani. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Anusurika kifo, mkwe atuhumiwa kuteketeza nyumba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa Kata ya Mhongolo, Manispaa ya Kahama, Winifrida Wambura (51), amenusurika kifo baada ya nyumba yake kumwagiwa mafuta ya petroli na kuteketezwa kwa moto akiwa ndani ya nyumba hiyo.

Tukio hilo linadaiwa kufanywa na Naimu Dyabato ambaye ni mume wa mtoto wa Winifrida, Oktoba 30, mwaka huu, majira ya saa moja jioni wakati akiwa anapika ndani ya nyumba hiyo na mke wa mtuhumiwa na mjukuu wake mwenye miaka mitatu.

Akisimulia tukio hilo Winifrida alisema, awali mtoto wake Teckla Deogratius (mke), alikuwa na ugomvi na mume wake kwa muda mrefu hali iliyowafanya kutengana kwa kipindi cha mwaka mmoja kutokana na manyanyaso yaliyokithiri ikiwamo kipigo cha kila siku mumewe anapokuwa amelewa.

Alisimulia kuwa mwanawe na mujukuu wake walirejea nyumbani baada ya kushindwa kuvumilia kukaa na mwanaume huyo.

Wambura alisema, mwanaume huyo alikuwa akiendelea kutoa vitisho vikali kwa binti yake na waliamini anayetaka kutenda jambo la kihalifu hawezi kulisema, lakini siku ya tukio mwanaume huyo alimwita mkewe waonane ili ampatie matumizi na alipogoma alimwambia atakuja kumfanyia jambo ambalo hatolisahau katika maisha yake.

Alisema, siku ya tukio alipigiwa simu na binti yake akiwa kanisani akimweleza waliyokuwa wamezungumza na mumewe juu ya vitisho na majira ya saa moja jioni akiwa ndani anaandaa chakula cha jioni alisikia harufu ya mafuta ya petroli na alipojaribu kutoka nje alikutana na moto mlangoni, wakati akitaka kuvunja dirisha alimuona mkwe wake akichoma moto madirisha mengine ili wafie ndani.

"Alijua wazi kuwa naishi na mtoto wake wa kumzaa mwenyewe na anadiriki kuchoma moto ili tufie wote ndani na nimemuona mwenyewe akiwasha moto madirisha tena nikamsemesha alivyomaliza kutekeleza tukio hilo alikimbia," alisema Wambura.

Teckla alisema, wamekuwa na ugomvi wa muda mrefu na mume wake Naimu Dyabato na watu wamejaribu kuwasuluhisha, lakini ilishindakana hali iliyosababisha mwaka jana mwezi Novemba kuondoka na kurudi kuishi nyumbani kwao.

Alisema, siku ya tukio aligoma kuonana naye ili ampatie fedha ya matumizi ya mtoto kwa sababu alikuwa anajindaa kwenda kwenye sherehe ndipo alipomwambia atakwenda kulipua nyumba yao au kuwadhuru wazazi wake na mazungumzo yao alikuwa akimrekodi kwa njia ya simu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mbulu, Hamza Abdallah alisema, taarifa ya kutokea kwa tukio hilo aliipata kupitia kwa mtendaji wake wa kata kwa sababu siku hiyo alikuwa nje ya ofisi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, ACP Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na mtuhumiwa anashikiliwa huku upelelezi ukiendelea, utakapokamilika atafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili na chanzo ni wivu wa kimapenzi.

## DC aonya ubadhirifu miradi ya maji

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKUU wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, ameonya ubadhirifu wa fedha za mauzo kwenye miradi ya maji na kuwataka wasimamizi wake wazitumie fedha hizo kwa maendeleo yenye tija na sio kujinufaisha wenyewe.

Alibainisha hayo juzi kwenye mkutano wa wadau wa maji wilayani humo ulioandaliwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), wilayani Kishapu na kwamba serikali inatekeleza miradi kwaajili ya kuwanufaisha wananchi na maendeleo ya nchi.

Alisema serikali inatumia fedha nyingi kuwatekelezea wananchi miradi ya majisafi na salama, hataki kusikia miradi hiyo inakwama kutoa huduma kutokana na hujuma za watu wachache.

Aidha, alionya watakao ihujumu miradi hiyo pamoja na kufanya ubadhirifu wa fedha za mauzo ya maji watachukuliwa hatua za kisheria.

"Miradi hii ya maji inasimamiwa na vyombo vya watoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO), nawaomba fedha ambazo mnazikusanya za mauzo ya maji mzitumie vizuri ili kuifanya miradi ya maji iwe endelevu kwa kuhudumia wananchi na sio kuzitumia kujinufaisha wenyewe tutaonana wabaya," alionya Mkude.

Aliwataka kutumia fedha wanazozikusanya za mauzo ya maji kutumika katika kufanya matengenezo ya haraka ili miradi kuendelea kutoa huduma kwa wananchi.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Wilaya ya Kishapu, Shadrack Kengese, aliwataka viongozi kuanzia ngazi za chini, pamoja na wananchi, kuilinda miundombinu ya miradi hiyo ili isihujumiwe, pamoja na kutoa taarifa RUWASA wanapoona mabomba yamepasukai yafanyiwe matengenezo haraka na kutosababisha upotevu wa maji.

Naye, Meneja wa RUWASA Wilayani Kishapu, Mhandisi Dicksoni Kamazima, alisema kazi ya RUWASA ni kutekeleza miradi ya maji kwa wananchi na kipimo cha utendaji wao ni miradi kuwa endelevu na kutoa huduma kwa muda mrefu, huku akiomba viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya chini wailinde, pamoja na kutofanya shughuli za kilimo kwenye nyanzo vya maji.

## HABARI KIMATAIFA

# AU yataka kusitishwa mapigano DRC

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

UMOJA wa Afrika umetoa wito wa kusitishwa kwa mapigano katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambapo waasi wamekuwa wakisonga mbele kuelekea mji mkuu wa Jimbo la Kivu Kaskazini mashariki mwa nchi hiyo.

DRC imemfukuza balozi wa Rwanda, ikiishutumu Kigali kwa kuwaunga mkono waasi wa M23 ambao sasa wanautishia mji wa Goma.

Inafuatia utekaji nyara wa waasi wa mji muhimu wa uchukuzi mashariki mwa nchi.

Hata hivyo, Rwanda imekanusha mara kwa mara madai kwamba inaunga mkono waasi.

Mji wa Kiwandja uliangukia mikononi mwa waasi Jumamosi, hiyo ikionesha uwezekano wa kuukata mji mkuu wa kikanda, Goma, kutoka kaskazini mwa jimbo lenye utajiri wa madini la Kivu Kaskazini.

AU imezitaka pande zote kushiriki katika mazungumzo yenye kujenga na inaziita kwenye mazungumzo ya amani nchini Kenya mwezi ujao. **BBC**



# Ukraine hakukaliki, milipuko kila kona

**KYIV,** Ukraine

MILIO ya ving'ora vya tahadhari vimesikika katika anga lote nchini Ukraine iliyoambatana na milipuko katika maeneo mengi.

Waandishi wa BBC wanaripoti juu ya milipuko kadhaa jana kuanzia asubuhi katika mji wa Kyiv ambayo ilisikika mara kwa mara.

Meya wa Kyiv, Volodymyr Klychko, alitangaza mashumbulizi miwili kwenye miundombinu muhimu huko Kyiv, na umeme ulikatika katika sehemu hiyo ya mji mkuu. Pia huduma ya maji ilikosekana katika baadhi ya maeneo.

Upande mwingine, mkuu wa eneo Oleg Sinegubov, OVA, alitangaza kutokea kwa mlipuko katika eneo jingine la Kharkiv.

"Adui amerusha makombora katika wilaya za Kharkiv na Chuguyiv. Hapo awali makombora ya S-300 yaliyorushwa kutoka Belgorod," aliandika.

Meya wa Kharkiv, Igor Terekhov, alifafanua kuwa kuna watu wawili waliofika huko Kharkiv.

"Warussia wameshambulia miundombinu muhimu katika jiji hilo," alisema.

Kutokana na mashambulio hayo mamlaka zinaonya kuhusu uwezekano wa kukatika kwa umeme.

"Katika eneo la Kharkiv, njia ya treni ya chini ya ardhi imefungwa kwa muda lakini mabasi yanaendelea na huduma," baraza la jiji lilifahamisha.

**Aligharamikia vilivyo usajili wa wanajeshi wa ziada kwa kutembea nchi nzima akitoa hamasa licha ya mamia wa raia kutoroka nchini humo huku wengine wakifanya maandamano ambayo hayajawahi kutokea.**

Warussia pia walishambulia kituo na miundombinu muhimu huko Zaporizhzhia.

Hapo awali, roketi zilirushwa kutoka kwenye ndege. Kukatika kwa umeme kunaweza kutokea katika jiji, aliripoti Oleksandr Starukh, mkuu wa Zaporizhzhia.

Miundombinu muhimu katika eneo la Cherkasy imeharibiwa, sehemu ya eneo hilo limepunguzwa nguvu, mkuu wa Cherkasy OVA aliripoti.

Jeshi la Russia lilirusha makombora katika eneo la Vinnytsia asubuhi na huku ndege za ulinzi zikidungua kombora moja, lakini likaanguka kwenye vituo vya raia, Serhiy Borzov, mkuu wa Vinnytsia OVA, aliripoti. Aliongeza kuwa kulikuwa na uharibifu, lakini hakuna majeruhi walioripotiwa.

Wakati huo huo, Taasisi ya Marekani ya Utafiti wa Vita (ISW) katika taarifa yake nyingine imesema Rais wa Russia Vladimir Putin, anajitayarisha kwa vita vya muda mrefu kwa njia za kawaida, kushikilia maeneo ya sasa iliyoyateka na kujaribu kuteka maeneo mapya.

Kwa mujibu wa wachambuzi wa ISW, hayo yanatokana na hatua ya Rais Putin kusajili wanajeshi wa ziada.

"Aligharamikia vilivyo usajili wa wanajeshi wa ziada kwa kutembea nchi nzima akitoa hamasa licha ya mamia wa raia kutoroka nchini humo huku wengine wakifanya maandamano ambayo hayajawahi kutokea," waandishi wa ripoti ya ISW wanaandika.

Kulingana na taarifa hiyo, Putin anatarajia kwamba wanajeshi wa akiba waliosajiliwa sasa watashikilia maeneo yanayokaliwa nchini Ukraine hadi mwisho wa msimu wa joto na wakati huo waliosajiliwa watakuwa wampitia mafunzo ya miezi minne hadi sita, na sasa watakuwa na uwezo wa kutumwa vitani kwa mashambulizi mapya.

Wakati huo huo, kwa mujibu wa ISW, Putin anadhania kwamba majira ya baridi kali na uhaba wa mafuta utazilazimisha baadhi ya nchi za Ulaya kukata misaada kwa Ukraine na kukubaliana zaidi katika uhusiano na Russia.

ISW inasisitiza kwamba inazungumzia msururu wa mawazo wa kiongozi huyo wa Russia sio kuhusu jinsi wanajeshi hao wa ziada watakavyoshawishi mwelekeo wa vita hivyo.

Wachambuzi wa Marekani walisema theluthi moja ya wanajeshi hao wa akiba kulingana na Putin wamewasili nchini Ukraine, lakini hakuna mabadiliko yoyote yaliopatikana hadi kufikia sasa. **BBC**



Wafanyakazi wa uokoaji wakibeba miili ya watu waliopolewa kwenye maji ya mto baada ya daraja la zamani kuvunjika na kusababisha mamia ya watu kuzama majini nchini India jana. **PICHA: REUTERS**

# Miili ya watu 141 yaopolewa kutoka mtoni India

**NEW Delhi,** INDIA

SHUGHULI za uokoaji zinaendelea katika wilaya ya Morbi ya Gujarat, ambako watu 141 wamefariki baada ya daraja la enzi ya ukoloni kuporomoka Jumapili jioni.

Maofisa 500 kutoka vikosi vya kitaifa na serikali vya kukabiliana na maafa wapo kwenye eneo la tukio wakiendelea na zoezi la kuwaokoa watu.

Wanajeshi pia wanasaidia katika juhudi hizo za uokoaji.

Maofisa wanatumia korongo kuchomoa vifusi vya daraja lililovunjika kutoka mtoni, huku waokoaji wakitumia boti ndogo kutafuta manusura zaidi.

Kufikia jana, miili 133 imerejeshwa kwa wanafamilia.

Mazishi yao yanatarajiwa kufanyika mjini Morbi Jumatatu.

Mwandishi wa BBC Roxy Gadekar, ambaye yuko katika eneo la tukio, aliripoti kwamba vikundi vya uokoaji bado vinajaribu kuopoa miili kutoka mtoni.

Miili mingi inayotolewa ni ya wanawake na watoto.

Prasanna Kumar, Kamanda wa Kikosi cha Kitaifa cha Kukabiliana na Maafa, aliiambia BBC kwamba wataendelea na operesheni hiyo hadi kila mtu atakapohesabiwa.

"Ilikuwa vigumu usiku kwa vile maji yametuama na kuna majitaka mtoni, mwonekano ulikuwa mdogo, hivyo ilikuwa vigumu kubaini miili," alisema.

Kulipopambazuka, timu za uokoaji ziliweza kutazama chini ya mabaki ya daraja lililovunjika na kupata miili zaidi.

"Tutapekua mto mzima na bila kuacha yeyote bila shaka, utafutaji utaendelea na hatutapumzika," alisema.

Wakati huo huo, machela chache zipo kwenye ukingo wa mto huku miili ikiopolewa na timu za uokoaji kutoka kwenye maji tulivu na kuletwa ufukweni.

Sehemu za bwawa dogo, ambalo liko karibu mita 500 kutoka chini ya mto kutoka kwenye mabaki ya daraja, zimevunjwa ili kupunguza kiwango cha maji katika mto huo kusaidia waokoaji. **BBC**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PATRICK HUMPHREY TARIMO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER** yenye usajili namba **T294 DUD ,** CHASSIS NAMBA: **ACU300012008** na ENGINE NAMBA: **2AZ1295213.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/PHQ/RB/422690/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PATIENS NOROBERT ERIYO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BAJAJ/BOXER/BM125** yenye usajili namba: **MC 876 DEJ, CHASSIS NAMBA: MD2B15BX3MWH94537** na **ENGINE NAMBA: JVXWMH70149.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: DAR/STA/RB/423726/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**THADEUS A MINJA** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma: cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0165-0081** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia URU SEMINARY mwaka 2014. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi , Polisi taarifa: **DAR/CHU/RB/424263/2022** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba: S1187-0732 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia ST MARY GORETI mwaka 2017 , kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa: **DAR/CHU/RB/424287/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA MAUAJI(CR.SESSION) NA. 05/2016**

**(Asilia Shauri la Uchunguzi wa Awali(PI) Na.44/2015. Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)**

**JAMHURI**

**DHIDI YA**

**1.GEOFREY S/O NTAPANYA**
**2.NDONGOS/O MBESHI**
**3.CHUPA S/O UPOLO.........................................WASHITAKIWA**
**4.IDDI S/O RASHID**

**KWA BWANA: 1. CHUPA S/O UPOLO**
**2. IDDI S/O RASHID.**

**POPOTE MLIPO TANZANIA.**

**KUITWA SHAURINI**

Mnaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani 07/11/2022 siku ya Juma tatu Saa3:00 Asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA Mkikosa kufika siku hiyo Shauri litasikilizwa upande mmoja bila nyinyi kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii Tarehe 19/10/2022.

NAIBU MSAJI MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

---

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 31/2016**

**(Asilia Shauri la Jinai Na.41/2015. Mahakama ya Wilaya Chunya)**

**JAMHURI.........................................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**JUMA TANGANYIKA...................MJIBU RUFAAA**

**KWA BWANA: JUMA TANGANYIKA**

**POPOTE ULIPO– TANZANIA.**

**KUITWA SHAURINI**

Mnaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani 07/11/2022 siku ya Juma tatu Saa3:00 Asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA Mkikosa kufika siku hiyo Shauri litasikilizwa upande mmoja bila nyinyi kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii Tarehe 27/09/2022.

NAIBU MSAJI MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GODFREY SAMSON KITENGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 157 CUJ - TOYOTA RAV 4.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **MBE/MBE/RB/405390/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**
**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**
**Shauri la Madai Na 174/2022**
**Jina la Mdai: RAPHAEL GEORGE**
**Jina la Mdaiwa: SHINYANGA PAMBE**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: SHINYANGA PAMBE**
**MWATULOLE-GEITA**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake**
Kwamba unaamriwa na Mahakama kuja kujibu madai yaliyopo hapa.Madai ya pesa sh.1,000,000/- Fika bila kukosa.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 03 Mwezi 11 Mwaka 2022 saa 2.00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo..
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 24 Mwezi 10 Mwaka 2022

..............................................
**HAKIMU**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER MWALALIKA KIBOJELA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 147 BMP.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **MBE/MBE/RB/412282/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**
**SHERIA YA UMILIKISHAJI**
**WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMBUKUMBU NA.**
**MMC/LD/30946**

**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: NAIMA OTHMAN MFURU**
Msimamizi wa miradhi ya **OTHUMAN SALUM MFURU WA S.L.P 21453, MOROGORO.**

**ARDHI: KIWANJA NA. 308 KITALU E KIHONDA- MANISPAA YA MOROGORO**

**MWOMBAJI: NAIMA OTHMAN MFURU WA S.L.P 3017, MOROGORO.**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa siku 30 toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.

**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana irudishwe kwa **MKURUGENZI WA MANISPAA- MOROGORO** S.L.P 166 MOROGORO

Valeboy H.K
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EDWARD JEROME** GONDWE ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA BMW YENYE NAMBA ZA USAJILI 270 DWH, YENYE CHASSIS NO : **WBAUF12080PN29574** NA ENGINE NO: **29574** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH /RB/ 731 /2022**

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie: 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Fally awalilia mashabiki wake waliofariki dunia

**KINSHASA, DRC Congo**

MWIMBAJI wa muziki wa rhumba wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Fally Ipupa, amezipa pole familia za watu 11 waliofariki Jumamosi wakati wa tamasha lake katika uwanja mkubwa zaidi wa michezo katika mji mkuu wa Kinshasa.

Uwanja huo ulikuwa umejaa kupita uwezo wake wa watu 80,000 - hata njia za eneo hilo zilikuwa zimejaa, kwa mujibu wa BBC.

Ripoti zimeeleza ukubwa wa umati wa watu ulizidi kwa kiasi kikubwa, idadi ambayo maafisa wa usalama wangeweza kudhibiti. Maafisa wawili wa polisi walikuwa miongoni mwa waliofariki.

Waziri wa mambo ya ndani nchini humo, Daniel Aselo Okito, ametaka waandaaji wa tamasha hilo kuadhibiwa kwa kukosa kuweka ukomo wa idadi ya wahudhuriaji.

Katika ujumbe wa Facebook, Fally Ipupa aliandika, “kulikuwa na uzingatiaji madhubuti wa taratibu za usalama katika tamasha hilo.

“Nimefadhaika sana na ninatuma rambirambi zangu kwa familia zote. Mungu kwa rehema zake nyingi aifariji mioyo iliyofiwa.

“Kwa hakika kabisa moyo wangu hauna furaha kuona mashabiki wangu wakifariki wakati wakija kufurahia shoo yangu. Mungu awatie wepesi ndugu wote wa familia waliofariki.”





# NANDY: NGUO FUPI BAIBAI

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva, Nandera Mfinanga maarufu Nandy, amesema kwa sasa hawezi tena kuvaa nguo fupi.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Nandy amesema kuwa, baada ya kuolewa na kupata mtoto mmoja wa kike na mumewe, Billnass au Nenga, sasa hawezi tena kuvaa nguo fupi.

“Baada ya kuolewa na kujifungua mtoto wangu na mume wangu Billnass kinachofuata sasa ni madera tu na kusahau nguo fupi,” aliandika.

Nandy alisema, kwa sasa mashabiki wake wasitarajie kumuona kwenye vimini kwa sababu mumewe huyo amemkataza na yeye anatambua kabisa ni mke wa mtu.

Hayo yanakuja miezi mitatu baada ya kufunga ndoa yao ya kifahari ambayo iliweka rekodi ya aina yake.

# *Wakazi aivulia kofia albamu ya Harmonize*

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya msanii wa muziki wa Bongo Fleva, Harmonize kuachia albamu yake ya tatu, rapa Wakazi amesema ndio bora zaidi kwa mwaka huu hadi sasa.

Harmonize ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Lebo ya Konde Gang, mwishoni mwa wiki aliachia albamu yake mpya aliyoipa jina la ‘Made For Us’.

Na sasa rapa Wakazi, amepamba album hiyo huku akienda mbali zaidi na kusema ‘Made For Us’ ndio album bora ya mwaka hadi sasa.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Wakazi ameandika: “Uandishi makini na pia ameonyesha namna alivyo na kipaji kwenye uimbaji na uwasilishaji.

“Albamu ya tatu ndani ya miaka minne, Mmakonde anaweka historia taratibu, hongera sana kwake.”



# SIMBA QUEENS HASIRA KWA DETERMINE GIRLS

**Na Somoe Ng'itu, RABAT**

BAADA ya timu yake kuanza vibaya Fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema watahakikisha wanafanya vizuri katika mechi ya pili dhidi ya Determine Girls, ili kufufua matumaini ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Determine Girls FC, kutoka Liberia ambayo nayo ilianza vibaya michuano hiyo kwa kuangukia kichapo cha mabao 4-0 dhidi ya nimeweka Green Buffalo ya Zambia, itaikaribisha Simba Queens katika mechi ya pili ya Kundi A itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan kuanzia saa 11:00 jioni kwa saa za hapa Morocco sawa saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Lukula, aliliambia gazeti hili hawajakata tamaa na wamepanga kubadilisha aina ya mfumo ili kuwashinda Determine Girls ambayo inaonekana inacheza soka la pasi fupi na wachezaji wake hawana kasi kubwa ukilinganisha na ASFAR FC waliyokutana nayo juzi na kukubali kichapo cha bao 1-0.

**Kocha huyo alisema mechi ya kesho itakuwa sawa na fainali yao kwa sababu wanahitaji ushindi tu na si matokeo mengine kwa faida ya kurejesha matumaini na hatimaye kutimiza malengo.**

"Tutashuka uwanjani tukiwa na ari kubwa, nakiri jana (juzi) hatukuwa katika kiwango chetu, tumeliona na tumelifanyia kazi, tunajua tunahitaji kuwa bora zaidi," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa timu yake haikuwa na bahati kwa sababu ilitengeneza nafasi nyingi ukilinganisha na wapinzani wao na walitawala mchezo kama vile walikuwa wenyeji.

"Hatukuwa na bahati, tulijipanga vizuri, tulionyesha kupambana na tulimiliki mpira hasa ndani ya dakika 30 za kwanza, tulipaswa kuimaliza mechi ndani ya dakika 20 za kwanza, imepita sasa tunajipanga na mchezo ujao," Lukula aliongeza.

Leo ni mapumziko na mechi nyingine ya mashindano hayo itakayochezwa kesho itakuwa ni kati ya ASFAR FC dhidi ya Green Buffalo FC itakayopigwa kuanzia saa 2:00 usiku kwa saa za hapa Morocco.

Timu mbili kutoka katika kila kundi zitasonga mbele kucheza hatua ya nusu fainali na nyingine mbili zitayaaga mashindano haya yanayofanyika kwa mara ya pili hapa barani Afrika.

Fainali za mashindano haya zitafanyika Novemba 13, mwaka huu wakati bingwa mtetezi ni Mamelodi Sundowns Queens ambayo iko Kundi B na jana usiku ilianza kutetea ubingwa wake kwa kuwakabili Bayesla Queens huku Wadi Degla kutoka Misri ikiwavaa TP Mazembe Queens kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).



Mshambuliaji wa Simba Queens, Aisha Mnunka (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa ASFAR FC katika mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan juzi usiku. Simba Queens ilifungwa bao 1-0. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Dulla Boys yazidi kutepeta Ligi Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Dulla Boys, imeendelea kufanya vibaya katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar inayoendelea visiwani hapa ikiwa katika mzunguko wa 10.

Dulla Boys juzi ilipoteza mchezo wake wa saba kati ya michezo 10 iliyocheza, baada ya kukubali kichapo cha mabao 3-1 dhidi ya Maafande wa Zimamoto.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdul Mutik Ali Haji, alisema tatizo kubwa linalosababisha kufungwa kwa timu yake ni wachezaji kutokuwa na uzoefu husuan pale wanapokutana na timu kubwa.

Alisema, timu yake ndio kwanza imepanda daraja msimu huu na kucheza Ligi Kuu, hivyo bado hawajazisoma vizuri mbinu za wapinzani wao ambao wapo kwa muda mrefu katika ligi hiyo.

Alisema, kushinda kwao katika michezo miwili ya awali, walianza kucheza dhidi ya timu ambazo viwango vyao vya uchezaji vinafanana. Aidha, alisema kuelekea mchezo wao wa mzunguko wa 11 dhidi ya Black Sailor, Novemba 5, mwaka huu wamejipanga kuhakikisha wanapata alama tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri.

Alisema, anajua anakutana na timu ngumu na wamepoteza michezo mingi kwa kufungwa, hivyo utakuwa mchezo ambao kila mmoja anahitaji kupata alama tatu.

Dulla Boys ipo nafasi ya 13 katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama saba, imeshinda michezo miwili, imetoka sare mchezo mmoja na imefungwa michezo saba wakati wapinzani wao, Black Sailor inaburuza mkia kwa kuwa na alama moja ikifungwa michezo tisa.

## Baraza aanika tatizo Kagera Sugar

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

HUKU aliyekuwa Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mkenya Francis Baraza akieleza kilichochangia matokeo mabovu ndani ya timu hiyo hadi kutimuliwa, uongozi wa Klabu hiyo baada ya kumrejesha kocha wao wa zamani, Mecky Mexime, kukinoa kikosi hicho, umesema una imani naye kuwa anaweza kuivusha timu hiyo hapo ilipo na kuipeleka mbele.

Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Ali Masoud, amesema kurejea kwa Mexime kwenye klabu yao si jambo la ajabu kwenye maisha ya soka kwani klabu nyingi duniani zimewahi kuwarejesha makocha wao na kwenye soka hakuna uadui wa kudumu.

"Sisi tuna imani na Mexime, tumekaa naye, tumempa matarajio yetu na yeye ametoa ya kwake, tumekubaliana kuipeleka timu mbele, hakuondoka kwa ubaya na wala hatukugomba naye, kwenye soka vitu hivi ni vya kawaida ni kama Mourihno na Chelsea, Stewart Hall kwa Azam FC, Abdallaah Kibadeni kwa Simba na mifano mingi ya kwamba makocha wanaondoka na kurejea tena kwenye klabu hizo.

"Kwenye maisha ya soka pia hakuna rafiki wala adui wa kudumu, ndiyo maana unaona Mexime amerejea na tuna imani naye kuwa anatuvusha hapa tulipo kuelekea sehemu tunayoihitaji," alisema Mtendaji Mkuu huyo.

Klabu hiyo ilimtangaza kocha huyo baada ya kuachana na Baraza ambaye alikuwa kwenye wakati mgumu msimu huu wa ligi.

Mtihani wake wa kwanza utakuwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza timu hiyo itakapokuwa mwenyeji wa KMC.

Mexime alitimuliwa Kagera Sugara, Machi mwaka jana na siku chache baadaye ikamtwaa kocha kutoka Biashara United, Baraza ambaye aliiongoza vema timu hiyo, lakini msimu huu hali imekuwa mbaya.

Wakati uongozi wa Kagera Sugar ukieleza hayo kocha aliyetimuliwa, Baraza amesema kutimuliwa kwake kutokana na timu kufanya vibaya, kumechangiwa na kikosi chake kuandamwa na majeruhi wengi.

"Nilikuwa nakutana na changamoto sana nilipokuwa kwenye timu ya Kagera Sugar, ambazo sijawahi kukutana nazo kwenye uzoefu wangu wa mpira, nilikuta timu ina wagonjwa nane vile vile kila tunapocheza lazima kuwe na majeruhi wengi, hivyo timu haiwezi kufanya vizuri," alisema Baraza.

Kagera Sugar inashika nafasi ya 13, kwenye msimamo wa ligi hiyo ikicheza mechi tisa, lakini ikiambulia pointi nane tu.

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM KUTUA MADRID

REAL Madrid wako katika nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, kutoka Borussia Dortmund msimu ujao. ***(Fichajes)***

### JONG HAONDOKI BARCA

KIUNGO wa kati wa Barcelona, Frenkie de Jong, ambaye alihusishwa na kuhamia Manchester United msimu wa majira ya joto, ana nia ya kusalia katika klabu hiyo ya Nou Camp na mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 25, hatasikiliza ofa yoyote Januari. ***(Sport)***

### JUVE KUMSHAWISHI CONTE

KLABU ya Juventus inataka kumleta kiungo wa kati wa Serbia, Sergej Milinkovic-Savic, mwenye umri wa miaka 27, kutoka Lazio na beki wa kati wa Italia, Alessandro Bastoni mwenye miaka 23, kutoka Inter Milan ili kumshawishi kocha wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte kujiunga nao. ***(Calciomercato)***

### NEDVED IMANI KWA ALLEGRI

MAKAMU wa rais wa Juventus, Pavel Nedved, amepuuzilia mbali mpango wowote wa Antonio Conte kwa kusema klabu hiyo ya Serie A “ina imani kamili” na kocha, Max Allegri. ***(DAZN)***

### SPURS KUMUUZA CELSO

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumuuza kiungo wa kati wa Argentina, Giovani lo Celso, ambaye yuko kwa mkopo Villarreal, na Spurs wanaweza kukubali ofa ya pauni milioni 18 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Insider)***

### FRIMPONG AWINDWA UNITED

KLABU ya Manchester United inavutiwa na mlinzi wa Bayer Leverkusen, Jeremie Frimpong, lakini wanaweza kukabiliana na ushindani kutoka kwa Chelsea kumnunua Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Football Transfers)***

### MALINOVSKYI AGOMBEWA

KLABU za Nottingham Forest, Tottenham, West Ham na Marseille wako tayari kufufua nia yao ya kumnunua kiungo wa kati wa Atalanta na Ukraine, Ruslan Malinovskyi, mwenye umri wa miaka 29. ***(Calciomercato)***

### ATLETICO NA FELIX SOKONI

ATLETICO Madrid ilikataa ofa ya euro milioni 100 kutoka kwa Bayern Munich kwa mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 22 katika msimu wa majira ya joto. ***(Marca)***


### ASENSIO MKATABA MPYA

REAL Madrid wanajiandaa kumpa kiungo wa kati wa Hispania, Marco Asensio mkataba mpya, huku mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 ukikamilika msimu wa majira ya joto. ***(Marca)***

### CAVANI AZAU HOFU URUGUAY

MSHAMBULIAJI wa Valencia, Edinson Cavani, mwenye umri wa miaka 35, aliumia kifundo cha mguu katika mchezo dhidi ya Barcelona Jumamosi na Uruguay wanasubiri kujua ukubwa wa jereha lake kuelekea Kombe la Dunia linaloanza. ***(Marca)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RASHFORD ALIZUNGUMZIA BAO LAKE LA 100 DIMBANI

**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford amezungumzia bao lake la 100 ndani ya Manchester United na kukiri kwamba, mabadiliko ya ‘nguvu’ hapo Old Trafford msimu huu yamechangia kuinua kiwango chake.

**Mshambuliaji huyo alikuwa amefunga mabao 98 ya klabu, lakini aliongeza mawili katika siku chache zilizopita kwanza dhidi ya FC Sheriff katika Ligi ya Europa na dhidi ya West Ham Jumapili kwenye Ligi Kuu England.**

Bao la kichwa maridadi la Rashford kipindi cha kwanza halijakuwa tu la 100 kwake kwa klabu hiyo, bali pia la ushindi katika mechi iliyokuwa na upinzani mkali kwenye Uwanja wa Old Trafford.

> ●●● Nimekuwa nikingojea tu ije na nashukuru leo imekuja, ninahisi kuhamasika sana, sasa...

Akizungumza baada ya mchezo huo na Sky Sports kuhusu karne ya mabao, Rashford alisema: “Ni (bao la 100) ambalo limekuwa akilini mwangu kwa mechi kadhaa zilizopita, lakini tumekuwa tukishinda michezo kwa hiyo nimekuwa na furaha.

“Nimekuwa nikingojea tu ije na nashukuru leo imekuja, kwa hiyo ndio, sasa tunajiandaa kwa mchezo unaofuata.”

Rashford pia, alichukua muda kujadili maboresho katika kiwango chake, akisema: “Ni nguvu tofauti kabisa katika klabu na uwanja wa mazoezi.

“Ninahisi kuhamasika sana sasa na nadhani wakati mwingine nilikuwa na shida ya akili kwenye kufunga, si utendaji wangu mwenyewe, lakini ilikuwa mambo mengine nje ya uwanja na hiyo ndiyo tofauti kubwa na msimu uliopita.

“Mara nyingi sana msimu uliopita sikuwa kwenye nafasi sahihi kwa kila mechi.”

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,046,4

JACKPOT
MECHI WIKI HII

TAREHE: 01,02 NA 03 NOVEMBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/11/22 | 20:30 | Racing Santander vs Alaves | 2.90 | 2.85 | 2.65 |
| 02. 01/11/22 | 20:45 | Porto vs Atletico Madrid | 2.38 | 3.27 | 2.83 |
| 03. 01/11/22 | 22:45 | Hull City vs Middlesbrough | 2.64 | 3.18 | 2.59 |
| 04. 01/11/22 | 22:45 | Coventry vs Blackburn | 2.41 | 3.17 | 2.87 |
| 05. 01/11/22 | 23:00 | Marseille vs Tottenham | 2.93 | 3.42 | 2.24 |
| 06. 01/11/22 | 23:00 | Sporting Lisbon vs Eintracht Frankfurt | 2.32 | 3.38 | 2.83 |
| 07. 01/11/22 | 23:00 | UD Ibiza Eivissa vs Leganes | 2.37 | 3.07 | 3.02 |
| 08. 02/11/22 | 22:45 | Birmingham vs Millwall | 2.54 | 3.19 | 2.69 |
| 09. 02/11/22 | 22:45 | Huddersfield vs Sunderland | 2.67 | 3.16 | 2.57 |
| 10. 02/11/22 | 23:00 | Mirandes vs Tenerife | 2.85 | 3.05 | 2.55 |
| 11. 03/11/22 | 20:45 | Olympiakos vs Nantes | 3.00 | 3.30 | 2.31 |
| 12. 03/11/22 | 20:45 | Zalgiris vs Slovan Bratislava | 3.04 | 3.39 | 2.24 |
| 13. 03/11/22 | 23:00 | Silkeborg vs Anderlecht | 2.36 | 3.40 | 2.85 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARTETA: FAULO YA SAKA NI MBAYA



**LONDON,** Egland

MIKEL Arteta, amezungumzia jeraha la Bukayo Saka baada ya ushindi mnono wa Arsenal dhidi ya Nottingham Forest, akisema kwamba 'ilikuwa mbaya na hakuweza kuendelea'.

Nyota huyo wa England alitolewa dakika ya 15 baada ya kufanyiwa faulo na beki wa pembeni wa Forest, Renan Lodi.

Baada ya kuhudumiwa kwa matibabu uwanjani mara mbili, Saka aliondolewa na Arteta. Reiss Nelson alichukua nafasi yake akitokea benchi na akafunga mabao yake mawili ya kwanza msimu wa Ligi Kuu England katika ushindi huo wa 5-0.

Akizungumza baada ya mchezo na Sky Sports, Arteta aliulizwa kuhusu jeraha la Saka, akijibu: "Alipigwa teke mbaya sana, kusema kweli alijaribu kucheza lakini hakuweza.

"Sidhani kama litamuweka nje kwa muda mrefu, baada ya uchunguzi wa kina itatolewa taarifa rasmi."

Arteta pia alichukua muda kujadili uchezaji wa Nelson na kurejea kwenye kiwango cha 'Washikabunduki' hao baada ya kushindwa katikati ya wiki na PSV Eindhoven kwenye Ligi ya Europa.

"Nina furaha sana kwake (Nelson), binafsi kwa sababu ni mchezaji ambaye anajaribu sana, amebadilika na anastahili nafasi. Bado hajapata dakika nyingi, lakini nina furaha kwake.



## *Kounde, Garcia waipa ahueni Barca*

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wametoa taarifa kuhusu jeraha la walinzi, Jules Kounde na Eric Garcia, baada ya wawili hao kulazimika kutoka uwanjani kwenye mchezo dhidi ya Valencia, Jumamosi.

Garcia alicheza kwa dakika 42 pekee katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Valencia Jumamosi kabla ya kutolewa nje na nafasi yake kuchukuliwa na Marcos Alonso.

Kisha Kounde alifanya mambo kuwa mabaya zaidi alipolazimika kutoka nje baada ya dakika 74.

Kuona wachezaji wawili waliokuwa chaguo lao la kwanza wakitolewa nje kwenye ushindi mdogo wakiwa wamejeruhiwa ilikuwa jambo la wasiwasi kwa klabu, lakini habari za sasa ni chanya.

Barcelona ilithibitisha ukubwa wa majeraha ya Kounde na Garcia kupitia Twitter jana. Ripoti hiyo ilieleza kwamba, Kounde aliumia misuli ya paja, huku Garcia akiumia nyonga yake ya kushoto.

Lakini majeraha yao hayaonekani kuwa makubwa na hayapaswi kuwazuia waw
hao kuwa nje ya uwanja kw
muda mrefu.

Majeraha kwa Kounde n
Garcia yangemtia wasiwa
anawakosa Andreas sa
Kocha Mkuu, Xavi, ambay
tayari Christensen na Ser
Roberto, huku Hector Be
lerin akiwa amerejea t
katika utimamu wa mwi
Jumanne watakuwa n
mchezo wa mwisho wa Li
ya Mabingwa Ulaya msim
huu wakiwa ugenini dhi
ya Viktoria Plzen. Alonso n
Gerard Pique ulinzi mbe
ya majeruhi hao.

## HABARI MICHEZO

433,814/-

# MSUGU MACHINJIONI WAIBUKA MABINGWA GGML - TOTO CUP

**Na Mwandishi Wetu, Geita**

TIMU ya watoto ya Mgusu Machinjioni imefanikiwa kutwaa taji la GGML- Toto Cup baada ya kuifunga timu ya Elimu Uwangani kwa mabao 2-0 katika mchezo wa fainali uliopigwa Nyakabale mkoani Geita.

**Mgusu Machinjioni walitangazwa kuwa mabingwa wa mashindano hayo ya soka ya watoto yanayofanyika kwa kushirikisha watoto wanaozunguka mgodi wa Kampuni ya Geita Gold Mining Ltd (GGML)**

GGML ambao ndio waanzilishi na waandaaji wa mashindano hayo, walizindua michuano hiyo katika Kata za Mtakuja na Nyankumbu za Geita Mjini kwa lengo la kutoa elimu kwa watoto, walezi na wazazi kuhusu madhara ya kuwanyonya watoto wadogo katika shughuli za uchimbaji madini na kuwanyima fursa ya masomo.

Akizungumza katika fainali hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita, Mkurugenzi Mkuu wa GGML, Terry Strong, alielezea furaha yake kwa kuhudhuria katika kilele cha mashindano hayo ya kandanda kwa vijana kutoka eneo jirani la mgodi.

Alibainisha kuwa tangu kuanza kwa shughuli zao mkoani Geita, uvamizi wa watoto wadogo umekuwa ni changamoto kubwa kwenye eneo la mgodi.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa watoto ni sehemu muhimu ya jamii inayozunguka mgodi huo katika kutekeleza shughuli zao za kibiashara.

"Kama sehemu ya kujitolea kwetu kwa jamii, tumefanya uwekezaji mkubwa katika shule, hospitali na kuchangia vifaa mbalimbali vya kutoa huduma. Mwaka 2018, GGML ilijenga zaidi ya madarasa 600.

"Hii yote ni katika kuwajengea mazingira mazuri ya elimu kwa watoto wetu kwani watoto ni kizazi cha siku zijazo na ndio wanufaika wa kwanza, jitihada zote tunazifanya katika kujitolea kwetu," alisema Strong.

Alibainisha kuwa kampuni hiyo inazingatia Kanuni Elekezi za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Kibinadamu na Kanuni za Hiari za Usalama na Haki za Kibinadamu (VP-SHR) (UNGP).

"Kwa hivyo, tumeahidi kuwalinda watoto dhidi ya hatari zozote zinazohusiana na mazoea yetu ya biashara," alisema.

Aidha, kwa mujibu wa Strong, idadi ya watoto wanaovamia na kuingia kwenye eneo la mgodi ni jambo ambalo linachukuliwa kwa tahadhari kubwa na mgodi huo.

Alisema kati ya mwaka 2019 na 2020, watoto 680 waliokolewa ndani na nje ya eneo la uendeshaji la GGML.

Alisema ili kukabiliana na hali hiyo, GGML imeshirikiana na serikali za mitaa kuanzisha programu kadhaa za uhamasishaji, ikiwa ni pamoja na mawasiliano ya moja kwa moja kwa shule za sekondari na msingi.

"Tunaamini kuwa kila shindano linapohitimishwa, wachezaji wenye vipaji vya soka wataibuka na kuchaguliwa na klabu kubwa kama Geita Gold Football Club (inayodhaminiwa na GGML) kuchuana katika uwanja wa Magogo ambao pia unadhaminiwa na GGML, lengo ni kuwaokoa hawa na kuwasaidia kukuza vipaji vyao kisoka," alisema.



Timu ya Watoto ya Mgusu Machinjioni ikifurahia ushindi baada ya kutwaa taji la GGML- Toto Cup kwa kuifunga Elimu Uwangani kwa mabao 2-0 katika mchezo wa fainali uliopigwa Nyakabale wilayani Geita juzi. Waliosimama nyuma ni baadhi ya viongozi wa GGML wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Terry Strong. **MPIGAPICHA WETU**

## Mgunda atoa siri 'gharika' Mtibwa

INATOKA UKURASA 32

darasani. Tulipoteza mechi iliyopita niliongea na askari wangu, nikawatengeneza kisaikolojia na kuwaweka katika utayari kwa mechi hii na kupata ushindi mnono.

"Tumefanikiwa mipango yetu, namshukuru Mungu na wachezaji wangu kufuata maelekezo na kufuata yale niliyowapa mazoezini na kuingia na mipango yetu na hivyo kufanikiwa kupata pointi tatu," alisema Mgunda.

Alisema hawezi kuweka wazi kuwa amepata kikosi cha kwanza kwa sababu anaamini vijana wake wanatambua falsafa yake, anahitaji nini kwa ajili ya mechi ijayo.

## *Yanga yaapa kuimaliza mechi CAF kwa Mkapa*

INATOKA UKURASA 32

ma Kamwe.

Alisema kwa sababu dhamira yao ni kufuzu hatua ya makundi, hivyo wanachukua tahadhari zote hata watakapokwenda kucheza mechi ya marudiano ugenini nchini Tunisia, huku akiongeza kuwa Yanga imeshapata uzoefu wa kutosha kucheza mechi hizi za mtoano za dakika 180.

Mabingwa hao wa Tanzania Bara wanakwenda kucheza mechi hiyo wakiwa wametolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan kwa jumla ya mabao 2-1, hivyo kuangukia kwenye Kombe la Shirikisho, ikiwania kucheza hatua ya makundi baada ya miaka minne. Mara ya mwisho iliingia hatua mwaka 2018.

Imeandaliwa na Adam Fungamwango, Saada Akida na Shufaa Lyimo


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/11/22 | 18:00 | Blackpool vs Luton Town | 2.83 | 3.23 | 2.48 |
| 02. 05/11/22 | 18:00 | QPR vs West Bromwich | 2.44 | 3.29 | 2.84 |
| 03. 05/11/22 | 18:00 | Nottingham vs Brentford | 2.73 | 3.28 | 2.54 |
| 04. 05/11/22 | 19:00 | AC Ajaccio vs Strasbourg | 2.73 | 3.08 | 2.63 |
| 05. 05/11/22 | 20:00 | Galatasaray vs Besiktas | 2.43 | 3.33 | 2.83 |
| 06. 05/11/22 | 20:30 | Everton vs Leicester | 2.33 | 3.27 | 3.03 |
| 07. 05/11/22 | 21:00 | PAU FC vs Amiens | 2.79 | 3.14 | 2.64 |
| 08. 05/11/22 | 21:00 | Bastia vs Paris FC | 2.49 | 3.11 | 3.01 |
| 09. 05/11/22 | 21:00 | Dijon vs Guingamp | 2.50 | 3.16 | 2.96 |
| 10. 05/11/22 | 22:30 | Arminia Bielefeld vs Kaiserslautern | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 11. 06/11/22 | 14:30 | Bologna vs Torino | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 12. 06/11/22 | 15:00 | Chelsea vs Arsenal | 2.63 | 3.28 | 2.63 |
| 13. 06/11/22 | 15:30 | KAA Gent vs Brugge | 2.54 | 3.59 | 2.54 |
| 14. 06/11/22 | 15:30 | Eintracht Braunschweig vs Greuther Furth | 2.54 | 3.28 | 2.73 |
| 15. 06/11/22 | 17:00 | Clermont Foot vs Montpellier | 2.31 | 3.52 | 2.83 |
| 16. 06/11/22 | 19:05 | Lille vs Rennes | 2.48 | 3.48 | 2.63 |
| 17. 06/11/22 | 19:30 | Tottenham vs Liverpool | 2.88 | 3.53 | 2.30 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 01/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1004 | Kfarsoum vs AL Karmel | 2.78 | 3.17 | 2.36 |
| 16:00 | 1371 | Coventry U23 vs Wigan U23 | 2.01 | 3.55 | 3.11 |
| 16:00 | 1498 | Polisi Tanzania vs Dodoma FC | 2.28 | 2.75 | 3.75 |
| 16:00 | 2432 | Bristol City U23 vs Charlton U23 | 1.63 | 4.86 | 3.55 |
| 16:00 | 3210 | Kagera Sugar vs KMC | 2.65 | 2.80 | 3.00 |
| 16:00 | 3569 | Buqaa Amman vs Ittihad AL Ramtha | 4.87 | 3.21 | 1.71 |
| 16:00 | 4992 | Barnsley U23 vs Sheffield United U23 | 3.10 | 4.17 | 1.86 |
| 16:30 | 5365 | Watford U21 vs Colchester U21 | 1.95 | 4.19 | 2.87 |
| 16:30 | 5914 | Venda Football Academy vs Pretoria Callies | 2.49 | 2.68 | 3.07 |
| 17:35 | 2121 | Al Qadisiyah vs AL Ain | 2.02 | 3.02 | 3.65 |
| 18:00 | 4659 | FC Otelul Galati vs Gloria Buzau | 2.39 | 3.17 | 2.73 |
| 18:10 | 1507 | AL Akhdood vs AL Arabi (SA) | 2.32 | 2.95 | 3.30 |
| 18:15 | 1702 | Zaragoza vs FC Andorra | 2.11 | 3.03 | 3.63 |
| 18:15 | 2797 | Ponferradina vs Huesca | 2.40 | 3.12 | 2.92 |
| 20:30 | 3366 | Las Palmas UD vs Burgos | 1.68 | 3.35 | 5.32 |
| 20:30 | 4536 | Racing Santander vs Alaves | 2.87 | 2.92 | 2.57 |
| 20:45 | 4106 | Bayer Leverkusen vs Brugge | 1.57 | 4.26 | 4.75 |
| 20:45 | 4595 | Porto vs Atletico Madrid | 2.47 | 3.26 | 2.72 |
| 22:00 | 2188 | Crewe vs Leeds United U21 | 1.75 | 3.90 | 3.66 |
| 22:45 | 1338 | Morecambe vs Derby | 4.37 | 3.58 | 1.75 |
| 22:45 | 1344 | Chesterfield vs Gateshead | 1.54 | 4.15 | 5.13 |
| 22:45 | 1401 | Lincoln vs Accrington | 2.26 | 3.37 | 2.93 |
| 22:45 | 1951 | Eastleigh vs Scunthorpe | 1.80 | 3.61 | 3.96 |
| 22:45 | 2241 | Barnet vs Southend | 2.77 | 3.46 | 2.30 |
| 22:45 | 2282 | Torquay vs Aldershot | 2.53 | 3.32 | 2.58 |
| 22:45 | 2323 | Notts County vs Bromley | 1.50 | 4.24 | 5.52 |
| 22:45 | 2469 | Wycombe vs Port Vale | 2.10 | 3.31 | 3.31 |
| 22:45 | 2570 | Oxford Utd vs Fleetwood Town | 1.87 | 3.46 | 3.91 |
| 22:45 | 2580 | Maidstone vs Solihull Moors | 3.55 | 3.79 | 1.85 |
| 22:45 | 3657 | Luton Town vs Reading | 1.94 | 3.31 | 3.81 |
| 22:45 | 3923 | Altrincham vs Wealdstone | 1.89 | 3.56 | 3.65 |
| 22:45 | 4115 | Woking vs Yeovil | 1.65 | 3.80 | 4.64 |
| 22:45 | 4164 | Portsmouth vs AFC Wimbledon | 1.50 | 4.10 | 5.27 |
| 22:45 | 4265 | Coventry vs Blackburn | 2.39 | 3.18 | 2.88 |
| 22:45 | 4352 | Halifax vs Dorking Wanderers | 2.01 | 3.55 | 3.26 |
| 22:45 | 4422 | Preston vs Swansea | 2.36 | 3.23 | 2.88 |
| 22:45 | 4517 | Hull City vs Middlesbrough | 2.93 | 3.23 | 2.33 |
| 22:45 | 4572 | Wrexham vs Maidenhead U | 1.29 | 5.34 | 8.31 |
| 22:45 | 5179 | Barrow vs Colchester | 1.81 | 3.41 | 4.26 |
| 22:45 | 5250 | Tranmere vs Stockport | 2.81 | 3.06 | 2.52 |
| 23:00 | 1703 | Rangers vs Ajax | 3.67 | 3.82 | 1.83 |
| 23:00 | 1820 | Bristol City vs Sheffield Utd | 3.02 | 3.47 | 2.17 |
| 23:00 | 2761 | Viktoria Plzen vs Barcelona | 8.32 | 5.43 | 1.29 |
| 23:00 | 2987 | Bayern Munchen vs Inter | 1.40 | 4.96 | 6.15 |
| 23:00 | 3946 | Sporting Lisbon vs Eintracht Frankfurt | 2.30 | 3.36 | 2.87 |
| 23:00 | 4135 | UD Ibiza Eivissa vs Leganes | 2.93 | 3.03 | 2.44 |
| 23:00 | 4298 | West Bromwich vs Blackpool | 1.68 | 3.71 | 4.65 |
| 23:00 | 4944 | Liverpool vs Napoli | 1.73 | 4.06 | 3.91 |
| 23:00 | 5417 | Marseille vs Tottenham | 2.83 | 3.38 | 2.32 |
| 23:30 | 1590 | Deportes Recoleta vs Magallanes | 5.85 | 3.80 | 1.50 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Novemba 1, 2022

Nipashe




Rashford alizungumzia bao la 100 UKURASA 29

KASI ZAIDI...



Beki wa Kulia wa Mtibwa Sugar, Franck Kahole, akilazimika kutumia mikono baada ya kuzidiwa kasi na winga wa Simba, Agustine Okrah, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa Simba kushinda 5-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Mgunda atoa siri ya ‘gharika’ Mtibwa Sugar

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HUKU akiwapongeza wachezaji wake kwa kupambana kiume na kufanikiwa kuichapa Mtibwa Sugar mabao 5-0, Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, ametoa siri ya ushinda huo ulioweka rekodi ya mabao mengi zaidi tangu kuanza kwa msimu huu.

Tangu Ligi Kuu ilipoanza hakuna timu yoyote iliyoshinda idadi hiyo ya mabao, huku matokeo ya idadi kubwa ya mabao kabla ya mechi hiyo ilikuwa ni Simba yenyewe kuifunga Geita Gold mabao 3-0, lakini ikaifunga Dodoma Jiji mabao 3-0, Mtibwa Sugar kuifunga Ihefu mabao 3-1, Yanga kuichapa Mtibwa Sugar mabao 3-0.

Simba iliipa Mtibwa Sugar kipigo kama hicho cha mabao 5-0 msimu wa 2020/21 kwenye uwanja huo huo, Aprili 15, 2021 mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, yakiwekwa wavuni na Clatous Chama, Rally Bwalya, Luis Miquissone na Medie Kagere aliyefunga magoli mawili.

Katika mechi ya juzi, mabao ya Simba yalizamishwa nyavuni na Mzamiru Yassin dakika ya 38, Pape Sakho (dk. 48 na 90), Augustine Okrah (dk. 63) na Mosses Phiri.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Mgunda alisema anawashukuru wachezaji wake kufanya mipango yao ya mchezo huo na kufanikiwa kupata ushindi huo mnono.

Alisema baada ya kupoteza mechi iliyopita dhidi ya Azam FC, alikaa na wachezaji ili kuwaandaa kisaikolojia na kuwaweka tayari kwa mchezo na hatimaye kupata ushindi mnono dhidi ya Mtibwa Sugar.

“Sasa tunajipanga na mechi ijayo ugenini dhidi ya Singida Big Stars, nakiri nilipoteza mechi ya Azam FC, kocha yeyote anayepoteza mechi yuko

INAENDELEA UK. 31

# Yanga yaapa kuimaliza mechi CAF kwa Mkapa

**Na Waandishi Wetu**

### ●●● Wachezaji wautaka mchezo huo, wajipanga ndani na nje ya uwanja, kocha asema...

WAKATI kwa sasa saa zikihesabika kabla ya Yanga kushuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Club Africain ya Tunisia kwenye mechi ya mchujo kusaka timu itakayotinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, klabu hiyo imesema inataka kuimaliza mechi hiyo nyumbani kwa kupata ushindi wa mabao mengi ili isiwe na kibarua kizito inapokwenda ugenini.

**Yanga imeingia kambini jana kuendelea na mazoezi ya kujiimarisha ili kukamilisha mpango wao wa kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho baada ya kushindwa kufurukuta Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema anaimani kubwa timu yao itasonga mbele na kwa kuanza kesho watahakikisha wanapata matokeo chanya.

Alisema kikosi kipo vizuri na wanaendelea kufanyia kazi madhaifu yaliyojitokeza katika michezo iliyopita ili kutojirudia katika mechi yao dhidi ya Club Africain.

Kaze alisema wana wachezaji wazuri na wenye uwezo mkubwa wa kufanya vizuri kwenye mashindano yaliyoko mbele yao ikiwamo mechi yao ya kimataifa dhidi ya klabu hiyo kutoka Tunisia.

Alisema wamewapa wachezaji mbinu ambazo zitawasaidia pamoja na mazoezi ya nguvu wakiwa na lengo la kufuzu kuingia hatua hiyo ya makundi.

“Leo (jana) jioni tutaanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu wa Jumatano, tuliwapa wachezaji mapumziko ya siku moja ili miili yao ipumzike baada ya uchovu wa safari ya Mwanza,” alisema.

Wakati Kaze akieleza hayo, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema jana kuwa safari hii ni lazima watumie faida ya kucheza nyumbani kuhakikisha wanapata ushindi mnono ili kujiweka kwenye mazingira mazuri katika mechi ya marudiano.

“Yanga tunautaka huu mchezo, hatutaki kuzungumza sana safari hii, hatutaki maneno mengi, zaidi ya vitendo, wachezaji wako tayari kupambana, wachezaji wetu waliumia sana baada ya kupoteza mchezo na kutolewa dhidi ya Al Hilal, sasa wanataka kwenda kupambana, kuonyesha ni kiasi gani waliumizwa na matokeo ya mechi ile ya Ligi ya Mabingwa.

“Lazima tutumie vizuri faida ya kucheza nyumbani safari hii ili tusiwe na kazi kubwa ugenini, ndiyo maana nasema safari hii tuache maneno, vitendo vitasema,” alise-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >